# Nipashe

Alhamisi Januari 31, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579829

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

ww.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13



## Timu kuundwa kuchunguza mauaji ya watoto 10 Njombe

UKURASA 2

# Shule kongwe wasoma chini ya mwembe

- **Ilianzishwa** mwaka 1946, mwalimu mkuu, walimu wabanana ofisi moja
- **Ofisa** elimu, Kaimu DED wageuka 'mabubu'... *Endelea ukurasa wa 2*



Wanafunzi wa darasa la tatu katika Shule ya Msingi Nakalola Kata ya Mkundi, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara, wakisoma chini ya mti kutokana na kukabiliwa na ukosefu wa vyumba vya madarasa kwa muda mrefu. **PICHA: HAMISI NASIRI**

## Mvumbuzi tanzanite afariki dunia

UKURASA 3

## Neema wakulima korosho mnunuzi mkubwa ajitokeza

UK. 3

**MICHEZO** **SIMBA MIKONONI SALAMA MISRI** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Wanafunzi shule kongwe wasomea chini ya miembe

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

WANAFUNZI 108 wa darasa la pili na la tatu katika Shule Msingi Nakalola, wilayani Masasi, wanasomea chini ya miti ya miembe kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa.

Shule hiyo kongwe iliyoanzishwa mwaka 1946, kwa sasa ina chumba kimoja cha ofisi ya walimu jambo ambalo walimu wa kawaida na mwalimu mkuu hulazimika kukaa kufanya kazi kwenye chumba hicho kwa pamoja jambo ambalo ni kinyume cha sera ya elimu inavyotaka mwalimu mkuu kuwa na ofisi yake binafsi.

Hayo yalibainishwa juzi na Kaimu Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Rashidi Tumaini, alipokuwa akizungumza na Nipashe shuleni hapo juu ya changamoto zinazoikabili shule hiyo.

Alisema miundombinu ya majengo si rafiki kwa wanafunzi na walimu wanaofundisha shuleni hapo licha ya viongozi mbalimbali wa serikali na chama kutembelea mara kadhaa na kujionea changamoto hizo.

Tumaini alisema kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa, wanafunzi wa darasa la kwanza, la tatu na wale wa awali, wanasomea chini ya miembe, hali inayosababisha hata ufundishaji kwa walimu kuwa mgumu.

Pia alisema hata uwelewa wa masomo kwa wanafunzi wenyewe unakuwa mdogo kutokana na miundombinu hiyo kutokuwa rafiki kwa wao.

Alisema tatizo hilo la wanafunzi wa madarasa hayo kusomea chini ya miembe ni la kila mwaka na linawaathiri wanafunzi wengi kisaikolajia hasa kushindwa kusoma kwa utulivu na ufasaha na mvua ikinyesha husitisha masomo kwa

INAENDELEA UK. 8



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimjulia hali Mbunge wa Misungwi, Charles Kitwanga, aliyelazwa katika Hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

## Wadau wanena muswada Sheria ya Vyama vya Siasa

**Na Mary Geofrey**

ASASI ya kiraia inayojihusisha na masuala ya kijamii na utetezi wa haki za binadamu (Ador), imesema kupitishwa kwa muswada wa marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, utawezesha kuwapo na ukomo wa madaraka kwa viongozi wa upinzani.

Vilevile, imesema ruzuku zinazotolewa na serikali kwa vyama vya siasa, zitadhibitiwa ili zitumike kufanya shughuli za maendeleo badala ya kunufaisha baadhi ya viongozi wa vyama.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Mkurugenzi wa Ador, Habibu Shaibu, alidai muswada huo utaondoa ukiritimba uliokuwapo ndani ya vyama vya upinzani nchini.

"Sioni sababu ya vyama vya upinzani kuuzungumzia vibaya muswada huu, hauna lengo la kukandamiza vyama vya siasa. Ninachoona chenye manufaa na ambacho viongozi walio waroho wa madaraka wanakiogopa, ni kuwapo na

INAENDELEA UK. 8


KUMBUKUMBU

MAMA AMOROPARADISO MASHOO.

Ni miaka 30 tangu ulipotutoka Januari 1989 – Januari 2019. Unakumbukwa kwa upendo mwingi na watoto wako: Eonike, Hellen, Filister, Geoffrey, Erene na Filimina.

JINA LA BWANA LIHIMIDIWE!


## MAUAJI WATOTO 10:

# IGP kuunda timu ya uchunguzi

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, amemtaka Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, kuunda timu kutoka makao makuu itakayokwenda kushirikiana na wapelelezi wa Mkoa wa Njombe kuchunguza matukio ya mauaji dhidi ya watoto 10 mkoani humo.

Masauni alitoa agizo hilo jana, akiwa wilayani Njombe baada ya kukutana na waganga wa kienyeji kuzungumzia matukio ya mauaji dhidi ya watoto, yaliyohusishwa na imani za kishirikina.

Alisema timu ya IGP inatakiwa kuchunguza matukio yote ya mauaji mkoani humo na kuhakikisha wahusika wanakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

"Agizo la pili IGP ahakikishe timu itakayotoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, inachunguza tukio la jana (juzi), lililosababisha polisi kutumia nguvu kwa kupiga mabomu ya machozi ili kutawanya wananchi, uchunguzi ujikite kubaini kiini na uwiano wa nguvu iliyotumika kuhusu uhalisia wa tukio," Masauni aliagiza.

Juzi, wakati naibu waziri huyo akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Njombe kwenye Viwanja vya Turbo, ghafla kulisikika milio ya mabomu ya machozi jirani na mkutano huo, kitendo ambacho kilisababisha taharuki na kusimama kwa mkutano huo.

Taarifa mbili zilizotolewa kwa Masauni kuhusu tukio hilo zilikinzana na kumfanya naibu waziri huyo kutaka uchunguzi ili kama amedanganywa, polisi wawajibike.

Katika agizo lake la tatu jana, Masauni aliitaka Jeshi la Polisi Mkoa wa Njombe kuongeza operesheni katika maeneo yote hususani kwenye mapori na misitu na kuhakikisha linakusanya taarifa za kiintelijensia ili kukomesha matukio hayo.

Kiongozi huyo wa serikali pia aliwataka Watanzania kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo, ili kukomesha vitendo vya uhalifu kwenye maeneo yao.

Masauni pia aliwataka wananchi kuacha tabia ya kuchukua sheria mkononi, badala yake watoe nafasi kwa polisi ili kuwalinda pindi yanapotokea matukio mbalimbali ya uhalifu.

Mwanzoni mwa wiki hii, iliripotiwa kuwa watoto 10 wameuawa mkoani Njombe na kuzua taharuki ambayo ililazimu Masauni kwenda mkoani humo na kuzungumza na wananchi kuhusu matukio hayo.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, akisalimiana na wavuvi katika Soko la Kimataifa la Samaki Feri Dar es Salaam juzi, baada ya kusikiliza malalamiko yao kuhusiana na operesheni ya kudhibiti uvuvi haramu katika Bahari ya Hindi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Neema wakulima korosho mnunuzi mkubwa ajitokeza

**Na John Ngunge,** ARUSHA

NI neema kwa wakulima wa korosho. Ndivyo unavyoweza kusema baada ya Kampuni ya Indopower Solutions ya Kenya kuwa itanunua tani 100,000 za korosho kwa Sh. bilioni 418, fedha ambazo zitalipwa ndani ya siku saba kuanzia jana.

Mkataba wa mauziano ulitiwa saini jana, kwenye ukumbi wa mikutano wa Ofisi za Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kati ya Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Hussein Mansoor na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Indopower Solutions, Brian Mutembei.

Hafla hiyo ilishuhudiwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, Waziri wa Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda, Naibu Waziri wa Kilimo, Innocent Bashungwa, Gavana wa Benki Kuu Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga, makatibu wakuu wa wizara hizo na Balozi wa Kenya nchini, Dan Kazungu.

Akizungumza kabla ya kuweka saini, Prof. Kabudi, alisema mauziano hayo yataipatia Tanzania Sh. bilioni 418 kama bei ya jumla na kwamba fedha hizo zitaingizwa BoT moja kwa moja. Alimshukuru Rais John Magufuli kwa kuchukua uamuzi wa kununua korosho zote moja kwa moja kutoka kwa wakulima na kusaka mnunuzi mkubwa wa zao hilo. Kwa upande wake, Waziri wa Viwanda Kakunda (Kakunda), alisema kampuni ya Indopower Solutions ni kati ya kampuni 18 zilizoonyesha nia ya kununua kiasi hicho cha korosho ghafi. Zingine hazikufanikiwa kukidhi masharti.

"Hii ni biashara ya faida, ambayo taifa limenufaika na wakulima pia wamenufaika," Kakunda alisema.

Aliongeza kuwa kuuzwa kwa kiwango hicho cha korosho kunafanya korosho ambazo zimebaki kwenye ghala kuwa tani 63,000.

Awali, Naibu Waziri wa Kilimo (Bashungwa), alisema Novemba 12, mwaka jana, Rais Magufuli, alilazimika kuingilia kati minada ya korosho, baada ya kuona wanunuzi wanaweka bei ya chini kwa lengo la kuwaumiza wakulima.

Alimshukuru Rais Magufuli kwa kutoa bei elekezi ya Sh. 3,300 kwa kilo ambazo zitamnufaisha mkulima.

# Askari polisi ajeruhiwa na ng'ombe, alazwa hospitali ya Muhimbili

**Na Mwandishi wetu,** LINDI

ASKARI Polisi wa Kituo cha wilaya ya Lindi mkoani hapa, Mosens Koyombo, amejeruhiwa vibaya na kukimbizwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili Jijini Dar es Salaam baada ya kugonga ng'ombe mwishoni mwa wiki.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Pidensian Protas, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kwamba askari huyo anadaiwa kupata ajali hiyo Januari 26, mwaka huu saa 11:0 alfajiri.

Kwa mujibu wa mashuhuda akiwamo mchungaji wa mifugo hiyo, Shamshi Swaibu, siku hiyo ya tukio akiwa na wenzake wawili aliyewataja kwa majina ya Said Selemani na Mathayo, walikuwa wanaswaga ng'ombe hao kupelekwa machinjioni kwa ajili ya kuchinjwa.

Swaibu alisema wakiwa wanawavusha ng'ombe hao kwenye baarabara kuu ya Kibiti-Lindi, walisikia milio ya pikipiki, hivyo kulazimika kuwasha tochi ikiwa ni ishara ya kumtahadharisha apunguze mwendo.

Alisema kutokana na pikipiki yake kutokuwa na mwanga wa kutosha na mwendo kasi, dereva huyo wa pikipiki alishindwa kutii Ishara aliyokuwa anaonyeshwa na hatimaye kugonga ng'ombe mmoja katikati ya kundi la mifugo hiyo waliokuwa wakipelekwa machinjioni eneo la makalioni na kumvunja mguu.

"Tuliposikia mlio wa pikipiki inakuja tulimuashia tochi kumpa tahadhari, lakini kutokana na mwendo kasi aliokuwa akitembea, alishindwa kupunguza na kumgonga ng'ombe sehemu ya makalioni na kuvunjika mguu," alisema Swaibu.

Swaibu alisema kufuatia tukio hilo, mfanyabiashara wa mbuzi aliyetajwa kwa jina la Abdallah, alisaidia kutoa taarifa kwa afisa mifugo anayesimamia uchinjaji, Rashidi Buna, ambaye alifika eneo la tukio na kumkuta askari huyo akiwa hoi hajitambui kutokana na maumivu makali aliyoyapata.

Nipashe ilipomtafuta Buna alikiri kupewa taarifa na mfanyabiashara huyo wa mbuzi, na alipokwenda eneo la tukio alimkuta askari huyo akiwa na sare zake za kazi akiwa amechanika eneo la kichwani sehemu ya usoni pamoja na kuvuja damu na masikioni.

Buna alisema kabla ya kupiga simu ya kuwataarifu askari wenzake, alimsogeza kutoka barabarani alipoangukia na kumweka kando, kisha kumpigia simu askari mwenzake aliyemtaja kwa jina la Gabbo.

# Mvumbuzi tanzanite afariki dunia

**Na Romana Mallya**

MVUMBUZI wa madini ya tanzanite, Mzee Jumanne Ngoma (85), amefariki dunia katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MHN) muda mfupi baada ya kufikishwa hapo.

Aprili 6, mwaka jana, Rais John Magufuli, alitangaza kumtambua Mzee Ngoma kuwa ndiye mvumbuzi wa madini hayo na alimpatia Sh. milioni 100, ili zimsaidie kwenye matibabu kutokana na maradhi yaliyokuwa yakimsumbua.

Rais Magufuli alitangaza kumtambua mzee huyo akiwa mji mdogo wa Mirerani ulioko Simanjiro mkoani Manyara, wakati akizindua ukuta uliozunguka machimbo ya madini ya tanzanite, uliojengwa na kikosi cha majeshi ya ulinzi.

Akizungumza na Nipashe jana jioni, mtoto wa marehemu, Hassan Ngoma, alisema baba yake alifariki dunia siku hiyo baada ya kufikishwa chumba cha dharura akitolewa Hospitali ya Boch iliyoko Kimara jijini Dar es Salaam.

Hassan alisema baba yake alikuwa akisumbuliwa na maradhi ya kiharusi.

"Baba yetu alilazwa jana (juzi) Hospitali ya Boch, Kimara na ilipofika mchana alihamishiwa Muhimbili, lakini wakati akiwa chumba cha dharura Muhimbili majira ya saa 7:00 mchana alifariki dunia," alisema.

Hassan alisema wakati huo akizungumza na gazeti hili walikuwa wamemaliza taratibu za kumhifadhi kwenye chumba cha kuhifadhia maiti hospitalini hapo.

"Utaratibu unaofuata hivi sasa ni kwamba jioni ya leo (jana) tutakuwa na kikao kitakachofanyika kwa kaka yetu mkubwa huko Mbezi Kimara, ambacho kitaamua lini atasafirishwa kwa ajili ya mazishi kama unavyojua mzee wetu alipewa heshima kubwa na Rais Magufuli baada ya kutambuliwa kuwa ndiye mvumbuzi wa tanzanite," alisema.

Baada ya Rais Magufuli kumkabidhi mzee Ngoma fedha hizo zilitumika kwa ajili ya matibabu, ambapo alipelekwa nchini India na baadaye kurejea Tanzania.

Alipokuwa akizindua ukuta wa Mirerani uliojengwa kwa Sh. 5,645,843,163, Rais Magufuli aliahidi kuandika barua maalum ya kumtambua Mzee Ngoma.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Rais Magufuli, alisema alipata ujumbe mfupi na baadaye kupata taarifa kutoka kwa mtoto wake, Hassan Ngoma na alipofuatilia alibaini ni za kweli. "Nimeambiwa tangu mwaka 1967 madini haya yaligunduliwa na mzee huyu, lakini pamoja na kutambuliwa na Rais wa Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere, kwenye barua niliyoiona iliyosainiwa tangu tarehe 3/8/1980 na nakala yake ya kuvumbua madini ya aina ya pekee na kuyapeleka kwa mtaalamu wa madini na miamba mwaka 1967, barua hiyo nayo ninayo hapa," alisema Rais Magufuli wakati huo.

INAENDELEA UK. 8

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
**40470DODOMA,**

28 Januari, 2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumatatu** tarehe **04/02/2019** kampuni ya **Mainline carriers Limited** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar es Salaam Port** kuelekea **Tunduma**, gari hilo lenye namba za usajili:

**T653DFA/T245BYM**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 20.0 |
| Upana | - | mita | 4.3 |
| Kimo | - | mita | 4.6 |

3. Njia itakayotumika: **Dar es Salaama Port hadi Tunduma Kupitia Mikumi,**

gari litasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

# HABARI KITAIFA


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

CHUO CHA MAFUNZO YA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVUKAZI (ATTI) – MBEYA

**TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI KWA WAHANDISI, MAFUNDI SANIFU NA MAKANDARASI WA BARABARA**

**1. Utangulizi:**
Chuo cha Mafunzo ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi "Appropriate Technology Training Institute" (ATTI-MBEYA) ni Chuo cha Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kinawatangazia wananchi wote kuwa kinatarajia kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe na Lami kwa Kutumia Tekinolojia Stahiki ya Nguvukazi. Kozi hizi zimepangwa kufanyika kwa nyakati tofauti kama ifuatavyo: -

| Na. | JINA LA KOZI | MUDA NA TAREHE | MAFUNZO YATAFANYIKA |
|---|---|---|---|
| 1. | Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | Wiki Kumi (10)<br>08/04/2019 - 14/06/2019 | ATTI- Mbeya |
| 2. | Kozi ya ujenzi wa Lami ("Bituminous Surfacing for Low Volume Roads"), kwenye barabara za mijini na vijijini kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | Wiki Nne (4)<br>02/09/2019 – 27/09 /2019 | ATTI- Mbeya |

**2. Malengo ya Kozi na Masomo Yatakayofundishwa: -**

(a) Kozi ya Mafunzo ya Barabara za Changarawe: Masomo yatakayofundishwa kwa kozi hii ni ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi, mpango wa kazi (Planning), Uongozi sehemu za kazi na mbinu za usimamiaji wa kazi, vipimo vya kazi, usimamiaji wa mikataba, Uwekaji wa changarawe, ujenzi wa makalavati pamoja na mafunzo ya kujenga barabara kivitendo. Mafunzo haya yatamwezesha mshiriki kuweza kufanya kazi za ukarabati na matengenezo ya barabara kwa ubora unaotakiwa. Kwa wajasiriamali masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi "SPECIALIST LABOUR BASED CONTRACTORS" daraja la tatu na kuweza kusajiliwa na bodi ya usajili wa makandarasi (CRB).

(b) Kozi ya Mafunzo ya Barabara za Lami: Masomo yatakayofundishwa ni aina mbalimbali za lami, aina mbalimbali za barabara za lami, aina mbalimbali za viunzi (materials) kwa barabara za lami, kuunda na kutengeneza tabaka la lami (Design of Surface Dressing), kuziba viraka (Pothole Repair in Surface Treatment Pavement), kuziba mipasuko (crack sealing), aina ya Vifaa na mitambo kwa kazi za lami, Usalama kazini, mafunzo haya pia yatahusu mafunzo ya kujenga barabara ya lami kivitendo. Masomo haya yatamwezesha mshiriki kuweza kufanya kazi za lami, kusanifu na kuunda barabara ya lami "Design of surface dressing".

**3. Walengwa wa Mafunzo haya ni:-**

a) Wahandisi wa barabara toka TANROADS, TARURA na Wakandarasi,
b) Mafundi Sanifu wa Barabara toka TANROADS, TARURA na Wakandarasi,
c) Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi nchini,
d) Makandarasi wenye nia ya kujenga uwezo wa kazi zao za matengenezo ya barabara kwa kutumia Tekinolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
e) Watu binafsi wenye uzoefu wa kazi za barabara na wanaotaka kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

**4. Gharama za Mafunzo:-**
Gharama ya mafunzo ni **Tshs. 1,000,000/=** kozi ya Lami na **Tshs. 1,600,000/=** Kozi ya Changarawe. Malipo ya ADA ya ushiriki yalipwe kabla ya kozi kuanza kwa: **"Principal ATTI, NBC Tukuyu, A/c No.038101001741",** tunashauri yalipwe kabla ya wiki mbili na wasilisha hati ya malipo (Bank Slip) unapowasili kwenye kituo cha kozi husika.

**5. Namna ya Kutuma Maombi ya Kozi hizi:-**
Wale wote watakaokuwa tayari kutaka kujiunga na kozi hii wanaombwa kutuma maombi yao Chuoni ATTI – MBEYA kwa kutumia anuani ya Chuo hapa chini na kupitia E-mail na simu zilizoonyeshwa, ili tuweze kuwaingiza kwenye orodha ya washiriki. Kwa kozi hizi kuna nafasi ishirini (20) tu kwa kila kozi; hivyo, wahi mapema kutuma maombi yako.

**Mkuu wa Chuo,**
**ATTI – Mbeya,**
**S.L.P 1957, MBEYA,**
**Tel: +255 732 951 524/717**
**Mob: +255 655 274 280.**
**Fax: +255 732 950 399**
**E-mail: attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com, sangoatti@yahoo.com, frankkisandu@gmail.com**


# MOI yachunguza moyo kwa MRI

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), kwa mara ya kwanza imefanya uchunguzi wa kibobezi wa moyo kwa kutumia kipimo cha MRI.

Uchunguzi huo umefanywa kwa ushirikiano kati ya madaktari bingwa wa radiolojia wa MOI, wataalamu wa radiolojia wa MOI na Muhimbili na Profesa Paul Suranyi kutoka Chuo Kikuu cha South Carolina cha Marekani. Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, akizungumza jana kuhusu kipimo hicho, alisema ni hatua kubwa katika kutoa huduma za uchunguzi kwa kutumia kifaa hicho kwa lengo la kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora na za kibobezi.

"Kwa kweli hii ni hatua kubwa kwa taasisi yetu, pia nitumie nafasi hii kuishukuru serikali kutuwezesha kuwa na vifaa vya kisasa vya uchunguzi hususani hiki cha MRI ambacho ni muhimu sana kwa huduma zetu. Pia miwashukuru wataalamu wetu ambao wamewezesha uchunguzi huu wa kipekee kufanyika kwa mara ya kwanza hapa nchini," alisema Dk. Boniface.

Aliongeza kuwa lengo la taasisi hiyo ni kuhakikisha huduma zote za upasuaji, uchunguzi na maabara zinapatikana kwa ubora wa hali ya juu, ili wananchi kutoka mataifa mbalimbali waendelee kuja nchini kupata huduma.

Naye Daktari Bingwa wa Radiolojia wa MOI, Dk. Joel Bwemelo, alisema ni heshima kubwa kwao kufanikisha uchunguzi huo ambao haukuwahi kufanyika hapo awali na umefanyika kwa mafanikio makubwa.

"Ziko njia nyingi za uchunguzi wa magonjwa ya moyo baadhi ni njia ya kutumia 'ultrasound' na 'cath lab' ambazo ndizo zinazotumika kwa asilimia kubwa kwa sasa nchini. Njia hii ya kutumia MRI ni nzuri kwa sababu inapunguza athari kwa mgonjwa kwa kuwa haitumii mionzi na sisi wataalamu tunaweza kuliona tatizo vizuri zaidi na kwa ufasaha mkubwa ukilinganisha na njia nilizozitaja," alisema Dk. Bwemelo.

Kwa upande wake, mshiriki wa uchunguzi huo, Dk. Rahma Hingora, ambaye pia ni bingwa wa radiolojia ameipongeza serikali kwa kuhakikisha vifaa vya uchunguzi vya MRI na CT Scan vinakuwapo, ili kuwahudumia wagonjwa ambao wamekuwa wakikosa huduma hizo nchini. Dk. Hingora alisema uwapo wa vifaa vya kisasa na wataalamu wabobezi pamoja na ushirikiano na taasisi mbalimbali duniani umewezesha utoaji huduma kwa mafanikio.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu (wa pili kulia), akipewa maelekezo na Ofisa Misitu, John Mtika, kuhusu hatua za miche ya miti ya miembe inavyokuwa, wakati alipotembelea ofisi za kurugenzi ya uzalishaji miche ya miti mkoani Morogoro jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Kurugenzi hiyo, Edgar Masunga. **PICHA: WMU**

# Maofisa jiji watumbuliwa kwa tuhuma za ubadhirifu

**Na Dege Masoli,** TANGA

VIGOGO wawili wa Halmashauri ya Jiji la Tanga wameshushwa vyeo kutokana na makosa ya kinidhamu ikiwamo kusababisha hasara ya Sh. milioni 18.

Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Madiwani, Mhina Mustapha, aliwataja watumishi hao na vyeo walivyokuwa navyo kuwa ni Flora Shija aliyekuwa Ofisa Maendeleo ya Jamii na Norbet Achiula aliyekuwa Kaimu Ofisa Michezo wa Jiji. Mustapha ambaye pia ni Meya wa Jiji hilo, alisema hatua dhidi ya tuhuma za watumishi hao ni za kinidhamu, udanganyifu na ubadhirifu wa fedha za umma.

Alisema ofisa maendeleo ya jamii amekumbwa na tuhuma za kuunda vikundi viwili ambavyo ni hewa vinavyoonyesha kuvilipa Sh. milioni sita, huku kaimu ofisa michezo akikabiliwa na tuhuma ya upotevu wa Sh. milioni 12.

Katika kikao hicho cha kamati ya nidhamu ya watumishi, alisema watu hao wawili wameshushwa vyeo vyao na kurudi kwenye utumishi wa kawaida, huku wakitakiwa kila mmoja kurejesha fedha anazodaiwa na halmashauri hiyo.

Wakati huo huo, Meya huyo alitoa wito kwa watumishi wa halmashauri, wakiwamo watendaji kata kusimamia kwa weledi utekelezaji wa majukumu yao, ili kutekeleza azima ya halmashauri ya ukusanyaji wa mapato na kuihudumia jamii.

Aliahidi kutembelea kata zote kwa lengo la kufanya ukaguzi wa ukusanyaji wa mapato ya halmashauri, huku akihakikisha utekelezaji wa maelekezo ya halmashauri unafuatwa na kuleta tija.

Naye Mkurugenzi wa Jiji la Tanga, Daudi Mayeji, aliahidi kutekeleza maagizo ya kamati na kutoa taarifa ya utekelezaji katika kikao cha baraza lijalo.

## HABARI KITAIFA



Naibu Meya wa Manispaa ya Ilala, Omary Kumbilamoto (kulia), akimsikiliza Mwenyekiti wa kikundi cha Umoja wa Wanakijiji wa Masawi Kondoa, waishio Dar es Salaam (Uwakimawada), Dellow Bakari, wakati wa ufunguzi wa tamasha la wajasiriamali lililoandaliwa na Guru Planet, lililofanyika jijini juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Samia atoa neno Bodi ya NEMC

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amewahakikishia Watanzania kwamba ana imani na bodi mpya ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) pamoja na uongozi wake, na kwamba ni timu zitakazoleta madadiliko chanya katika kutekeleza sheria ya mazingira na sheria nyingine za nchi.

Alitoa kauli hiyo wakati akifunga mkutano wa wadau wa sekta ya madini.

Makamu alisema ana imani na bodi mpya ya NEMC na uteuzi wa Dk. Samuel Gwamaka na kumtaka asimame ili wajumbe wa mkutano huo wamuone na hatimaye wamtumie.

Makamu aliwaambia wajumbe kwamba anaamini bodi na uongozi wa baraza ni vikosi mahususi vya kuleta mabadiliko.

"Nina imani na uongozi na bodi, wana uwezo wa kusimamia NEMC, mabadiliko mengi yatafanyika chini ya NEMC mpaya. Mkurugenzi Mtendaji mpya ana uwezo mkubwa wa kuleta mabadiliko katika taasisi hiyo akishirikiana na bodi," alisema.

INAENDELEA UK. 8

# Waziri ataka wananchi wachangie miti

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameahidi kufuatilia ugawaji wa miche ya miti bure kwa wananchi iliyooteshwa na Kurugenzi ya Uzalishaji Miche ya Miti.

Imeelezwa kuwa uzoefu uliopo unaonyesha vitu vingi ambavyo serikali imekuwa ikivigawa bure kwa kananchi bila wananchi hao kuchangia gharama yoyote, hushindwa kuthaminiwa hivyo kutoleta matokeo chanya.Ka yasu alitoa kauli hiyo jana mkoani Morogoro alipotembelea ofisi za kurugenzi hiyo kwa lengo la kujua imejipangaje kuzalisha miche za miti yenye ubora ikiwamo ya mbao na ya matunda ambayo itasambazwa nchi nzima.

Alisema utaratibu huo itabidi uangaliwe upya kwa vile ni ngumu kwa wananchi wengi kuitunza kwa sababu hawasikii uchungu na wengi hujikuta wakiitupa au kuiacha bila kuimwagilia hadi inakufa.

"Ukichukua miche leo halafu ukaipeleka mkoani Shinyanga ukagawa bure yote, itaiwa na ng'ombe na vivyo hivyo ukaipeleka Dodoma yote itakufa kwa vile haitamwagiliwa maji kwa sababu ni ya bure,' alisema.

Naibu Waziri Alisema siku zote kitu cha bure hakithaminiwi, hivyo lazima kila Mwananchi achangie kidogo lakini isiwe bure kabisa.

Hata hivyo, Kanyasu alisema miche ya miti inaweza kutolewa bure kwa taasisi za umma kama vile shule ila kwa makubaliano maalumu lakini si kwa wananchi.

Aidha, aliitaka kurugenzi hiyo ijiendeshe kibiashara badala ya kujikita kutoa huduma kwa wananchi.

Katika hatua nyingine, Kanyasu aliiagiza kurugenzi hiyo ifungue utalii wa bustani wa miti na maua katika jiji la Dodoma ambao ni moja ya aina za utalii zinazopendwa hasa na wanamazingira.

Alisema miji kama Arusha na Mwanza imeanzisha utalii huo licha ya kuwa kumekosekana mwongozo wa kuziboresha bustani hizo lakini watalii wengi wamekuwa wakimiminika katika bustani hizo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Kurugenzi hiyo, Edgar Masunga, alisema maelekezo yote aliyoyatoa atayatekeleza na kumwahidi Naibu Waziri kuwa wanatarajia kuzalisha tani milioni tatu za miche ya miti katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha.

# Prof. Mchenga bosi mpya DSFA

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, amemteua Dk. Islam Seif Salum Mchenga, kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu (Deep Sea Fishing Authority – DSFA).

Taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, ilieleza jana kuwa uteuzi wa Dk. Mchenga ulianza Desemba 1, 2018 na kwamba kabla ya uteuzi huo alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Zanzibar.

Wakati huo huo, Rais Magufuli amemteua Dk. Emmanuel Andrew Sweke kuwa Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA).

Taarifa ilieleza kuwa uteuzi wa Dk. Sweke ulianza tangu Desemba 1, 2018 na kabla ya uteuzi huo alikuwa Ofisa Utafiti wa Uvuvi Mwandamizi na Kaimu Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Uvuvi Tanzania (Tanzania Livestock Research Institute - TAFIRI) – Kigoma.

Katika hatua nyingine, Rais Magufuli amemteua Prof. Sebastian Chenyambuga, kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI). Uteuzi wa Prof. Chenyambuga ulianza Januari 26, 2019.

Kadhalika, Rais Magufuli amemteua Prof. Justinian Rwezaula Ikingura, kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (Geological Survey of Tanzania - GST). Uteuzi wa Prof. Ikingura ulianza Januari 18, mwaka huu.


**MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA**

TFDA
Tanzania Food & Drugs Authority

**TANGAZO KWA UMMA**

22 Januari, 2019

**UTARATIBU MPYA WA KULIPIA HUDUMA ZA TFDA KUPITIA MFUMO WA SERIKALI WA GePG**

1. Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) inapenda kuwafahamisha wateja wake na wananchi kwa ujumla kuwa, kuanzia tarehe 1 Desemba 2018, imeanza rasmi kutumia mfumo wa malipo wa Serikali wa kielektroniki (Government e-Payment Gateway-GePG) kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348.
2. Malipo yote kwa huduma zitolewazo na TFDA yatafanyika kwenye akaunti za Mamlaka na kwa kuzingatia namba maalum ya utambuzi (Payment Control Number) zinazooneshwa kwenye ankara kifani (proforma invoice).
3. Huduma itatolewa baada ya malipo kukamilika kwa mujibu wa Kanuni za Ada na Tozo za mwaka 2015 na marekebisho yake ya mwaka 2017.
4. Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana nasi kupitia anuani ifuatayo;

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu**
**Mtaa wa Mwanza, Block T,**
**Kiwanja Na. 6, S.L.P. 1253,**
**DODOMA, Tanzania.**
**Simu (Landline): +255 26 320156**
**Simu (Mobile):+255 658 445222/+255 685 70173**
**Barua pepe: info@tfda.go.tz**
**Tovuti: www.tfda.go.tz**

**TFDA- Ofisi Ndogo**
Barabara ya Nelson Mandela, Mabibo-External,
S. L. P 77150, DAR ES SALAAM,
Simu; +255 222 450512/658 445222/777 700002
Nukushi; +255 222450793
Barua pepe; info@tfda.go.tz
Tovuti; www.tfda.go.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Matumizi ya ovyo viboko shuleni sasa yadhibitiwe

**SERIKALI** imeshapiga marufuku walimu kuwachapa viboko wanafunzi na kutoa mwongozo na maelekezo kuhusiana na adhabu ya viboko shuleni.

Marufuku hiyo ya serikali ilitokana na matumizi mabaya ya adhabu ya viboko kwa baadhi ya walimu na matokeo yake ni kuwasababishia wanafunzi athari.

Kuna matukio kadhaa ambayo baadhi ya walimu waliwapa adhabu ya viboko na kujeruhiwa. Wako pia waliowaadhibu kwa voboko na kuwasababishia vifo.

Kutokana na matukio hayo ndipo serikali kupitia wizara yenye dhamana na elimu ilipoamua kupiga marufuku matumizi ya viboko shuleni pamoja na kutoa maelekezo na mwongozo.

Kwa mujibu wa mwongozo huo, wanaoruhusiwa kutumia adhabu ya viboko ni walimu wakuu au mwalimu yeyote kwa kibali cha walimu wakuu.

Mwongozo huo uliwekwa ili kuweka udhibiti katika matumizi ya ovyo ya viboko ili kuepusha uwezekano wa kusababisha athari kwa wanafunzi kama tulivyoeleza awali.

Katika kusisitiza hilo, wizara pia hivi karibuni ilitangaza kwamba walimu hawaruhusiwi kutembea na viboko wawapo katika maeneo ya shule. Bila shaka lengo ni kuwafanya wanafunzi wayaone mazingira ya shule na walimu kuwa ni rafiki kwao.

Licha ya mafuruku hiyo, kuna matukio yanayoendelea ambayo yanatoa picha kwamba baadhi ya walimu hawaheshimu marufuku ya serikali kuhusu adhabu ya viboko kwa wanafunzi. Tunaendelea kusikia katika shule kadhaa kuwa walimu wamewachapa wanafunzi na kuwasababishia majeraha makubwa.

Miongoni mwake ni tukio la wiki hii lililotokea mkoani Shinyanga, ambapo iliripotiwa kuwa mwanafunzi anayesoma kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Bugarama, Halmashauri ya Msalala, amelazwa katika Kituo cha Afya Bugarama baada ya kupigwa viboko na mwalimu wake sehemu mbalimbali za mwili hadi kupoteza fahamu.

Tukio hilo lilitokea Januari 25, mwaka huu na kwamba kufuatia kipigo hicho, alipoteza fahamu kwa siku mbili.

Akizungumza kwa shida akiwa amelezwa hospitalini, mwanafunzi huyo alisema siku ya tukio mwalimu anayetuhumiwa kufanya kitendo hicho (jina tunalihifadhi kwa sasa), alitoa adhabu ya viboko kwa wanafunzi ambao hawakufanya kazi yake na kwamba yeye alipigwa sehemu mbalimbali za mwili hadi kuzimia. Baba mzazi wa mwanafunzi Mabala, Mabala Lung'wecha ambaye anamuuguza mwanawe, alisema kitendo hicho kimemsikitisha sana na kuomba serikali kumchukulia hatua za kisheria muhusika.

Alidai mwanawe alipigwa na alizimia, na kwamba alimkuta hospitali akiwa haongei, wakakaa naye kwa siku mbili ndipo alipopata fahamu, lakini kwa sasa hawezi kuinuka wala kutembea kutokana na maumivu anayoyapata sehemu za mwili.

Tukio hili linadhihirisha kuwa bado kuna umuhimu kwa mamlaka za serikali kuchukua hatua zaidi za kudhibiti matumizi ya viboko shuleni, ambapo athari zake ni kubwa kiasi kwamba upo uwezekano wa kuwasababishia wanafunzi vilema vya maisha au vifo. Diwani wa kata hiyo amesema mwalimu anayetuhumiwa kumjeruhi mwanafunzi huyo anashikiliwa na vyombo vya dola, hivyo ni matumaini yetu kuwa taratibu zitafuatwa ikiwamo kufikishwa mbele ya mkono wa sheria kama ushahidi utabainisha kuwa anahusika.

Aidha, wataribu wa elimu wa kata, maofisa elimu na wahusika wengine watawajibika kwa kuzifuatilia shule kuhakikisha matumizi ya ovyo ya viboko yanadhibitiwa.

Kwa upande wake, wizara husika hainabudi kuwachukuliwa hatua za kinidhamu walimu wakuu ambao watabainika kutozingatia mwongozo wa adhabu ya viboko.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mhariri Wikiendi:** Epson Luhwago
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Makondakta wa daladala toeni kauli nzuri kwa wateja

Na Yasmine Protace

**TUNAPOSEMA** usafiri wa daladala, ndio roho yetu katika mizunguko ya kazi hasa wa mjini na kwingineko kwenye usafiri huu, kila kukicha.

Uhusiano wetu abiria, dhidi ya madereva na makondakta katika usafiri wa daladala, ni kama 'pete na kidole.' Kila mmoja anamtegemea mwenzake.

Kinachonisikitisha ni kwamba, ndugu hao wamekuwa na kauli mbaya dhidi ya abiria wao, kila wakati tunapokutana ndani ya usafiri huo.

Mara zote, makondakta ambao tuko katika ushirika nao, kauli zao siku zote zinatia kichefuchefu, inapotokea katika mazingira ya kuombana kusogea au abiria atakapotoa nauli kubwa, basi suala la kurudishiana chenji linabeba kurushiana kauli chafu.

Si ajabu kumsikia kondakta ana nena kwamba 'sina chenji' au abiria anapotokea hajaridhishwa na kupewa chenji ya fedha iliyochakaa kutoka kwa kondakta.

Tuanze na hilo la noti kubwa, yaani abiria kutoa ama Shilingi 5,000 au hata Shilingi 10,000, akitaka ikatwe Shilingi 400, inakuwa tatizo kubwa.

Kuna wakati unakuta abiria katoa noti hiyo, kondakta anakuwa na mtazamo kama vile amedharauliwa na kumtaka abiria atoe pesa nyingine.

Inawezekana kondakta akawa na hoja, lakini cha muhimu na msingi, ni ustaarabu utumike. Kwa bahati mbaya, hapo ndipo suala la kukosekana ustaarabu linapoanza kuonekana na ndio mwanzo wa pande hizo kuanza

**Kuna wakati unakuta abiria katoa noti hiyo, kondakta anakuwa na mtazamo kama vile amedharauliwa na kumtaka abiria atoe pesa nyingine.**

kutofautiana kauli.

Tunashuhudia sana kondakta anavyokosa heshima, anaanza kumdhalilisha mteja wake, akitumia lugha mbaya akidhani ndio njia sahihi ya kupata suluhisho.

Makondakta wengi huwa wana tabia kwamba bila ya kujali umuhimu wa dhana hiyo ya heshima, wanaanza kuongea kauli za kumdhalilisha mteja wake, kisa kikuu ni hilo la kupewa pesa kubwa.

Malumbano hayo yanapozidi, yanafikia pabaya. Unamkuta kondakta anagoma kumshusha mteja wake,

badala yake anachukua hatua ya kugoma kumshusha abiria mahali anakotaka, anaelekea naye katika kituo cha mafuta ili apate chenji.

Nasisitiza kwamba, makondakta wanakosea sana kutoa lugha mbaya kwa abiria, baadhi yao wako katika umri wa kuwazaa. Wanakuwa wamepitiliza mipaka ya nidhamu zao.

Tena kuna makondakta wengine wanaamua kurudisha chenji yenye pesa nyingi ndogo kama shilingi mia, hamsini na kadhalika.

Kwa kurejea upande wa abiria kurudishiwa chenji, mathalani noti iliyochanika, huwa panashuhudiwa malumbano na abiria, ikibeba mlolongo wa lugha chafu.

Rai yangu ni kwamba, makondakta wanatakiwa kujiheshimu na kuacha kuwadhalilisha wateja wao, wakikumbuka kuwa bila ya watu hao, ajira yao nayo haipo.

Ikumbukwe, abiria wa magari ni watu wa rika tofauti, lakini makondakta wanashindwa kulitambua hilo, wanaendekeza lugha mbaya bila ya kujali waliomo katika gari.

# Precision Air wasafirishaji rasmi Kilimanjaro Marathon

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Ndege la Precision Air limetangaza kuwa msafirishaji rasmi wa mashindano ya Kilimanjaro Marathon.

Meneja Masoko na Uhusiano wa shirika hilo, Hillary Mremi, alisema jana kuwa mashindano haya si tu kwamba yanasaidia kuinua vipaji vya wanariadha hapa nyumbani, lakini pia yanatangaza utalii kwa nchi na Precision Air kama wadau wakubwa wa utalii nchini wanasikia faraja kubwa kushiriki katika tukio hilo,” alisema Mremi.

“Kilimanjaro Marathon ni moja kati ya mbio za riadha zilizofanikiwa sana katika ukanda wa Afrika Mashariki na ni furaha kubwa kwetu kuwa sehemu ya mashindano haya. Tukiwa kama shirika la ndege Tanzania na safari zinazounganisha Kilimanjaro na Dar es Salaam, Zanzibar, Mwanza, Nairobi na Entebbe, tumejizatiti kutoa usafiri wa anga wa haraka, uhakika na nafuu kwa wale wote wanaopanga kushiriki.”

“Tuna wasihi wale wanaopanga kuhudhuria Kilimanjaro Marathon mwaka huu, kuchangamkia fursa ya punguzo la nauli kwa safari zetu zote za ndani ya nchi, ambapo wanaweza kujipatia tiketi ya kwenda tu, kwa nauli ya kuanzia Sh. 90,000,” alisema Mremi na kuongeza:

“Kupitia safari zetu 6 kati ya Dar es Salaam - Kilimanjaro, safari tatu kati ya Nairobi-Kilimanjaro, safari moja kati ya Mwanza - Kilimanjaro na safari moja kati ya Entebbe - Kilimanjaro, abiria wetu watakuwa na uhuru mkubwa wakuchagua muda wa safari wakati wakipanga safari zao.”

Mashindano ya Kilimanjaro Marathon ambayo yalianzishwa mwaka 2003 na kampuni ya Wild Frontiers yakiwa na lengo la kuutangaza utalii Tanzania yameendelea kukua na kuwa moja ya matukio makubwa ya kimichezo katika ukanda wa Afrika Mashariki na Afrika nzima kwa ujumla. Akizungumzia udhamini wa Precision Air, Mkurugenzi wa mbio hizo, John Addison, alisema wanayo furaha kulikaribisha shirika hilo kama mshirika rasmi wa mashindano hayo.

“Ushirikiano tunaopata kutoka kwa mashirika ya nyumbani kama Precision Air umesaidia kwa kiwango kikubwa kukuza hadhi ya mashindano haya na kuwezesha watu wengi zaidi kushiriki ikiwa ni pamoja na wanariadha na mashabiki watakaosafiri kuelekea Kilimanjaro kwa gharama nafuu kwa ajili ya kushiriki riadha pamoja na kusherehekea,” alisema Addison.

## Mbunge asaidia ujenzi zahanati

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MBUNGE wa Jimbo la Morogoro Mjini, AbdulAziz Abood, ametoa Sh. milioni 11.7 kwa ajili ya kununua vifaa vya kumalizia ujenzi wa Zahanati ya Kata ya Sultani, pamoja na ujenzi wa madarasa ya Shule ya Msingi Nanenane, Manispaa ya Morogoro.

Abood aliamua kutoa fedha hizo baada ya kufanya ziara zake za kustukiza katika kata hizo kujionea shughuli za maendeleo na kukuta miradi ya ujenzi ikiendelea kusuasua kutokana na kukosekana kwa fedha za ununuzi wa vifaa hivyo.

IN THE DELEGATE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.1/ OF 2019
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE WILFRED ALARO KOMINGO
AND
IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY JACKLINE WILFRED KOMINGO

**GENERAL CITATION**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased s are hereby invited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of petition for letters of administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before 20th day of February , 2019.

The will if any of the said deceased is deposited and open for inspection of the court.

Dated 18th This day of January 2019.

........................................................
Resident Magistrate
DODOMA.




# Wanafunzi shule kongwe wasomea chini ya miembe

INATOKA UK. 2

sababu hakuna sehemu ya kukaa na kusoma.

"Kwa miaka mingi sasa shule yetu imekuwa na janga kubwa la wanafunzi kusomea chiti ya miti ya miembe kutokana na ukosefu wa vyumba vya madarasa. Tunaiomba serikali na wadau wengine kutusaidia kutujengea vyumba vya madarasa. Wako viongozi waliokuja hapa mara kadhaa lakini hakuna utekelezaji wowote uliofanyika hadi sasa," alisema Tumaini.

Kwa mujibu wa Tumaini, shule hiyo ina wanafunzi 266 kuanzia wa darasa la kwanza hadi la saba pamoja na wale wa awali lakini ina vyumba vinne vya kudumu na tisa vya muda mfupi.

Alisema hata baadhi ya vyumba vya madarasa vya muda vilivyopo hali yake si mzuri kwa kuwa vipo vilivyo na nyufa na vilivyobomoka kabisa ambavyo hata kuwaweka wanafunzi ni hatari hasa kwa kipindi hiki cha mvua.

Mmoja wa mzazi wa wanafunzi hao, Nasoro Loya, alisema chanzo cha kuwapo kwa changamoto mbalimbali kwenye kijiji hicho, ikiwamo ya sekta ya elimu, ni viongozi wa ngazi za juu kukitenga kijiji hicho kutokana na kutokuwa na utamaduni wa kufika na kukutana na wananchi ili kusikiliza kero zao.

Alisema kama viongozi wangekuwa na utaratibu wa kufika na kusikiliza kero za wananchi na kuzifanyia kazi, hata kwa asimilia 50 ya changamoto zilizopo zingepungua ikiwamo ya wanafunzi kusomea chini ya miti ya miembe.

Mzazi mwingine, Maimuna Ally, alisema wanasikitishwa kuona watoto wao wakiwa wanasomea chini ya miembe na kuona watoto wengine wakiwa katika shule bora huku hata watoto wao wanahitaji elimu bora pia kama ilivyo kwa watoto wengine.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, Barna Sijale, alisema licha ya changamoto ya elimu, kijiji pia kina changamoto zingine ambazo ni kikwazo cha maendeleo, zikiwamo maji na afya.

Alisema wananchi wa kijiji hicho wana utamaduni wa kujitolea kwenye shughuli za maendeleo lakini baadhi ya mambo yanakwama kwa sababu ya viongozi wenyewe kukigeuzia kisogo kijiji hicho badala ya kuwahamasisha .

Kaimu Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Rajabu Saidi, alipohojiwa kuhusu changamoto ya shule hiyo, alikataa kuzungumza chochote na kusema mpaka apate kibali kutoka kwa mkurugenzi mtendaji wa halmashauri hiyo.

"Sisi wakuu wa idara hata kama kitu tunakijua, hatuwezi kuzungumzia au kuzungumza na waandishi wa habari mpaka tupate kibali kutoka kwa DED (Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya), hivyo nakuomba ndugu mwandishi nenda kwa mkurugenzi, sitaki kusema chohote hata kama ninafahamu," alisema Saidi.

Nipashe ilipiga hodi ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Changwa Mkwazu, lakini mwandishi alielezwa kuwa amesafiri na nafasi yake inakaimiwa na Ofisa Kilimo, Winfrid Tamba.

Alipioulizwa juu ya suala hilo, alisema: "Mimi ni ofisa kilimo wa halmashauri hii. Leo (juzi) nimekaimu kama mkurugenzi. Kuhusu changamoto hiyo ya wanafunzi kusomea chini ya miti, siwezi kuisemea ni bora uje baada ya mkurugenzi kurudi safari ili aizungumzie mwenyewe."



Mfanyabiashara wa Kenya, Brian Mutembei wa kampuni ya Indopower Sol Ltd (kulia mwenye suti na tai nyekundu ), akisaini mkataba wa mauziano ya korosho tani 100,000 yenye thamani ya Sh. bilioni 418 kati ya serikali na kampuni yake jijini Arusha jana. kushoto (shati la kitenge) ni Mkurugenzi wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Dk. Hussein Mansoor. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Mvumbuzi tanzanite afariki dunia

INATOKA UK. 3

Aliongeza kuwa: "Hii inadhihirisha tanzanite haijavumbuliwa na mtu kutoka nje, nimeambiwa mzee huyu hivi sasa amepooza kidogo," alisema.

Magufuli alisema barua ya mtaalamu wa madini aliitia saini Septemba 23, 1967 na alishatia saini hati ya kupewa tuzo ya sayansi ya ufundi mwaka 1984.

Alisema licha ya kuvumbua madini hayo, lakini mzee huyo amekuwa akihangaika siku nyinyi tangu mwaka 1967.

"Ukifanya chochote hata kama ni kizuri namna gani, hata ungegundua nini, ninafahamu wagunduzi wengi chuo kikuu lakini hawakutambuliwa, hata mimi niligundua kitu fulani cha Kemia, lakini nilivyoomba kutambuliwa mpaka leo wamebaki na kitabu changu kwenye Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam," alisema na kuongeza:

"Nimeona nimlete hapa ili Watanzania wamtambue, ili kusudi akatibiwe vizuri, serikali itampa Sh. milioni 100 ili akazitumie katika matibabu yake na kujisitiri mambo mengine, fedha hii itawekwa kwenye akaunti yake kesho au kesho kutwa zimsaidie."

## Wadau wanena

INATOKA UK. 2

ukomo wa uongozi badala ya kutawala milele kama ilivyo sasa," alisema.

Alisema kuwapo kwa mabadiliko hayo kutawezesha kudhibiti matumizi ya ruzuku kwa vyama vya siasa nchini, kuwapo kwa ukomo wa uongozi kwa wananasiasa ndani ya vyama vyao na wanasiasa kuwa na mamlaka ya kutoa malalamiko kwa msajili.

"Kama mwanademokrasia ambaye nimeshakuwa sehemu ya mwanzilishi wa Chama cha ACT-Wazalendo, naona kuwa kuwapo kwa muswada huu kutaondoa ukiritimba uliopo kwenye vyama hivi, msajili atafuatilia matumizi ya ruzuku na kupokea malalamiko ya wanasiasa," alisema Shaibu.

Muswada huo ulisomwa kwa mara ya pili bungeni juzi na kujadiliwa na wabunge na baadaye kupitishwa na chombo hicho cha kutunga sheria.

Katika mjadala wa muswada huo bungeni, wabunge wa upinzani walilalamikia vifungu vinne walivyodai ni hatari kwa ustawi wa siasa na demokrasia nchini.

Miongoni mwa vifungu vilivyolalamikiwa ni kifungu cha 3(c) ambacho kinatoa mamlaka kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kuingilia mfumo wa uchaguzi ndani ya vyama, wakidai kinapunguza uhuru wa vyama vya kufanya uchaguzi bila shinikizo kutoka katika Ofisi ya Msajili.

## Samia atoa neno

INATOKA UK. 5

Akizungumza kauli ya Makamu wa Rais, Dk. Gwamaka alisema tukio hilo limekuwa ni motisha kwa bodi na uongozi wa NEMC, na kwamba bodi na NEMC wana deni kwa Wtanzania na Serikali na kwamba NEMC italipa deni hilo kwa kuchapa kazi kutosheleza matarajio ya Makamu wa rais na Serikali.

"Binafsi naheshimu na kutambua uteuzi wangu. Naheshimu na kutambua kauli ya mkuu wa nchi kwamba ana imani na bodi, ana imani na mimi na uongozi wa baraza. Tuna deni kwa Watanzania na serikali yetu na tutalilipa kwa kufanyakazi," alisema na kufafanua kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais ndiyo wizara mama ya baraza.

Alisema kauli ya Samia imewapa mwanga mzuri wa kufanyakazi kwa bidii na kutekeleza Sheria ya Mazingira na kanuni zake, na hicho ndicho watakachokifanya.

Amesema serikali imeeleza wazi namna ya Tanzania kuwa taifa lenye uchumi wa kati na wa viwanda na kwamba majukumu ya NEMC katika kutekeleza shabaha hii yako wazi, hivyo kilichobaki ni kutekeleza majukumu hayo.

Bodi mpya ya NEMC ilizinduliwa na Waziri wa Nchi (Muungano na Mazingira) hivi karibuni na kuiagiza kupiga vita kwa nguvu zote rushwa na utoaji vyeti vya kugushi.

Bodi mpya ipo chini ya uenyekiti wa Prof. Esnati Osinde Chaggu ambapo wajumbe wake ni Dk. Flora Tibarazwa, Prof. Husseain Sosovele, Dk. Catherine Masao, Damas Masologo, Dk. Neduvoto Mollel, Prof Dos Santos Silayo, Dk. Ezekiel Mwakalukwa na Prof. William Mwegoha.

# Mchakato wa kuboresha sekta ya uvuvi waanza

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

ILI kuhakikisha sekta ya uvuvi inachangia pato la taifa na kuboresha maisha ya Watanzania, serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imesema imedhamiria kuboresha Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003 namba 22 na kuanzisha mpya ya viumbe maji.

Akizungumza wakati akizindua mkutano wa kitaifa wa utoaji maoni ya kuboresha sheria ya uvuvi mwaka 2003 na sheria mpya ya kuendeleza viumbe maji ulifanyika kwa Kanda ya Ziwa mkoani Mwanza, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alisema mkutano huo umewashirikisha zaidi ya wajumbe 200 wakiwamo wavuvi, wachakataji wa samaki, wafanyabiashara wa samaki na wenye viwanda.

Washiriki wengine ni wamiliki, mawakala, wauzaji wa nyavu, wakuu wa wilaya, viongozi wa dini, wanafunzi wa vyuo vikuu, maofisa uvuvi, wastaafu, taasisi za serikali na binafsi.

Alisema wameamua kuandika sheria upya ya uvuvi kwa kuifanyia mageuzi ana wamefanikiwa kupata maoni ya wadau ambayo michango yao itasaidia kufikia malengo waliyokusudia na yanayoendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia na kutoa ulinzi, fursa ya uwekezaji, kuleta ufanisi katika uzalishaji na kuongeza thamani kwenye uzalishaji.

"Tumelipa umuhimu jambo hili la kubadili sheria ya uvuvi na kuunda mpya ya kuendeleza viumbe maji kwa sababu Tanzania kwa kiasi kikubwa inategemea sekta ya uvuvi na unapozungumzia suala hilo unakuwa unazungumzia maisha ya wananchi, ambapo unatoa ajira, watatumia kama chakula katika kuboresha afya zao na watauza katika masoko ya ndani na nje ya nchi, hivyo kulipatia taifa mapato sambamba na kuufanya uwe endelevu kwa kizazi kijacho na kuimarisha maisha ya Mtanzania," alisema Mpina.

Alisema kutokana na umuhimu wake wameona iko haja ya kubadili sheria hiyo ambayo imedumu kwa takribani miaka 16 ili kuondoa changamoto ambazo hazina manufaa.

Pia alisema, wameamua kuanzisha sheria mpya ya ukuzaji wa viumbe maji kutokana na sheria ya uvuvi ya mwaka 2003 kutotambua vizuri ukuzaji wa viumbe kwenye maji, hivyo kukosa usimamizi thabiti pamoja na kutokuwa na utaalamu wa uzalishaji vifaranga vya samaki na chakula cha samaki na matokeo yake kufanya uvuvi kushindwa kuchangia pato la taifa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Rashid Tamatamah, alisema wizara imeamua kuja na mchakato wa kuboresha sheria ya uvuvi na kuandaa mpya ya ukuzaji viumbe maji ambayo itaendana na mabadiliko ya sasa na kunufaisha Watanzania kiuchumi, hivyo watakusanya maoni nchi nzima kwa kanda sita Kanda ya Ziwa Victoria, Kanda ya Ziwa Tanganyika, Kanda ya Ziwa Nyasa, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kati na Kanda ya Pwani.

Naye aliyewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Saidi Mecky Sadiki, ambaye aliwakilisha kundi la wastaafu na wafugaji wa samaki, alisema katika ufugaji wa samaki sheria iangalie namna ya kurahisisha wakati wa mchakato wa kutafuta kibali pamoja na gharama ili hata wavuvi wenye kipato cha chini waweze kuwekeza.

Pia kila wilaya kuwe na mtaalamu wa kutoa elimu ya ufugaji samaki, gharama za ushuru zipunguzwe kwa wafanyabiashara wanaoagiza neti China za kufugia samaki kwenye viziba.

Kadhalika wanataka wizara kutenga na kuainisha maeneo ziwani ya kufugia ili mwekezaji akitaka kuwekeza aanze moja kwa moja kufuatilia vibali na pia kuendelea kuzuia samaki na vifaranga kutoka nje kwa kuwa inasababisha kupoteza samaki asilia pamoja na kuruhusu sato kuuzwa nje.

# Iringa yajipa matumaini ATCL kuongeza watalii

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, amesema ifikapo Machi mwaka huu mkoa huo utaanza kupokea ndege za Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) baada ya kukamillika kwa ukarabati wa uwanja wa Nduli.

Hapi aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na vyombo vya habari na kufafanua kuwa kuanza kwa safari hizo kutasaidia kukuza uchumi wa mkoa na kuongeza idadi ya watalii.

Alisema ukarabati unaendelea na ndege hizo zikianza safari za Iringa watapokea wageni wengi, wawekezaji katika sekta ya hoteli na watalii wengi wa ndani na nje ya nchi.

Alisema ndege zinazotua katika kiwanja hicho ni ndogo na gharama yake ni kubwa na mtu akiwa ametoka kutalii Mkoa wa Kilimanjaro akitaka kwenda Ruaha itambidi alipie sio chini ya Dola za Kimarekani 800.

"Baada ya kufanya ukarabati katika kiwanja chetu cha ndege tumeamua kutumia nguvu zetu kama mkoa pamoja na wadau kuboresha jengo la kupokelea wageni, hatukutaka kusubiri bajeti ya serikali tumetumia nguvu zetu wenyewe na tayari tumeshapata mashine ya ukaguzi, hivyo tunatarajia ifikapo Machi tutaanza kupokea ndege za ATCL," alisema Hapi.

Aidha, alisema kuna mradi wa kukuza utalii Kusini ambao utapanua uwanja wa ndege kuwa wa kisasa na kuanza kupokea ndege kubwa.

"Katika huo mradi kutajengwa barabara ya lami kutoka Iringa hadi Hifadhi ya Ruaha yenye kilometa 104, hii itakuwa ni sehemu ya mradi wa utalii wa kusini na kutatua changamoto ya usafiri," alisema.

Pia alisema kutajengwa kituo cha utalii cha Nyanda za Juu Kusini ambacho kitakuwa mkoani Iringa kwa ajili ya kufuatilia na kukuza sekta ya utalii.

"Sisi kama mkoa zipo juhudi ambazo tunazifanya kutangaza mkoa wetu, bado tuna kazi ya kufanya ya kutangaza vivutio vya mkoa wa Iringa, ili viweze kujulikana ndani na nje ya nchi," alisema Hapi.

Hapi alisema mkoa huo una vivutio vingi ambavyo havijatangazwa kama ilivyo hifadhi nyingine, jambo ambalo linatakiwa kufanyiwa kazi.

"Huwezi kufanya hivyo kama unataka watalii watoke Arusha kwa basi hadi Iringa, hii haiwezekani ndio maana tunataka kuanzisha safari za ndege," alisema na kuongeza:

"Ukishafungua safari za ndege, gharama zitapungua na kurahisisha usafiri, hii ni mikakati ambayo tunataka kuifanya Iringa ifanane kabisa na mikoa kama Arusha kwa maana ya utalii."

Alisema baada ya kipindi kifupi Iringa itaanza kung'aa kwa vivutio vya utalii na kuanza kupokea idadi ya watu wengi kutokana na mi-



Naibu Waziri waViwanda Zanzibar, Hassan Hafidh Amir (kushoto), Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Ayubu Mohamed Mahmood, Mtendaji Mkuu wa SAGCOT, Geoffrey irenga na Mratibu wa Mradi wa Kuendeleza Kuku katika kampuni ya Silverlands, Mwanamvua Ngocho, wakijadiliana jambo baada ya kutembelea miradi ya kuku Zanzibar. **MPIGAPICHA WETU**

# Vigogo wa jiji wavuliwa vyeo

**Na Dege Masoli,**
TANGA

VIGOGO wawili wa Halmashauri ya Jiji la Tanga wameshushwa vyeo kutokana na kukumbwa na makosa ya kinidhamu ikiwamo kusababisha hasara ya Sh. milioni 18.

Akisoma maazimio ya Kamati ya Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Tanga, mwenyekiti wa kamati hiyo, Mhina Mustapha, aliwataja watumishi hao na vyeo vyao walivyokuwa navyo kabla ya adhabu hiyo kuwa ni Flora Shija (ofisa maendeleo ya jamii) na Nobert Achiula (kaimu ofisa michezo).

Mustapha ambaye pia ni Meya wa Jiji hilo, alieleza tuhuma za viongozi hao kuwa ni za kinidhamu, udanganyifu na ubadhirifu wa fedha za Umma.

Alisema Shija amekumbwa na tuhuma za kuunda vikundi viwili ambavyo ni hewa vinavyoonyesha kuvilipa Sh. milioni sita, huku Achiula akikabiliwa na tuhuma ya upotevu wa Sh. milioni 12.

Alisema kikao hichi kiliwashusha vyeo watu hao wawili na kurudi kwenye utumishi wa kawaida, huku kutakiwa kurejesha kila mmoja fedha anazodaiwa na halmashauri hiyo.

Wakati huo huo, Meya alitoa wito kwa watumishi wa halmashauri wakiwamo watendaji kata kusimamia weledi katika utekelezaji wa majukumu yao ili kutekeleza azima ya halmashauri ya ukusanyaji wa mapato na kuihudumia jamii.

Mkurugenzi wa Jiji la Tanga, Daudi Mayeji, alisema atatekeleza maagizo hayo ya kamati na kuahidi kutoa taarifa ya utekelezaji katika kikao cha baraza lijalo.

# Sugu atamani Dk. Ulisubisya kuwa Mkuu Mkoa Mbeya

MBUNGE wa Mbeya Mjini (Chadema), Joseph Mbilinyi, ameliambia Bunge kwamba angekuwa Rais John Magufuli asingemteua Dk. Mpoki Ulisubisya kuwa balozi, badala yake angemteua kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya.

Amesema kumpeleka Dk. Mpoki nje ya nchi ni kupeleka huduma mbali na Watanzania, kwa vile balozi huyo alifaa kuendelea kutoa mchango wake ndani ya nchi.

"Ili kuondoa dhana kwamba wapinzani hawezi kupongeza, wao kila kitu ni kupinga, leo kwa mara ya kwanza naipongeza serikali na hasa Dk. Mpoki aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya ambaye ameteuliwa na Rais (Magufuli) kuwa balozi.

Ingekuwa mimi ningemteua kuwa RC Mbeya, huyu anastahili kuendelea kutoa utaalamu wake," alisema.

Dk. Mpoki aliteuliwa na Rais Magufuli hivi karibuni kuwa Balozi wa Tanzania, ingawa bado hajapangiwa nchi atakayokwenda kuiwakilisha nchi.

Katika swali lake la msingi, Mbilinyi maarufu kama 'Sugu' alitaka kujua ni kiasi gani cha fedha kimeshatolewa mpaka sasa kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la kisasa la maabara katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya.

Alisema katika bajeti ya mwaka 2017/2018 Wizara ya Afya iliomba kutengewa Sh. bilioni tano kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la maabara na ununuzi wa vipimo vya kisasa kama CT Scan na MRI Scan katika Hospitali ya Rufani ya Mbeya.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Faustine Ndugulile, alisema katika mwaka wa fedha 2016/2017 serikali ilipeleka Sh.bilioni moja na baadaye katika mwaka wa fedha 2018/2019, wizara iliomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. bilioni tano kwa ajili ya ukamilishaji mradi wa ujenzi wa jengo la huduma za Radiolojia na jengo la wazazi Meta katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya.

Naibu waziri huyo amelieleza Bunge kuwa hadi sasa kiasi cha Sh. bilioni tatu zimeshapokelewa kwa ajili ya kazi hizo, ambapo Sh. bilioni mbili ni kwa ajili ya kumalizia mradi wa ujenzi wa jengo la radiolojia na ununuzi wa baadhi ya vifaa vya radiolojia.

Alisema Sh. bilioni moja ni kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa jengo la wazazi Hospitali ya Rufani Meta.

Kuhusu ni lini ujenzi huo utakamilika, serikali imesema ujenzi huo umeshakamilika kwa asilimia 90 na kwa sasa mafundi wanakamilisha kuingiza umeme katika jengo baada ya ununuzi wa transfoma.

Hivyo hadi kufikia mwezi Machi 2019 litakuwa limekamilika rasmi.

Aidha, Wizara ya Afya imeeleza serikali tayari imeshanunua CT Scan kwa ajili ya Hospitali ya Rufani ya Mbeya ambayo inasubiria kukamilika kwa jengo maalumu ili liweze kusimikwa rasmi na vilevile hospitali inategemea kupatiwa mashine za MRI kupitia mradi wa ORIO wa Wizara ya Afya.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Mbunge wa Busega, Dk. Raphael Chegeni, kwenye viwanja vya Bunge jijini Dodoma, juzi. **PICHA: OWM**

# Mwongozo kukomesha ukatili kwa wanawake, watoto waja

**Na Godfrey Mushi,**

DODOMA

SERIKALI imesema inaandaa mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (2017/18-2121/22), ambao miongoni mwa shabaha zake ni kuhakikisha watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na kufanya kazi mitaani wanapata huduma stahiki.

Kauli hiyo ilitolewa jana Bungeni na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum, Aisha Rosse Matembe (CCM).

Mbunge huyo alitaka kujua kama serikali ina mpango gani wa kuanzisha kampeni ya kitaifa kukabiliana na tatizo hilo kwa nchi nzima ikiwamo kuwaweka kwenye vituo maalum na kuwapatia huduma za msingi.

Pia, alitaka kujua kama serikali inatambua idadi kamili ya watoto wa mitaani wanaoishi kwenye mazingira hatarishi.

"Tatizo la watoto waishio katika mazingira hatarishi linazidi kuwa janga la kitaifa nchini, huku jitihada za kukabili zikionekana kutopewa kipaumbele hali ni mbaya sana katika majiji makubwa kama Dar es Salaam,

Mwanza na Mbeya, ambapo idadi kubwa ya watoto hao hujihusisha na kuomba pamoja na matukio ya uhalifu ikiwamo wizi wa vifaa vya magari kwenye maegesho.

"Je, serikali ina mpango gani wa kuanzisha kampeni ya kitaifa kukabiliana na tatizo hilo nchi nzima ikiwamo kuwaweka kwenye vituo maalum na kuwapatia huduma za msingi?

Pia alitaka kujua kama serikali inatambua idadi kamili ya watoto wa mitaani wanaoishi kwenye mazingira hatarishi, alisema.

Dk. Ndugulile alisema serikali ina mpango wa kuwaunganisha watoto hao na familia zao na pale itakapobainika kuwa wazazi hawapatikani, watoto hao wataunganishwa katika familia za kuaminika wakati taratibu nyingine za kudumu zikiendelea kufanyiwa kazi na mamlaka husika, ikiwamo taratibu za malezi ya kambo, kuasili au kuwapeleka katika makao ya watoto.

Alisema kuwa serikali kwa kushirikiana na wadau imeandaa mwongozo wa watambuzi wa watoto wao katika mazingira hatarishi na kuwaunganisha na huduma.

"Katika kipindi cha Julai 2017 hadi 2018 jumla ya watoto 864,496, ambapo wanaume ni 454,053 na wanawake ni 410,443, walitambuliwa kuwa wanaishi katika mazingira hatarishi katika mikoa yote nchini kasoro mikoa ya Lindi na Mtwara," alisema.




**Habari zote na Godfrey Mushi,** DODOMA

## 367,985 wahudumiwa vituo vya afya

SERIKALI imesema jumla ya wananchi 367,985 wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime mkoani Mara, wanapata huduma za afya katika Hospitali ya Wilaya ya Tarime mkoani Mara, pamoja na vituo vya afya 8, vitano vikiwa vya serikali na vitatu vikiwa vya binafsi na zahanati 23, huku 16 vikiwa vya serikali na saba vikiwa vya binafsi.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais –TAMISEMI, Josephat Kandege, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche (Chadema).

Mbunge huyo alitaka kujua ni kwanini serikali isipandishe hadhi Hospitali ya Wilaya ya Tarime na kuwa hospitali ya Mkoa kutokana na hospitali hiyo kwa sasa kuelemewa na wagonjwa wengi.

"Hospitali ya Wilaya ya Tarime imeelemewa na mzigo wa wagonjwa kwa sababu inapokea wagonjwa wengi kutoka Wilaya ya Tarime na Rorya, pamoja na uchache wa vituo vya afya katika maeneo mengi ya wilaya hiyo, je,ni kwanini serikali isipandishe hadhi hospitali hiyo na kuwa hospitali ya mkoa?" Alihoji Heche.

Kandehe alisema ni kweli kuwa hospitali hiyo inahudumia Wilaya ya Tarime, Rorya, Msoma na Bunda na wagonjwa kutoka nchi jirani ya Kenya na kusababisha msongamano wa wagonjwa.

Hata hivyo, alisema serikali haina mpango wa kupandisha hadhi hospitali hiyo kuwa Hospitali ya Mkoa, kwa kuwa Mkoa wa Mara huna hospitali ya rufani iliyoko Musoma mjini.

"Ili kutatua changamoto za utoaji wa huduma za afya katika Mkoa wa Mara, serikali katika mwaka wa fedha 2018/19 imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 4.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali tatu za halmashauri katika halmashauri za Bunda, Rory na Musoma.

"Tayari fedha zote zimepelekwa kwenye halmashauri husika kwa ajili ya kuanza ujenzi, vilevile serikali inaendelea na ukarabati na ujenzi wa vituo sita vya afya katika Mkoa wa Mara vinavyogharimu jumla ya Shilingi bilioni 2.4.

"Ujenzi wa hospitali tatu za halmashauri na vituo sita vya afya utaimarisha huduma katika ngazi ya msingi na kupunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali ya Wilaya ya Tarime," alieleza Kandege.

# Watendaji serikali wadaiwa kuendeleza kibano kwa machinga

**Na Allan Isack,** ARUSHA

BAADHI ya watendaji wa serikali wameanza kuwabughudhi wamachinga wenye vitambulisho vinavyotolewa na Rais John Magufuli kwa kuwatoza ushuru na kukamata mali zao.

Mwenyekiti wa machinga Mkoa wa Arusha, Amina Samson, alisema licha ya kununua vitambulisho hivyo kama maelekezo ya Rais Magufuli yalivyokuwa, lakini bado wanapata adha ya kunyanganywa mali zao na kushinikizwa kulipa kodi kwa nguvu.

Alisema hali hiyo, inawakatisha tamaa wamachinga kuendelea kujisajili kwa ajili ya kupewa vitambulisho hivyo, ambavyo vinatolewa kwa watu wenye mauzo ghafi kuanzia Sh. milioni nne kushuka chini kwa mwaka.

"Rais wetu anawajali wanyonge, lakini maagizo yake aliyoyatoa hayafanyiwi kazi kwa sababu wamachinga wameitikia kununua vitambulisho, lakini bado wanateswa kwa kunyanganywa na kukimbizwa masokoni na watumishi wa serikali.

"Sisi wamachinga tumeitikia agizo la Rais lakini kutokana na manyanyaso tunayoyapata katika masoko wamachinga wamevunjika moyo kuendelea na zoezi la kujiandikisha kuchukua vitambulisho ambayo kimsingi vililenga kutusaida kujikimu kimaisha na kuongeza kipato," alisema.

Alisema wamekuwa wakifanya biashara zao kwa wasiwasi mkubwa kutokana na kuhofia kuporwa bidhaa zao hivyo.

Wamemwomba Rais Magufuli kuwachukulia hatua kali za kisheria watendaji hao ambao wamekiuka agizo lake.

Akizungumzia sakata hilo la wamachinga kusumbuliwa kulipa ushuru kwa nguvu na kuporwa bidhaa zao, ofisa biashara Mkoa wa Arusha, Franco Nusu, alikiri kusikia malalamiko hayo na aliahidi kufanyia kazi suala hilo. Kwa upande wa Ofisa Biashara wa Jiji la Arusha, Godfrey Edward, alikiri kupokea malalamiko ya wamachinga kubughudhiwa na wakuu wa masoko yaliyopo jijini hapa.

"Ni kweli malalamiko hayo nimeyasikia haswa katika soko la Samunge, Kilombero na Soko Kuu kwamba wanaokusanya ushuru katika masoko hayo, siyo wazabuni ni watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha," aliongeza. Hata hivyo, uchunguzi uliofanywa na mwandishi wa gazeti hili, umebaini mpaka sasa zoezi la kugawa vitambulisho vya wamachinga linaendelea.

Mwenyekiti wa UVCCM, Mkoa wa Arusha, Saitoti Zelote, alitoa onyo kali kwa watendaji wa serikali mkoani hapa wanabughudhi machinga kwa kuwadai ushuru kwa nguvu na kupora mali zao. Aidha, aliwaahidi machinga hao, kufikisha kilio chao serikalini ili hatua kali ziweze kuchukuliwa dhidi yao.

"Rais John Mgufuli alishaagiza kuwa wamachinga wote wenye vitambulisho wasibughudhiwe lakini kuna baadhi ya watendaji ambao wanapuuza agizo la Rais, hao tutahangaika nao ili wachukuliwe hatua kali za kisheria," alisema. Mkoa wa Arusha ulipewa jumla ya vitambulisho 25,000 vya wamachinga, lakini mpaka kufikia mwisho wa wiki iliyopita vitambulisho vilivyokuwa vimegawanywa kwa machinga ni 10,400 pekee, ambapo hadi sasa zaidi ya vitambulisho 14,000 bado havijagawanywa kwa machinga hao.



Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara, Chelestino Mofuga, akikagua madaftari ya wanafunzi wa kidato cha kwanza wa Shule ya Sekondari Singland juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Aomba msaada wa fedha kutibiwa Hospitali Ocean Road

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKAZI wa Mtaa wa Longdongi, Kata ya Sokoni One, Jijini Arusha, Bakari Omary Makungu, (28), anaomba msaada wa fedha za matibabu katika Hospitali ya Ocean Road jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe baada ya kutembelewa nyumbani kwake, Makungu alisema anaishi katika chumba kimoja na hana mtu wa kumsaidia tangu aanze kuugua mwaka 2017.

"Ugonjwa huu ulianza kama muwasho, huku vikiota vipele vidogo vidogo baadhi ya sehemu za mwili na baadaye mwili ukaanza kuchanika mithiri ya nyoka aliyemwagiwa mafuta ya dizeli," alisema huku akijikuna. Akielezea jinsi ugonjwa huo unavyomtesa, alisema hawezi hata kuvaa shati, kwa sababu ya muwasho anaoupata mwili mzima.

Aidha, alisema ameshatibiwa Hospitali ya Kaloleni, jijini Arusha, mara kadhaa, huku wakipima bila kujua anasumbuliwa na ugonjwa gani.

"Mwaka jana nilienda hospitali ya Kanisa Katoliki Moshi, nikapimwa na kuambiwa huenda nasumbuliwa na kansa ya ngozi, lakini ikawa imebakia kipimo kimoja nifanyiwe, lakini kutokana na kukosa fedha sikurudi hadi sasa," alisema.

Aliomba Watanzania watakaoguswa, wamsaidie kwa hali na mali ili aweze kwenda Hospitali ya Ocean Road kupata vipimo na matibabu.

Said Makungu ambaye ni kaka yake, alisema mdogo wake anaumwa tangu mwaka 2017 na jitihada ya kumpeleka hospitali zinakwama kutokana na hali ngumu ya maisha ambayo wanayo. "Kwa kweli tumefika mahali tumekata tamaa kwa sababu kama mnavyoona hapo chini ni rundo la makasha ya dawa, ambayo ameshatumia bila kupona," alisema.

Alisema kadri siku zinavyozidi kwenda mbele hali ya mdogo wake inakuwa mbaya, lakini akipelekwa hospitali anapatiwa dawa zile zile.

"Naomba viongozi wa madhehebu ya dini, viongozi wa serikali, jamii pamoja na mtu atakayeguswa na habari hizi, atusaidie tuweze kumpeleka mdogo wetu Ocean Road kwa vipimo na matibabu," alisema.

Ameomba watakaoweza kutoa msaada huo watume kwa namba **0767702580 na 0758757461.**

# DC ataka ushirikiano kupata haki za binadamu

**Na Mwandishi Wetu,** HANANG'

MKUU wa Wilaya ya Hanang', Joseph Mkirikiti, amezitaka taasisi za serikali kushirikiana na wadau wanaotetea haki za binadamu kuongeza upatikanaji wa haki za binadamu kijamii, kiuchumi na kiutamaduni kwa wananchi wote.

Alisema hayo mjini Babati juzi, wakati akizundua jarida la taarifa za msaada wa kisheria, lililotolewa na mtandao wa mashirika yasiyo ya kiserikali mkoani Manyara (Macsnet).

Alisema licha ya umuhimu wa watu hao bado kuna baadhi ya maeneo wanakosa nafasi inayostahili na kuonekana ni tatizo ili hali wanatatua migogoro katika jamii nyingi na kupata haki zao.

Alisema kuwapo kwa wasaidizi wa kisheria kutasaidia kupunguza kwa upatikanaji wa haki kwa wengi na kuchangia kuleta maendeleo endelevu katika jamii. "Katika mkoa huu na wilaya zake kuna changamoto nyingi sana katika ngazi ya kata, vijiji na vitongoji, hivyo wasaidizi hao wa kisheria watasaidia kwa kiwango kikubwa kuondoa changamoto hizo katika maeneo hayo," alisema.

Alisema ni watu wengi wanaokosa haki katika vituo vyetu vya sheria ila wanakosa haki ama kwa kutoelewa au kuwa na hofu ni wengi zaidi.


Aliwataka wasaidizi hao wa sheria kufanya yale mambo yanayopiganiwa katika jamii ikiwamo nafasi ya mwanamke katika kumiliki mali na siyo kuunga mkono mambo ambayo hayana tija kwa jamii za kiafrika.

Mratibu wa Macsnet, mkoani Manyara, Nemence Iriya, alisema upatikanaji wa haki nchini una changamoto nyingi ikiwamo upungufu wa mahakama, umbali wa kufikia huduma za kisheria, uelewa mdogo juu ya masuala ya kisheria na kuendelelea kufuata mila na desturi zilizopitwa na wakati.

"Wanawake wa vijijini na makundi yanayoishi katika mazingira hatarishi yana uwezo mdogo wa kusimama na kutetea haki zao kama haki ndani ya ndoa, haki ya kumiliki mali na kumiliki ardhi hii inasababisha wengi wao kushindwa kujiamini," alisema.

Alisema Macsnet inajihusisha katika kusaidia wasaidizi wa kisheria Manyara katika nyanja tofauti tofauti ikiwamo kutoa mafunzo na midahalo lengo ikiwa ni kuongeza uwezo wa wasaidizi hao katika kutoa msaada wa kisheria kwa makundi yanayoishi katika mazingira hatarishi ili kuweza kulinda haki zao katika mazingira wanayoishi. Mmoja kati ya aliyepata msaada wa wasaidizi wa kisheria, Regina Matle, alisema ameteseka kwa miaka mitatu bila msaada, huku akichomewa nyumba na watoto wake kukatwa na panga lakini alipokutana na wasaidizi wa kisheria suala lake limepata msaada na kesi ipo mahakamani.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoa wa Manyara, Anna Fissoo, alisema wanapaswa kushirikiana na wasaidizi wa kisheria ili kuifanya Manyara kuwa mahali salama kwa kila mtu, iwe kwa mtoto aliye tumboni iwe kwa baba na mama.





# Watendaji wa halmashauri kortini tuhuma za rushwa

**Na Paul William,** MOSHI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imemfikisha mahakamani aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Rombo, Judethadeus Mboya, pamoja na Mwanasheria wa halmashauri hiyo, Andrew Gregory, kwa matumizi mabaya ya mamlaka na kuisababishia halmashauri hiyo hasara ya Sh. milioni 226.68.

Kesi hiyo ya uhujumu uchumi namba ECC. 1/2019 ilifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, mbele ya Hakimu Mfawidhi, Bernazitha Maziku, huku upande wa Takukuru ukiwakilishwa na mwanasheria wake, Suzan Kimaro.

Katika shtaka la kwanza Mboya ambaye kwa sasa amestaafu utumishi wa Umma na Gregory ambaye kwa sasa amehamishiwa Halmashauri ya Mpwimbwe mkoani Katavi, wanashtakiwa kwa kutumia madaraka yao vibaya kwa kuingia mkataba usio na tija kwa kuipangisha ardhi kampuni ya Junyu Investment Company Ltd kinyume na kifungu cha sheria namba 31 ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

Kosa la pili, wote wawili kwa pamoja wanashtakiwa kwa kuisababishia

hasara kwa makusudi Halmashauri ya Wilaya ya Rombo jumla ya Sh. milioni 226, ambapo washtakiwa hawakutakiwa kujibu makosa yao kwa kuwa mahakama hiyo haina uwezo wa kusikiliza kesi hiyo.

Hakimu Mfawidhi Maziku alisema kuwa, dhamana iko wazi ambapo masharti ya dhamana ni wadhamini wawili kwa kila mmoja, ambapo wataweka dhamana ya fedha taslimu Sh. milioni 56 au hati ya mali isiyohamishika yenye thamani ya fedha hiyo.

Washtakiwa hao walishindwa kutimiza masharti ya dhamana, ambapo walipelekwa mahabusu hadi Februari 8 mwaka huu kesi hiyo itakapokuja mahakamani hapo kwa usikilizwaji wa awali.



Madarasa mapya kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule za Sekondari za Kata, Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara, yanaendelea kujengwa ili kuhakikisha wanaanza masomo haraka iwezekanavyo. Huu ni msingi wa moja ya madarasa yanayojengwa katika Shule ya Sekondari Nyambono. **PICHA: OFISI YA MBUNGE**

# Agizo la serikali mwiba kwa shule binafsi

**Na Paul William,** MOSHI

WADAU wa elimu mkoani Kilimanjaro wamesema agizo la serikali kuzuia shule za binafsi kutowarudisha wanafunzi ambao hawajalipa ada ni

kuzibebesha mizigo na kuzorotesha ubora wa elimu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wadau hao walisema kuwa agizo hilo la serikali ni kuzibebesha mizigo shule hizo na kuziua kutokana na shule hizo kutegemea ada za wanafunzi kujiendesha.

Walisema kuwa hilo ni wazo zuri na linatoa unafuu kwa wale wazazi ambao hawana uwezo mzuri lakini, ikumbukwe kwamba jambo hili ni ngumu kwa waendeshaji wa shule, walimu pamoja na wamiliki.

"Kumbuka shule binafsi hakuna ruzuku kutoka serikalini na asilimia kubwa tunategemea ada katika uendeshaji wa shule na kuwalipa walimu pamoja na watumishi wengine," alisema.

Askofu mstaafu wa T.A.G Jimbo la Kilimanjaro, Dk. Glorious Shoo, alisema kuwa nia ya serikali ni nzuri, lakini kuna haja serikali kuliangalia upya na kulipima kwanza.

"Jambo hilo ni ngumu sana mimi ningeshauri serikali ifikiri upya namna ya kuwasaidia wazazi wakatakaoshindwa kulipa ada kwa wakati kwa sababu baadhi ya shule ni za mabweni na watoto wanatakiwa kula pamoja na mishahara ya waalimu," alisema.

Alisema kuwa pia baadhi ya wazazi wanaweza kutumia fursa hizo kutolipa ada kwa makusudi kwa kisingizio kwamba serikali imeagiza wanafunzi wasirudishwe.

Alisema kuwa katika shule yake ya Fountain of Hope na Shule ya Fountain of Joy asilimia 30 ya wanafunzi ni wale wanaotoka kwenye mazingira magumu na kwamba hawalipi ada, hivyo asilimia 70 ya wanaolipa ada zinatumika katika uendeshaji wa shule.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Sayansi ya wavulana St. Joachim inayomilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo la Same, Deogratus Mchagi, alisema kuwa agizo hili litakwamisha uendeshaji wa shule binafsi

kutokana na kwamba wanategemea ada za wanafunzi kununua vifaa vya shule hasa kwa shule za sayansi.

"Tunategemea ada za wanafunzi kununua vifaa vya shule hasa kwa sisi ambao tunafundisha masomo ya sayansi na vifaa vya masomo ya sayansi vinauzwa ghali leo hii unasema wanafunzi ambao wasirudishwe nyumbani kweli jambo hili ni hatari," alisema.

Askofu wa Jimbo Katoliki Same, Rogathe Kimaryo, alisema kuwa serikali inatakiwa kukaa meza moja na wadau wa elimu ili kujadili masuala ya uboreshaji wa huduma za elimu.

Alisema kuwa huduma ya elimu inahitaji ushirikiano wa pande zote mbili ili kuangalia namna ya kuboresha elimu ya Tanzania.

# Wazazi wakalia kooni Bodi ya Shule

**Na Mary Mosha,** MOSHI

BAADHI ya wazazi wa Shule ya Msingi Mwangaria, iliyopo Kata ya Kahe Magharibi, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro wameiomba serikali kuvunja bodi ya uongozi wa shule hiyo kutokana na madai ya kutoshirikishwa katika miradi ya maendeleo ikiwamo kukatwa kwa miti bila wazazi kushirikishwa.

Wakizungumza jana katika kikao cha dharura cha uongozi wa shule hiyo na wazazi kilichofanyika shuleni hapo, Grayson Yusufu, alisema bodi hiyo chini ya uongozi wa mwenyekiti wao, Stantaely Saimon, umekuwa ukifanya mambo bila kuwashirikisha wazazi jambo ambalo linakwamisha maendeleo.

Alisema tumefikia hatua ya bodi ya uongozi hiyo ivunjwe kutokana na kushindwa kutushirikisha juu ya mambo ya miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kukata na kuiuza bila taarifa.

"Uongozi wa shule unatupa sababu nyepesi eti kulikuwa na pesa zinahitajika tukaamua kuuza miti hiyo bila kuwashirikisha jambo ambalo sisi hatukubaliani nalo...kama kuna shida yoyote tulipaswa kushirikishwa ili tuweze kuchangia kama wazazi kuliko kukata miti ya shule," alisema Magdalena Zakaria

"Miti hiyo tumeiotesha kwa gharama kubwa sana sisi kama wanakijiji na na hatutamruhusu mtu yoyote kuikata kutokana na hali ya hewa ya ukanda wa chini, hivyo tunajitaidi kutunza mazingira yetu wenyewe," alisema.

Akijibu tuhuma hizo Mwenyekititi wa Bodi ya shule hiyo, Saimon, alikiri kufanya hivyo na kusema kuwa fedha hizo zililekezwa kwenye matumizi madogo madogo ya shule ambayo yameonyeshwa kwenye mapato na matumizi.

"Tulilazimika kuuza miti hiyo kutokana na kuwepo kwa wageniwaliokuwa wakichimba kisima kama mradi wa maji katika kuwagharamia chakula cha mchana muda wote ambao walikuwa shuleni na matumizi mengine madogo madogo ya shule," alisema. Akizungumzia suala la kutowashirikisha wazazi, Saimon, alisema kuwa yapo baadhi ya matukio ambayo yanafanyika kwa udharura lengo ni kuja kuwashirikisha wazazi kwenye vikao, lakini imekuwa ikishindikana kutokana na wazazi kukaidi wito wa vikao mara kwa mara.

ama
ALHAMISI JANUARI 31, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 18

**Hivi ndivyo zilivyo safura na utapiamlo**



Ukurasa 17

Kimea cha nafaka zinavyoboresha mlo



Ukurasa 14

**Mitandao yakimbiza mahudhurio ya chanjo**



# KCMC yawanusuru walemavu ngozi ikiwazalishia dawa inayozuia kansa

Ukurasa 19

## Mitandao yakimbiza mahudhurio ya chanjo

**London,** Uingereza

WAKATI kuna himizo la kutakiwa kinga sahihi dhidi ya chanjo, hivi sasa kuna hofu inayosambazwa na mitandao ya jamii kwamba ina athari, wazazi wengi nchini wakiongoza kuikimbia.

Ripoti ya asasi ya kimataifa inayohusika na afya ya umma, iitwayo Royal Society for Public Health (RSPH), inafafanua kuna ujumbe hasi ambao unatikisa usalama wa watumiaji.

Shirley Cramer, Mtendaji Mkuu wa RSPH, anasisitiza kwamba, mamilioni ya maisha yamenusuriwa na chanjo na athari zinazotajwa ni adimu sana.

Akiunga mkono hoja hiyo, Ofisa Afya Mkuu wa Uingereza, Profesa Dame Sally Davies, anasema wazazi hivi sasa wajitahidi kukwepa upotoshaji kuhusu chanjo, badala yake wawawahishe watoto wao katika chanjo.

Hata hivyo, kuna ripoti ya kitafiti inayofahamisha kwamba kuna wastani asilimia 90 ya wazazi wanaopeleka watoto wao katika chanjo ya kitaifa, nchini, jumla yake zinafiklia 11.

Pia, katika sura nyingine utafiti umegundua kwamba, asilimia 10 ya wazazi bado wako katika msimamo wa kukwepa chanjo hizo.

Inaelezwa kuwapo athari chache za chanjo kama vile kuchoka na kuumwa kichwa.



Mtoto akipatiwa chanjo. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

SIMULIZI KUTOKA KILIMANJARO

# Dawa kulevya 'mfupa mgumu' safari ya kufikia afya bora ilipo



Kamanda wa Polisi Mkoa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP) Hamisi Issah (mwenye kaptula), akikagua shehena ya mirungi kilo 320, iliyokamatwa wilayani Hai ikisafirishwa kupelekwa mkoani Arusha, kwa kutumia gari aina ya Alphard. **PICHA ZOTE: JAMES LANKA.**

**Na James Lanka,** Moshi

USAMBAZAJI na uuzaji dawa za kulevya nchini, kama zilivyo sehemu nyingi duniani, bado kuna usugu wa tatizo, licha ya vita vikubwa vinavyopiganwa na serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama, ikiwamo Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Imeshuhudiwa kutajwa majina yenye hadhi kubwa ndani ya jamii yakihusishwa na dawa hizo, zinazouzwa kwa njia ya siri kubwa.

Ameshuhudiwa, Rais, Dk. John Magufuli, akimteua Rogers Sianga, kuwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini, ili kuongeza kasi ya kupambana na biashara hiyo haramu.

> **Kwa wanawake, kunakuwapo mabadiliko ya hedhi na kushuka mapigo yao ya moyo.**

Kabla ya kuundwa mamlaka, vita hiyo ilikuwa chini ya Kitengo cha Kupambana na Dawa za Kulevya, kilichokuwa chini ya Jeshi la Polisi

Inafahamika kwamba, nchi nyingi hasa zilizoendelea bado zinageuza ukanda uliopo, ikiwamo Tanzania kuwa njia ya kupitishia dawa hizo, hali inayoitia doa taifa katika sifa yake ya 'nchi ya amani na upendo.'

Umoja wa Mataifa umetenga siku ya Juni 26 ya kila mwaka, kupinga biashara na matumizi ya dawa za kulevya duniani na maadhimisho yake hufanyika kwa shughuli mbalimbali duniani, ikiwemo maandamano, hotuba, midahalo na kongamano.

Mathalan, mwaka 2007 kaulimbiu ililenga kuelimisha udhibiti dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya, yasitawale maisha yetu; mwaka 2008, ilitaka uzalishaji wa dawa za kulevya, usitawale maisha ya jamii; mwaka 2009, Biashara ya Dawa za Kulevya Isitawale Maisha Yetu.

### MADHARA YAKE

Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini, inaorodhesha aina za dawa za kulevya, kuu nchini ni: Heroin, cocaine, bangi na mirungi.

Heroin inayotajwa kuwa yenye madhara makubwa, chanzo chake kikuu ni mmea unaojulikana kama 'Opium Poppy' na inaelezwa kwamba, huingizwa nchini kutoka Mashariki ya mbali.

Moja ya vijarida ya iliyokuwa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya, inabainisha kwamba dawa hizo zina majina mengi mitaani kama vile; unga, brown sugar, ngoma, ubuyu, mondo, poda, dume na farasi

Pia, jarida lingine linalozungumzia dawa aina ya heroine, hutumika kwa njia ya kuvuta, kunusa unga, kunusa moshi 'kuchesi' na kujidunga, ili kuongeza wingi wa dawa.

Inaeleza kwamba wauzaji wengi wanaongeza sukari, kahawa, pia dawa za maumivu aina ya asprini na panadol, kuzalisha mchanganyiko unaoelezwa kuwa hatari na sumu zaidi kwa watumiaji.

### MADHARA YAKE

Inaelezwa kuwa, watumiaji wengi wanakumbana na madhara ya dawa hiyo, yanayojenga hali ya ulevi wa kuzubaa maarufu kama 'uteja,' kuliko dawa zingine.

Utafiti unaonyesha, katika kila watu wawili waliojaribu kutumia heroin, mmoja alifikia hali ya 'uteja na mtumiaji hupata usugu unaosababisha aongeze kiwango cha matumizi kila kukicha.

Madhara mengine ni uchafu wa mwili na kuishi kwenye mazingira machafu, kukosa umakini, kuzubaa na kupungua uwezo wa kufanya kazi, pia kuharibika kwa mfumo wa ubongo na fahamu.

Jarida linabainisha kwamba, mtumiaji wa dawa hizo anakumbwa na madhara katika moyo, ini kifua na mapafu.

Katika mfumo wa kuongea, mwathirika huyo huwa anapatwa na kigugumizi, kichefuchefu, kutapika na kufunga choo.

Kwa wanawake, kunakuwapo mabadiliko ya hedhi na kushuka mapigo yao ya moyo.

Sehemu kubwa ya madhara ni kwamba, matumizi ya dozi kubwa yanaangukia katika kifo. Pia, mchanganyiko wa heroin na pombe, inaleta madhara makubwa zaidi, ikiwa ni pamoja na kifo cha ghafla.

Watumiaji heroin kwa njia ya kujidunga, wanakaribia madhara

AFYA

# Dawa kulevya 'mfupa mgumu' safari ya kufikia afya bora ilipo



mengine ya maambukizi yaVirusi vya Ukimwi (VVU) na magonjwa mengine ya damu, sababu kuu ni kushirikiana sindano na vifaa vingine.

Kwa wenye ujauzito, ni pamoja na kupata matatizo ya upungufu wa damu, moyo, mimba kuharibika, kuzaliwa watoto njiti.

Madhara mengine, ni watoto kupata matatizo ya kiafya, ikiwamo kuchelewa kukua kiakili na kimwili, sambamba na kujifungua watoto ambao mara nyingi hufa wakiwa na umri chini ya miaka mitano.

Dawa nyingine zenye kuleta athari ni mirungi: Ni aina ya mimea inayostawi kwenye hali ya unyevunyevu na milima yenye urefu kati ya futi 4,000 hadi 9,000.

Nchini, mimea hiyo inapatikana kwa wingi kama uoto wa asili katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga. Hata hivyo, kiasi kikubwa cha mirungi inayopatikana nchini inatoka katika nchi jirani.

Kama ilivyo kwa heroine, mirungi mitaani imebeba majina kama ya miraa, mbaga, mogoka, veve, gomba na kashamba, ambapo madhara yake ni kutokea matatizo ya kisaikolojia kama kukosa hamu ya kula na kukosa choo; vidonda tumboni na mdomoni.

Kwa mujibu wa kijarida hicho, madhara mengine ni kupungua maji mwilini, shinikizo la damu, kukosa hamu ya kufanya mapenzi, mwili kuwasha, maumivu makali ya kichwa, kuharibika kwa ini na kupungua nguvu za kiume.

Pia, kuna vimiminika kama petroli, navyo vinatumiwa kama dawa za kulevya. Hapo inatumiwa kwa njia ya kuvuta hewa yake kupitia pua na mdomoni na kuzaa athari. Katika kundi hilo kuna vileo visivyoruhusiwa ambavyo hutengenezwa kienyeji, kama vile gongo.

Dawa za kulevya zinazotumika sana nchini ni pamoja na bangi, mirungi, mandrax, heroini na cocaine, inayopatikana katika hali ya unga mweupe na inatumiwa kwa njia ya kuvuta kwa pua au kuchanganywa na maji na baadaye kujidunga mwilini kwa kutumia sindano.

Heroin vilevile inaweza kupatikana katika vipande vidogo vya kahawia vijulikanavyo kama 'sukari ya kahawia.'

Njia nyingine ya kuzungumzia dawa za kulevya ni kutokana na madhara yake. Zipo dawa zinazopagawisha, kuzubaisha au kupoozesha kama vile kileo, nikotini, dawa za usingizi zinazomfanya mtumiaji kujisikia shwari, pia zinahuzunisha.

Dawa zinazochangamsha ni kama mirungi, cocaine na zile za kuvuta, kwa mfano petroli, zina madhara ya kumfanya mtumiaji ahamasike na kujisikia ana nguvu.

Kwa upande wa dawa zinazopagawisha, zinaleta hisia, sauti, taswira, harufu kwa mtu japokuwa, katika uhalisia vyote hivyo havipo. Bangi imo katika kundi hilo.

> **Baadhi ya watuhumiwa wanakamatwa na dawa hizo wakiwa wameficha tumboni, katika shanga za kimasai na mashine za maji.**

### MKOA KILIMANJARO

Katika kipindi cha mwezi huu unaoisha leo, polisi mkoa Kilimanjaro, ilinasa wasafirishaji na wauzaji wa dawa za kulevya, hasa mirungi katika maeneo mbalimbali, chanzo chake ni kutoka nchi jirani.

Ndani ya mtazamo wa jumla kuna historia ya kuwanasa watuhumiwa kutoka ndani na nje ya nchi, katika viwanja vya ndege nchini, ukiwemo Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KIA), uliopo mkoani Kilimanjaro.

Ni watuhumiwa walionaswa na dawa za kulevya za aina mbalimbali, zikiwemo cocaine na heroin.

Katika tukio lililovuma mwaka jana lilihusisha vijiji 28 vya ukanda wa milimani vilivyopo wilayani Same mkoani Kilimanjaro, kubainika kuwa na mashamba makubwa ya dawa za kulevya aina ya mirungi zikichukua ekari nyingi mafichoni.

Kutokana na uzio na ukubwa wa tatizo hilo, vyombo vya ulinzi na usalama mkoani hapa vilianzisha opereseni kabambe ya kuteketeza mashamba yote ya mirungi, iliyoongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro wakati huo; Amos Makala.

Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Hamis Issah anasema anaendeleza mapambano dhidi ya mirungi, chini ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mkuu wa Mkoa, Anna Mghwira.

Tukio la hivi karibuni lililotokea Januari 11 na Januari 12, polisi mkoa ilipowakamata wasafirishaji wa mirungi katika mabasi yanayosafiri kati ya Moshi na Arusha.

Kwa mujibu wa Kamanda Issah, Januari 12 mwaka huu walimnasa, mkazi mmoja akisafirisha kilo 79.5 za mirungi kutoka Moshi kwenda Arusha, kwa kutumia gari dogo aina ya Noah, katika mji mdogo wa Bomang'ombe, wilayani Hai.

Pia, anataja siku chache zilizopita, Jumapili Januari 27 mwaka huu saa tisa alasiri, polisi ilinasa magunia matatu na viroba 11 vilivyojaa mirungi, vikisafirishwa na gari binafsi aina ya Toyota Alphard, wilayani Hai, Kilimanjaro.

Kamanda ACP Issah, anasema watuhumiwa wake walikimbia na kulitekelekeza gari katika kizuizi anachokitaja 'KIA Junction' baada ya kubaini wanafuatiliwa na polisi. Zilipatikana kilo 320 za mirungi.

### MATUKIO MENGINE

Takwimu zinaonyesha, Polisi Kikosi cha Viwanja vya Ndege, limekamata zaidi ya kilo 14 za dawa za kulevya katika viwanja vya ndege vya kimataifa vya Julius Nyerere (JNIA) Dar es Salaam na Kilimanjaro (KIA) mkoani Kilimanjaro, katika kipindi cha mwaka jana.

Idadi hiyo inatajwa kuwa kubwa baada ya ulinzi kuongezwa katika viwanja hivyo, tofauti na ilivyokuwa mwaka 2015, zilipokwapo kilo 3.583 za heroine zilipokamatwa.

Aliyekuwa Kamanda wa Polisi wa Viwanja vya Ndege, Martin Otieno, anasema ripoti ya mwaka jana, inaonyesha kilo 9.364 za dawa za kulevya aina ya heroine na kilo 5.73 za cocaine, zilikamatwa kutoka kwa watuhumiwa 13 tofauti, zilipoingizwa kupitia viwanja hivyo, kutoka nchi mbalimbali duniani.

"Wauzaji wa dawa za kulevya, wamekuwa wakitumia njia mbalimbali kila kukicha. Wapo wanaoficha katika soli za viatu, mfano kuna mtu alitokea Liberia, alikuwa ameficha katika taulo za watoto (pampers)," anasema Kamanda Otieno.

Anasema, baadhi ya watuhumiwa wanakamatwa na dawa hizo wakiwa wameficha tumboni, katika shanga za kimasai na mashine za maji.

Kimsingi sheria zinazodhibiti dawa za kulevya nchini, zinatoa adhabu kali, ambazo ni faini kali na kifungo cha muda mrefu.

***• Mwandishi wa makala anapatikana kwa anwani ya barua pepe: jlanka6@gmail.com na simu: (+255) 752 691 129.***

AFYA

## SIMULIZI KUTOKA KIBONG'OTO

# 'Gereji' kuu ya TB nchini inayotimiza umri karne

**Na Mary Geofrey,** aliyekuwa Hai

- Mkurugenzi ashuhudia mafanikio ya kimataifa
- TB sasa kila wilaya 'kiwango cha Kibong'oto'

KIBONG'OTO ni hospitali maalum ya kutibu Magonjwa yanayoambukiza kama Kifua Kikuu (TB), kwa wagonjwa wote nchini iliyopo wilayani, Siha mkoa wa Kilimanjaro.

Hospitali hiyo ilianza mwaka 1926 kama kituo cha kutunza wagonjwa wa TB, wakati huo hakukuwapo tiba za ugonjwa huo duniani kote.

Mwaka 1956, dawa za kutibu TB ya kawaida zilianza kupatikana duniani, hivyo kituo kilianza kutoa huduma za matibabu.

Hospitali hiyo ilianza kutoa tiba na mwaka 2009, serikali iliamua kituo hicho kiwe maalum cha kutibu ugonjwa wa TB sugu.

### MKURUGENZI HOSPITALI

Kaimu Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Dk. Riziki Kisonga, anaeleza historia hiyo katika mazungumzo maalum na maofisa mawasiliano kutoka taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, katika ziara ya kukagua mafanikio ya miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk.John Magufuli, katika sekta hiyo nchini yenye kaulimbiu: 'Tumeboresha Sekta Afya.'

Anasema, kuanzia wakati huo wanatoa tiba za TB za viwango mbalimbali: TB sugu zaidi na za kawaida.

Pia, wanatibu magonjwa yanayoambukiza, kutoa mafunzo na kutibu watu walio jirani na hospitali hiyo na kufanya utafiti wa vimelea vya kifua kikuu. Dk. Kisonga anaongeaza: "Hatubagui wagonjwa wote wa kifua kikuu Tanzania nzima wanakuja kutibiwa hapa."

Dk. Kisonga anasema kwamba, mwaka 2009 walianza kutoa huduma kwa agonjwa 16 waliosajiliwa kutoka mikoa yote na kwa sasa wanalaza wagonjwa 168, huku idadi ikiendelea kuongezeka kadri siku zinavyosonga mbele.

### UNAIELEWAJE TB?

Dk.Kisonga anataja kwamba, kuna aina mbili za kifua kikuu; kinachoshambulia mapafu na kinachoshambulia nje ya mapafu.

Anasema, ugonjwa huo chanzo chake ni uchafuzi wa mazingira unaosababisha vimelea kushambulia mapafu na kusababisha maradhi

Dk. Kisonga anasema mtu akipata maambuzikizi ya TB yanapokutana na kinga za mwili, vimelea vinaweza kwenda kujificha sehemu yoyote kwenye mwili na kukaa hata miaka 10 bila ya dalili kujitokeza.

Anasema inapotokea akapata mtu mwenye kinga dhaifu, ndipo anaweza kupata maambukizi na dalili kuonekana ndani ya mwaka mmoja.



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, akikagua huduma za hospitali ya Kibong'oto iliyopo wilayani Hai. Katika picha nyingine, akizungumza na watumishi wa hospitali hiyo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **Kuanzia wakati huo wanatoa tiba za TB za viwango mbalimbali: TB sugu zaidi na za kawaida.**




Dk. Kisonga anasema takwimu za nchini, zinabainisha kuwapo jumla ya wagonjwa 63,000 kila mwaka mwaka kuwa na maambukizi ya TB na katika hao, kuna wagonjwa wa marudio na waliopona moja kwa moja.

"Asilimia moja ya wagonjwa sugu wa dawa wanarudia kupata TB na na asilimia 3.1 ya wagonjwa wapya wanakuwa na kifua kikuu sugu nchini," anasema Dk. Kisonga na kuongeza: "Hivyo tukipiga hesabu, utakugundua kuwa wapo wagonjwa wengi wa mtaani wanazunguka na hawajaanza matibabu."

Mtaalamu huyo anasema, ugonjwa huo unashambulia maeneo ya nywele na kucha na hivyo jamii inapaswa kuwa makini na mabadiliko ya miili yao.

"Mtu mmoja mwenye TB ambaye hajaanza matibabu, anaweza kuambukiza watu 20 wapya kwa mwaka," anasema.

Kwa mujibu wa Dk. Kisonga, kuna jumla ya wagonjwa wa TB kati ya 400 hadi 500 wanaogundulika kwa mwaka na wagonjwa 168 wa TB sugu ndani ya kipindi hicho.

Anasema gharama za matibabu kwa kila mgonjwa, ni kati ya Sh. milioni nane hadi 16, kuanzia hatua ya kwanza hadi ya mwisho. Gharama ambazo zinatolewa na serikali pamoja na chakula kwa wagonjwa wote.

Dk. Kisonga anasema, jumla ya wagonjwa waliolazwa wodini ni 123 na wagonjwa wenye usugu wa dawa, ndio wanakabiliwa na tatizo la njaa zaidi.

Anataja takwimu za miaka mitatu kuanzia mwaka 2015 hadi 2018; mwaka jana walipokea wagonjwa 317; mwaka 2017 walipokea wagonjwa 167; mwaka 2016 walipokea wagonjwa 142; na mwaka 2015 walipokea wagonjwa 148.

### MAFANIKIO YAO

Dk. Kisonga anasema, mafanikio yaliyopatikana ni kushirikiana na Kitengo cha Kudhibiti Ugonjwa wa TB, wamewafikia Watanzania wengi na kufungua vituo 89 nchini.

Anasema, baada ya kufungua vituo vingine katika mikoa mbalimbali, wamegundua wagonjwa wapya na kuwaanzishia matibabu mapema.

Mtaalamu huyo, anasema kwa jijini Dar es Salaam wana jumla ya vituo 12, ambavyo vinapima ugonjwa wa TB na kutoa tiba badala ya wagonjwa kufuata huduma hiyo, mkoani Kilimanjaro.

Anasema wamefanikiwa kununua mashine kubwa na za kisasa za kufanya uchunguzi wa ugonjwa huo wa kifua kikuu, zenye thamani ya Sh. milioni 201,123.

Dk. Kisonga anasema serikali imetoa fedha Sh. bilioni 2.1 kwa ajili ya kujenga maabara ya kisasa ya kutoa huduma za tiba, kwa wagonjwa na kufundishia wanafunzi na kusaidia tafiti zinazofanyika kuwa za kiwango cha juu.

"Kwa sasa serikali itakuwa na maabara tatu, moja ipo Hospitali ya Taifa Muhimbili, nyingine Mabibo (Dar es Salaam) na moja ndio inajengwa hapa Kibong'oto (Kilimanjaro) na ujenzi wake utakamilika mwaka 2020," anasema.

Mkurugenzi huyo wa Kibong'oto anasema, wamefanikiwa kubaini wagonjwa wapya kutoka kituo chao kipya walichojenga katika machimbo ya Mererani mkoani Manyara na watu 2,561 walipimwa afya zao.

"Katika Kituo cha Merenani tumepima na kubaini kuwa watu 13,800 kati ya 100,000, wanaugua kifua kikuu na tayari serikali imeshaweka mikakati ya kupunguza ugonjwa huo," anasema Dk. Kisango.

Hata hivyo, katika kukabiliana na changamoto, hospitali hiyo inatoa elimu ya kujikinga kwa wafanyakazi wa migodini, pia wamenunua mashine za kisasa kubaini wagonjwa wakiwa katika hatua za awali na kupata majibu kwa muda mfupi.

"Katika kukabiliana na changamoto hii, tumeanza kutoa elimu kwa jamii hiyo, kuwahasa watumie vifaa vya kujikinga wanapokuwa migodini kwa sababu kinachowaathiri ni lile vumbi ambalo linashambulia mapafu na hatimaye kusababisha vimelea vya TB kuingia ndani ya mwili," anasema Dk. Kisonga.

Anasema hadi sasa hospitali hiyo inalaza wagonjwa wa TB 123 kwa mwaka wakiwamo 86 sugu na wagonjwa 32 wenye TB ya kawaida.

Anasema wana mashine ya kubaini usugu wa dawa daraja la kwanza na la pili, kwa muda usiopungua saa 48 na kubaini usugu na dawa na kuweza kubaini usugu wa dawa wanazotumia.

Dk. Kisonga anasema, hadi sasa idadi inaongezeka kwa sababu mashine za kugundua TB kwa haraka ndani ya saa mbili ziko 77.

Pia, anaongeza kuwa mwishoni mwa mwaka jana, serikali ilisambaza mashine za kupima TB haraka ndani ya saa mbili katika kila wilaya nchini, Dk. Kisonga anadokeza kwamba ni kati ya sababu ya wagonjwa wengi kupelekwa hospitali na kuanza tiba.

Anasema, kwa sasa wanatoa elimu kwa jamii kutambua dalili za ugonjwa, lakini anataadharisha kwamba kwa wenye maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU), utapiamlo, wanaotumia dawa za kutibu kansa, huwa zinashusha kinga za mwili, hivyo wana uwezekano mkubwa wa kupata maambukizi ya TB.

> **Hadi sasa hospitali hiyo inalaza wagonjwa wa TB 123 kwa mwaka wakiwamo 86 sugu na wagonjwa 32 wenye TB ya kawaida.**

Dk. Kisonga anasema katika moja ya mafanikio ya tiba ya TB sugu wameshuhudia katika wagonjwa 100, kati yao 75 wanapona nchini.

Anaitaja kuwa mafanikio, kwa sababu wastani wa kimataifa ni katika kundi la wagonjwa 100, kati yao 56 ndio wanapona, huku akijisifu katika hatua aliyofikia ni kwamba, katika orodha ya wagonjwa wake wanaougua TB sugu, hakuna wanaojirudia tena.

Anaeleza kuwa, wagonjwa wa TB huwa wanapata magonjwa ya figo na uziwi kutokana na matumizi ya sindano za TB na hao wanaothirika wako asilimia 12 ya wagonjwa wanaotibiwa TB.

Pia, anasema wanaongeza vituo vya kubaini wagonjwa hao, katika kila wilaya kunatakiwa kuwapo chumba maalum cha kuwalaza.

Hiyo inaendana na kuwapo, maabara ya kisasa inayowasaidia kuwafahamisha uwapo wa vimelea vya ugonjwa huo.

Pia anasema, wana mpango wa kuanzisha maabara inayotembea ili kufika kwenye jamii kwa ajili ya kutoa elimu na kufanya vipimo.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Dunuani (WHO) kati ya kila watu 100,000, wapo watu 246 wanaugua TB duniani.

---

# Kimea cha nafaka zinavyoboresha mlo

**Na Barnabas Maro**

UTUMIAJI wa mbegu zilizooteshwa ili kupata kinachoitwa 'kimea' ni moja ya teknolojia za asili zinazotumika kuboresha chakula cha kulikiza.

Teknolojia nyingine inayotajwa, ni pamoja na kuchachua vyakula, kama inavyofanyika kwa kinywaji cha togwa.

Ndani ya msamiati wa Kilimo na Lishe; kimea ni mbegu za nafaka zilizooteshwa (zilizomea au zilizochipua) zinazotumika katika uboreshaji chakula na kumpatia mlaji lishe bora.

Kimea, kinafahamika na kutumika katika mlo wa makabila jamii nyingi ndani na nje ya nchi. Kiasili au katika mtazamo wa jadi, makabila mengi yanatumia kimea, kwa ajili ya kutengeneza pombe, mfano mmojawapo ni togwa.

Pia, kuna sura ya pili ya matumizi hayo kwamba, inatumika katika mtazamo wa sura au jami ya uji unaopikwa.



Kijana akipata kinywaji cha togwa. **PICHA: MTANDAO**

### FAIDA & INAVYOTAYARISHA

Faida za matumizi ya kimea: Unga wa nafaka iliyooteshwa, yaweza kutumika kwa wingi kutayarisha uji mwepesi wenye virutubisho vingi.

Kimea kikiongezwa kwenye lishe hiyo, inarahisisha uyeyushaji wake na matumizi ya chakula tumboni kwa mtoto.

Pia, kuna suala la uoteshaji wa mbegu, ili kukipata kimea hicho, ni jambo linalosaidia kupunguza viini vinavyozuia ufyonzaji wa virutubisho husika.

Jinsi ya kukitayarisha kimea: Mwanzo, unatakiwa kuchukua nafaka ya aina yoyote kama vile ulezi, mahindi, mtama au uwele.

Hatua inayofuata ni kuupepeta na kisha kuchagua, ili kuondoa taka na mbegu ambazo hazijakomaa au zilizooza na kisha safisha nafaka, ili kuondoa vumbi.

Ngazi nyingine ni kuiloweka katika maji mengi (maji yafunike nafaka) kwenye chombo usiku kucha na siku inayofuata, mtu unatakiwa kuondoa nafaka kwenye maji na kusafisha tena, ili kuondoa povu husika.

Baada ya hapo, weka nafaka iliyolowekwa katika ungo au gunia safi, kisha sambaza na funika. Acha nafaka sehemu yenye kivuli ili iote kwa siku moja.

Kinachofuata, ni kuangalia kama nafaka hiyo imeota, pia kama kuna ukungu ulioota, isafishe nafaka hiyo kuondoa ukungu. Irudishe nafaka kwenye chombo cha kuoteshea na acha iendelee kuota kwa siku moja au zaidi.

Nafaka ikishaota, itoe na ianike katika chanja na hakikisha imekauka kabisa. Hapo ndio inakuja jukumu la kuitwanga, ili kupata unga. Huo ndio unajulikana kama 'unga wa kimea.'

Unga huo unatakiwa kuwekwa katika kimea cha chombo kilichokauka na kisafi, kifunikwe na kuhifadhiwa.

### UJI WA KIMEA

Uji wa kimea unaweza kupikwa kwa kutumia unga wa kimea peke yake, kupika uji mzito kwa kutumia unga wa kawaida, kisha kulainisha kwa kutumia unga wa kimea.

Mtayarishaji anaweza kuchagua njia mojawapo kati ya hizo mbili anapopika uji wa kimea. Njia ya kutumia unga wa kimea peke yake, mapishi yake ni sawa na yale yanayotumika wakati wa kupika uji wa kawaida. Tofauti iliyopo, ni kwamba unga mwingi zaidi hutumika unapopikwa uji wa kimea, kuliko unapopikwa uji wa kawaida.

Kutayarisha uji wa kimea kwa kutumia unga wa kawaida: Hapo inaanza kwa kuandaa uji mzito unaotosha mlo mmoja wa mtoto.

Baada ua kuiva, uji huo unaachwa upoe mpaka unapofikia hatua ya kuwa na vuguvugu. Baada ya hapo, mtu anatakiwa aongeze unga wa kimea kijiko kimoja cha chai au mfinyo wa vidole vyako vinne, kisha anakoroga uji uchanganyike na kimea.

Hapo, kunatakiwa kuendelea kuongeza unga wa kimea na kukoroga, hadi uji ulainike na kuwa maji maji. Urudishe uji jikoni na uchemshe tena kwa muda mfupi kisha ipua, ongeza sukari au chumvi ili kuongeza ladha, upooze na mlishe mtoto.

**• Makala hii imeandaliwa kwa mujibu wa taarifa za Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania na Mwandishi anapatikana kwa anuani ya: barua pepe marobarnabas@yahoo.com au simu: (+255) 0784 334 096**

AFYA

# Hivi ndivyo zilivyo safura na utapiamlo



Vyoo vya umma vinavyoonekana ambavyo ni moja ya vyanzo vya kichocho. **Picha ndogo;** mgonjwa wa utapiamlo akipatiwa matibabu. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Barnabas Maro**

SAFURA ni ugonjwa unaosababishwa na minyoo au michango inayoitwa tegu au kitalaamu 'hookworms,' unaopatikana katika nchi zilizoendelea na zinazoendelea.

Aina ya minyoo wanaosababisha ugonjwa huo wako wa aina mbili; Kutoka jamii ya 'hookworms' ambao ni 'ancylostoma duodenale' na waitwao kitaalamu 'Necator Americanus.'

Minyoo hiyo inaishi kwenye utumbo mdogo wa chakula na unawapata sana watoto walioko shuleni na wakati mwingine watu wazima

Ile inayohusu safura inatajwa kuwa ya hatari na kusababisha upungufu wa damu mwilini, ikileta madhara ya kiafya kwa binadamu na inaelezwa kuhatarisha maendeleo ya jamii kwa jumla.

**DALILI ZAKE**

Dalili za safura zinatajwa kuwa; mtu anasumbuliwa na maradhi ya kikohozi kikavu kinachosababishwa na minyoo kuingia kwenye mapafu hadi tumboni.

Matokeo ya hatua hiyo ni kuumwa tumbo, kuharisha, kupungua uzito na upungufu wa damu.

Kwa kawaida, safura inaenezwa kwa njia ya kinyesi cha binadamu. Tatizo hilo huwa kubwa miongoni mwa jamii isiyokuwa na vyoo majumbani. Mtu mwenye safura anapoenda haja ovyo bila ya kutumia choo, husambaza minyoo ardhini.

Pia, kuna watu wanaoishi kwenye eneo hilo lililojaa wadudu hao, hupenya katika ngozi zao na wanasonga hadi kwenye mishipa ya damu na kusafirishwa mpaka kwenye utumbo wanakoishi na kuzaliana.

> **Wanawake wajawazito na wenye umri chini ya miezi sita, baada ya kujifungua, mzingo wake huwa sentimeta 19.0 au zaidi.**



Minyoo ya safura inaishi kwa kufyonza damu ya binadamu na inajishikiza kwenye utumbo, hali inayosababisha uvujaji mwingi wa damu kwa mwanadamu.

**KUJIKINGA**

Inashauriwa, kaya zijenge vyoo na kukitumia itakiwavyo' watu wanawe mikono kila waingiapo na kutoka chooni.

Hiyo inaendana na kunawa mikono kabla ya kuandaa chakula; kuosha matunda kabla ya kula; kupenda kuvaa viatu; kutumia dawa ya minyoo kila mara, kwa kuzingatia maelekezo ya waganga wa zahanati.

Mengine yanayochangia upungufu wa damu, ni magonjwa ya malaria na kichocho; pia ulaji duni wa vyakula vinavyokosa matunda, mboga za majani, nyama, dagaa, samaki na vinginevyo.

Magonjwa ya malaria na kichocho nayo yanasababisha upungufu wa damu mwilini.

**TIBA YA UTAPIAMLO**

Utapiamlo wa nishati na utomwili ni moja ya matatizo ya kiafya yanayoathiri jamii. Ni ugonjwa unaojitokeza kwa watu wengi wenye maradhi kama vile Virusi vya Ukimwi (VVU).

Wenye VVU hushindwa kula chakula cha kutosha na wana ufyonzaji duni wa virutubishi mwilini na mahitaji yake yanaongezeka.

Pamoja na kuwapo jitihada za kitabibu, watu wengi wenye VVU hupoteza maisha kwa kukosa lishe bora. Hivyo, kuna umuhimu mkubwa wa kufuatiliwa hali zao za lishe, ili kuchukuliwa hatua za kuboresha ulaji wao, ikiwa ni pamoja na matibabu kwa kutumia chakula na dawa.

Mtu mwenye utapiamlo wa nishati ya utomwili, hutambuliwa kwa viashiria vya uwiano wa uzito wa mwili na eneo la nje ya mwili.

Kiashiria hicho kinajulikana kama farihisi, ambacho hupatikana kwa kupima mzingo wa mkono wa kushoto, katikati ya kiwiko na kifundo cha bega na uvimbe wa miguu yote miwili unaobonyea.

**AINA ZAKE**

Utapiamlo umegawanyika katika sehemu kuu mbili: Utapiamlo Mkali na Utapiamlo wa Kadri.

Matibabu ya utapiamlo mkali: Kwa watoto wenye umri wa miaka mitano hadi 14, huwa na dalili za uvimbe wa miguu yote miwili (inayobonyea), anakosa hamu ya kula, damu inakosa wekundu ulioko lea.

Ili kuwatibu, vijana wanaoanzia umri wa miaka 15, kinamama wasio wajawazito, wasionyonyesha na wanaume watu wazima, wanastahili kupewa pakiti sita za gramu 92 za chakula dawa (kilokalori 3,000) kwa siku na waendelee kula chakula cha familia au cha nyongeza, chenye virutubishi kwa wingi.

Wanawake wajawazito na wenye chini ya miezi sita baada ya kujifungua, wanapaswe pakiti sita ( gramu 92) za chakula dawa ambazo ni sawa na kilokalori 3,000 kwa siku, pamoja na vyakula mchanganyiko vyenye virutubishi kwa wingi.

Vigezo vya kuachisha huduma ya chakula dawa: Mtoto mwenye umri wa miaka mitano hadi tisa mwenye hamu ya kula. Anapaswa aendelee kupatiwa chakula cha familia, ikiambatana na nyongeza yenye virutubishi kwa wingi.

Miaka10 hadi 14: Ni kwa mtoto mwenye hamu ya kula na mwenye mzingo wa mkono wa sentimeta 16.0 au zaidi,

Pia, wako vijana wenye umri kuanzia miaka 15, wanawake wasio wajawazito na wasionyonyesha na wanaume watu wazima, mzingo wao wa mkono ni sentimeta 19.0 au zaidi.

Wanawake wajawazito na wenye umri chini ya miezi sita, baada ya kujifungua, mzingo wake huwa sentimeta 19.0 au zaidi.

Utapiamlo kadiri; Kwa watoto wenye umri wa miaka 5 hadi 14, endapo ametoka kwenye matibabu ya utapiamlo mkali, anapaswa kupewe pakiti moja ya chakula dawa kwa siku na ale chakula cha familia au cha nyongeza, chenye virutubishi kwa wingi.

Endapo mlengwa ni mgeni (hatoki kwenye matibabu ya utapiamlo mkali), anatakiwa apewe chakula cha familia au cha nyongeza chenye virutubishi vingi.

Vijana kuanzia miaka 15, wanawake wasio wajawazito na wasionyonyesha na wanaume watu wazima, wanafaa waendelee kula chakula cha familia au cha nyongeza chenye virutubishi kwa wingi, ili kukidhi mahitaji ya mwili.

Kinamama wajawazito wenye umri chini ya miezi 6 baada ya kujifungua nao waendelee kula chakula cha familia na cha nyongeza (panapotolewa huduma hiyo) yenye virutubishi kwa wingi.

Uachishaji huduma: Una vigezo tofauti kuzingatia umri, ujauzito, uzito na mzingo wa ukubwa wa eneo la mzingo wa mikono yao

• ***Makala hii kwa mujibu wa marejeo ya maandiko ya Taasisi ya Chakula na Lishe. Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa simu (+255) 0784 334 096 na barua pepe:marobarnabas@yahoo.com***

AFYA

## SIMULIZI KUTOKA KILIMANJARO

# KCMC yawanusuru walemavu ngozi ikiwapatia dawa kansa

• Inawagawia bure walengwa 25,000 • NHIF yawapatia mkopo mabilioni • Wamrithi mfadhili, wajitutumua...

**Na Mary Geofrey,** aliyekuwa Moshi

HOSPITALI ya Rufaa ya KCMC, ni pekee inayozalisha mafuta maalum kwa ajili ya kuwahudumia watu wenye ulemavu wa ngozi albino nchini.

Hospitali hiyo iliyopo katika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, inatoa huduma ya kutengeneza mafuta hayo na kuyagawa bure kwa Watanzania zaidi ya 5,000 kila mwaka.

Mamlaka ya hospitali hiyo, inalenga kutoa huduma hiyo bure kwa watu wenye ulemavu wa ngozi wanaokadiriwa kufika 25,000 nchini kote.



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, akikagua Benki ya Damu, iliyopo hospitalini KCMC, Moshi.

**WATALAMU NGOZI**

Mtaalamu wa kutengeneza mafuta hayo, Mhandisi Ebeneza Fabian, anawaambia wanahabari walioandamana na maofisa mawasiliano wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, katika ziara ya kukagua uboreshaji sekta hiyo, yenye kaulimbiu: "Tumeboresha Sekta ya Afya."

Akizungumza na Nipashe, Fabian, anasema kitengo cha kutengeneza mafuta hayo, kilianzishwa mwaka 2013 wakati huo kikihudumia watu 25, lakini sasa wenye ulemavu wa ngozi wanaohudumiwa wako 5,000 kwa mwaka.

Mhandisi Fabian anasema wanatengeneza mafuta kwa ajili ya watu wazima na watoto wadogo na wanayagawa bure na wanaohudumiwa mafuta hayo wanatoka katika mikoa 25 ya Tanzania Bara na Visiwani, lengo ni kuwafikia wahitaji wote nchini.

Kwa mujibu wa Mhandisi Fabian, mwenye ulemavu wa ngozi, anapofika hospitalini, anapatiwa daktari maalum wa ngozi anayemchunguza hitaji lake na kumpatia kopo la mafuta kwa ajili ya kutumia.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Ngozi, Dk. Daudi Mavura, anasema moja ya vitu vinavyowasaidia watu wenye ulemavu wa ngozi wasipate kansa ni mafuta hayo.

Anasema mbali na mafuta, wanapaswa kutumia vifaa vya kujikinga kama vile kofia, miamvuli, nguo za kufunika mikono na miguu, ili kuwasaidia wasipate maradhi ya kansa ya ngozi.

Anasema mafuta hayo ya kuzuia mwanga wa jua yanayotengenezwa nchini, yana ubora wa hali ya juu kuwakinga kikamilifu wenye ulemavu wa ngozi.

Dk. Mavura anasema, yapo mafuta yanayotengenezwa nje ya nchi, lakini kutokana na hali ya hewa iliyopo, yanawahi kuyeyuka.

> **Kwenye upande wa ngozi, tunatoa huduma za mafuta maalum ya kuwakinga watu wenye ulemavu wa ngozi na tunayatoa bure kwa mikoa 22.**




Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali ya KCMC, Dk. Gileard Masenga (kushoto), akiwa katika majukumu yake kazini. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Anaongeza kuwa mafuta hayo yanayotoka nje ya nchi, yana harufu ya manukato ambayo kuna wakati yanawasumbua wenye ulemavu wa ngozi, tofauti na yanayotengenezwa nchini hayana harufu ya manukato.

Anasema mafuta hayo yenye uzito wagramu 300, hayauzwi na Dk. Mavura anaongeza: "Gharama ya mafuta kwa kopo moja ni 25,000 na tunatengeneza makopo mengi ya kuhudumia watu zaidi ya 5,000 kila mwaka. Tunatoa huduma hii kwa kipindi cha miaka sita mfululizo sasa."

Anasema, malighafi za kutengeneza mafuta hayo wanayatoa nje ya nchi na zinapoingia nchini, hayatozwi ushuru na ndio sababu ya kugawa bure na endapo yangetozwa ushuru, yangeuzwa.

"Kwa kipindi cha Desemba hadi Machi, huyu mfadhili anayetuletea mafuta alisitisha huduma. Hospitali tulilazimika kuendelea kutoa huduma kwa wenye ulemavu wa ngozi na kwa miezi hiyo minne, tulitumia milioni zaidi ya 54," anasema Dk. Mavura.

Anasema kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2016 waligawa kwa watu 4,000; mwaka 2017 waligawa kwa watu 5,055; na mwaka 2018 waligawa kwa watu 6,000.

"Bado kuna changamoto ya kuwafikia watu kwa sababu nchini kuna watu 25,000, lakini tumewafikia 6,000 tu, ina maana watu 19,000 bado wanasubiri huduma zetu," anasema.

Mkurugenzi KCMC

Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, Dk. Gileard Masenga, anasema wanatibu ugonjwa wa macho na ngozi, ikiwamo kwa watu wenye ulemavu wa ngozi.

"Kwenye upande wa ngozi, tunatoa huduma za mafuta maalum ya kuwakinga watu wenye ulemavu wa ngozi na tunayatoa bure kwa mikoa 22,'" anasema.

Anasema, serikali inawezesha malighafi ya kutengeneza mafuta hayo na kutotozwa kodi kunachangia kurahisisha utoaji huduma kwa walengwa.

Pia, anakumbusha katika jukumu la uzalishaji, hitaji la aina

INAENDELEA UK.20

AFYA




# KCMC yawanusuru walemavu ngozi ikiwapatia dawa kansa

**INATOKA UK.19**

hiyo si la wakati wote wafadhili wanaweza kutoa bure huduma za malighafi, hivyo kinachofanyika ni kushirikiana na serikali kuagiza bidhaa hiyo, ili kuzalisha bidhaa kwa wingi badala ya kuendelea kutegemea wafadhili.

**HUDUMA MATIBABU**

Mkurugenzi huyo, Dk. Masenga, anasema hospitali hiyo ina jumla ya vitanda 639 na majukumu wanayotekeleza, ni kutoa huduma ya tiba, pia wanafundisha kupitia chuo chao na kufanya tafiti za tiba mbalimbali.

Anasema, awali hospitali hiyo ilikuwa na vitanda 400 na katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, wameongeza idadi zaidi ya 200.

Dk. Masenga anafafanua zaidi, akisema idadi ya wagonjwa wa nje wanaopokea kila siku ni kuanzia 800 hadi 1,000 wote wanapatiwa huduma na kuondoka.

"Kiukweli hatuwamudu, tuna upungufu wa watumishi, kwa sababu daktari mmoja analazimika kuhudumia zaidi ya idadi inayotakiwa," anasema.

KCMC ni hospitali inayomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), kwa kushirikiana na serikali inayotoa ajira kwa wastani wa asilimia 95.

"Kazi ya serikali ni kutoa ajira na kazi ya hospitali na kutoa huduma na kurekebisha majengo na shughuli nyingine za hospitali," anasema.

Pia, anasema katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi uliopo nchini, huduma za hospitali hiyo zimeboreshwa zaidi, akitaja kwa kutibu wagonjwa wengi kwa mfumo wa Bima ya Taifa ya Afya (NHIF) Dk. Masenga anasema, pia wanatibu wagonjwa wa saratani na kutoa wagonjwa wa moto ambao wana wodi maalum.

Anasema sekta ya viungo bandia nayo imeboreshwa na wanatoa viuongo bandia kwa wagonjwa waliokatwa viungo kutokana na ajali mbalimbali.

Dk. Masenga anaeleza hatua zinazochukuliwa kukabili walakini wa kimahitaji kutoka kwa wagonjwa, wameagiza mashine za kisasa za uchunguzi (MRI na Ct-scan) zenye gharama ya Sh.. bilioni nne.



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, akikagua dawa za ngozi, zinazotengenezwa hospitalini KCMC, Moshi. **PICHA: MTANDAO**

> **KCMC inatekeleza majukumu yake vizuri kutokana na kazi zake nzuri ambazo zimekuwa zikifanywa.**

Anasema, hizo zimetokana na mapato ya ndani ya hospitali, zitakazosaidia kufanya uchunguzi kwa wagonjwa wao.

Kwa mujibu wa Dk. Masenga, changamoto kubwa waliyo nayo ni uhaba wa wafanyakazi na serikali imekuwa ikitoa vibali vya kuajira, ingawa bado hawatoshelezi mahitaji, hata kuifanya hospitali kutumia pato lake la ndani kuongeza matumishi.

"KCMC inatekeleza majukumu yake vizuri kutokana na kazi zake nzuri ambazo zimekuwa zikifanywa," anaeleza.

Anasema awali walikuwa na CT-Scan waliyoinunua kwa Sh. milioni 600, lakini bado haitoshelezi mahitaji na ndio sababu ya kuongeza mashine nyingine mpya.

Akitaja kiwango cha utendaji, kwa wastani wanawafanyia vipimo wagonjwa 40 hadi 50 kupitia mashine za MRI na CT-Scan.

Pia, katika kitengo cha mafunzo ya viungo bandia, huwa wanapata wanafunzi kutoka nchi mbalimbali duniani, jambo anabalo ni ishara njema Tanzania wanatoa huduma zilizo bora zaidi.

Anasema, pia wanatoa huduma za kusafisha figo kwa kipindi cha miaka mitatu sasa, ambayo imesaidia kuokoa maisha ya watu wengi waliotakuwa kwenda nje ya nchi kufuata huduma hiyo.

**USHIRIKIANO UKOJE?**

Dk. Masenga anasema, JCMC inashirikiana na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), inayochangia kuiongezea mapato hospitali.

Anasema NHIF, imekuwa ikitoa mikopo kwa hospitali hiyo na tayari waliwapa Sh. bilioni 1.7 kwa ajili ya ujenzi wa chumba cha dharura.

Dk. Masenga, anaongeza kuwa mfuko huo umewaongezea Sh. milioni 600 kwa ajili ya ujenzi wa mtambo wa kutengeneza gesi ya matumizi ya hospitali hiyo.

Anasema, huduma hiyo itakuwa na uwezo wa kutengeneza mitungi 400 wakati hospitali hiyo hutumia mitungi zaidi ya 60 kila siku hivyo itasaidia kuwauzia hospitali za jirani ili kujipatia fedha za kuendesha hospitali.

"Badala ya kupokea wagonjwa wengi kutoka nje wanaohitaji hewa ya Oksieni, tumeona ni vyema tukawauzia kwa bei nafuu ili nao wawatibu wagonjwa wao kuliko wawalete wagonjwa kwetu wajaze nafasi," anasema.

Anaeleza, kwamba wanashirikiana na Bohari Kuu ya Dawa (MSD), kupata huduma za dawa na mahitaji wanayopata ni asilimia kubwa, tofauti na awali walikuwa wakipata asilimia 20.

Anasema MSD inaendelea kuboresha utoaji huduma katika hospitali hizo, hivyo anaamini wataongezewa dawa na vifaa tiba zaidi, ili kuokoa fedha wanazotumia kununua dawa kutoka kwa mawakala.

"Tunafanya kazi na MSD kwa karibu na wanafanya kazi nzuri sana, kuna maeneo ambayo wameshasambaza dawa kwa asilimia 90, naamini na hapa tutafikia kiwango hicho kwa sababu kazi wanayofanya inaonekana," anasema Dk. Masenga.



## DC atoa siku 10 machinga kutumia vitambulisho

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, ametoa siku 10 kwa machinga kuhakikisha wote wanakuwa na vitambulisho vilivyotolewa na Rais John Magufuli.

Itakumbukwa kuwa serikali ilitoa vitambulisho kwa wakuu wa mikoa kwa lengo la kuhakikisha vinagawiwa kwa machinga ili wasibughudhiwe na watendaji.

Mfune alitoa kauli hiyo jana, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kilichokuwa na lengo la kupitisha muhtasari wa mpango na bajeti ya miaka mitatu 2019/2020-2021/2012 na makisio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2019/2020.

"Kufikia tarehe 10 ya mwezi Februari kila machinga awe na kitambulisho, nia ni njema kwamba tunahitaji kuwatambua, lakini kuongeza mapato kwa serikali yetu wale ambao wana namba ya utambulisho yaani Tin, lakini sio za kibiashara pia wanatakiwa kupewa vitambulisho waliochukua namba hizo kwa ajili ya biashara hawapaswi kupewa, jambo hili ni la haraka na dharura watendaji wote wa kata makatibu tarafa mnayo kazi ya kuwahamasisha machinga kuvichukua alisema Mfune.

Awali akisoma taarifa ya makisio ya bajeti, Ofisa Mipango wa Wilaya hiyo, Emmanuel Kishimbo, alisema katika bajeti ya mwaka 2019/20120 itajikita katika vipaumbele kama vile uchaguzi wa serikali za mitaa 2019, ujenzi au ukamilishaji wa zahanati katika vijiji, kuboresha miundombinu ya sekta ya kilimo, mifugo, afya na elimu na kuboresha lishe kwa watoto.

Kishimbo alifafanua kuwa katika maandiko ya miradi ya kutolea huduma halmashauri iliwasilisha maandiko yenye jumla ya Shilingi bilioni 1.5 kutoka kwenye Idara ya Afya, elimu msingi na sekondari.

" Idara ya Afya tumetenga kiasi cha Shilingi milioni 525 na fedha hizo zitatumika kukamilisha ujenzi wa zahanati kumi za Manienge, Ikanutwa, Iheha, Iwalanje, Azimio, Mswisi, Malamba, Iugelele, Ukwama na Iyambogo na ukamilishaji wa ujenzi wa kituo cha afya cha Mahongole," alisema Kishimbo.

Hata hivyo baadhi ya madiwani akiwamo wa Kata ya Luhanga, Dira Funika, wameomba serikali kuhakikisha inamalizia ujenzi wa maboma yote ambayo yalijengwa kwa nguvu za wananchi, ili kupunguza changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa.

# Mfanyabiashara adakwa kwa kuzalisha mbegu feki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Udhibiti wa Mbegu nchini (Tosci), imemkamata na kumfungia kuendelea na biashara mfanyabiashara, Fortunatus Lutanikwa wa Jiji la Mbeya kwa kosa la kuzalisha mbegu feki na kughushi nembo ya taasisi hiyo pamoja na kampuni zingine zinazozalisha bidhaa hiyo.

Aidha, taasisi hiyo inakusudia kumfikisha mahakamani mfanyabiashara huyo kwa madai kuwa kitendo alichokifanya ni kosa kwa mujibu wa sheria na taratibu za uzalishaji wa mbegu.

Mfanyabiashara huyo anayefanya shughuli zake katika eneo la Uyole jijini Mbeya, alikamatwa jana wakati maofisa wa Tosci kutoka makao makuu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi walipofanya ukaguzi wa kushtukiza katika maduka mbalimbali ya mbegu jijini Mbeya.

Mkaguzi wa Tosc kutoka makao makuu, Emmanuel Mwakatobe, alisema mfanyabiashara huyo alikuwa anauza mbegu ambazo baadhi hazina nembo ya taasisi hiyo na zingine zikiwa hazina vielelezo vinavyoonyesha mahali alikozinunua mbegu hizo.

"Tunaendelea na ukaguzi huu katika nchi nzima na niwahakikishie Watanzania hatutaweza kuwavumilia wafanyabiashara wa aina hii, kwa sababu wanachangia kushuka kwa sekta ya kilimo na wanachafua kampuni zingine," alisema Mwakatobe.

Vilevile Mwakatobe alisema sio mara ya kwanza kwa mfanyabiashara huyo kutuhumiwa kwa biashara hizo kwa madai kuwa awali wananchi walikuwa wanamlalamikia.

Hata hivyo Lutanikwa alipohojiwa kuhusu mbegu hizo alishindwa kutoa majibu yanayoeleweka, hivyo maofisa hao wa Tosci wakaamua kumfungia duka lake na Jeshi la Polisi likampeleka selo.

Alisema baadhi ya mbegu hizo zilikuwa ni mabaki ya zile alizokuwa anauza mwaka jana, lakini baadaye baada ya kubanwa na maswali kutoka kwa wataalamu hao akaeleza kuwa anazinunua kutoka kwa mawakala wa kampuni zinazozalisha mbegu.

Alisema mbegu hizo alikuwa amezihifadhi kama pambo dukani kwa madai kuwa msimu wa kupanda mazao umeshaisha hasa kwa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo kwa kiasi kikubwa inategemea kilimo cha mvua. "Mzigo waliochukua unagharimu Shilingi milioni 20, lakini sikukusudia kuziuza kwa wakulima, nilizihifadhi baada ya msimu wa kilimo kuisha kwa sababu nilikuwa sina kwa kuzipeleka," alisema Lutanikwa.

Baadhi ya maofisa kutoka kwa maofisa wa kampuni zinazozalisha mbegu walikana kumuuzia mbegu mfanyabiashara huyo, huku baadhi ya wakidai kuwa nembo za mbegu alizokuwa anatumia mfanyabiashara huyo ni mpya na hawajaanza kuzitumia.




Mkuu wa Huduma za Kifedha wa Tigo, Hussein Sayed (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya shilingi milioni 20, kwa Vicky Ibrahim baada ya kuibuka mshindi mkubwa wa promosheni ya mwisho wa mwaka 2018, inayojulikana kama " Chifu wa Mawakala" kwa Kanda ya Pwani, katika hafla iliyofanyika, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkuu wa Bidhaa Huduma za Kifedha, James Sumari. **PICHA: JOHN BADI**

# Halmashauri yajitafakari biashara ya kakao

**Na Nebart Msokwa, KYELA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, imesema inahitaji zaidi ya miezi sita kutathmini mfumo wa ushirika katika kuuza zao la kakao kwa madai kuwa mfumo huo ni mpya na unakabiliwa na changamoto nyingi katika wilaya hiyo.

Hayo yalisemwa juzi na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Hunter Mwakifuna, wakati alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani kilichokuwa kimelenga kujadili mapendekezo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020.

Mwakifuna alisema mfumo wa ushirika unalenga kuwasaidia wakulima kuuza mazao yao kwa faida pamoja na kuepusha utoroshaji wa mazao unaosababisha serikali kukosa mapato yatokanayo na ushuru.

Alisema katika wilaya hiyo mazao yanayotakiwa kuuzwa kupitia vyama vya ushirika ni kakao na korosho lakini akaeleza kuwa mfumo huo wa ushirika umeanza hivi karibuni katika wilaya hiyo na hivyo ni vigumu kuutathmini kama una faida ama la!

Alizitaja baadhi ya changamoto zinazoukabili mfumo huo kwa Wilaya ya Kyela kuwa ni pamoja na baadhi ya wakulima kuogopa kupeleka mazao yao kwenye vyama vya msingi vya ushirika kutokana na historia mbaya ya mfumo huo.

"Mfumo wa kuuza kakao kwa kutumia vyama vya ushirika katika wilaya yetu ulianza mwezi Oktoba na umekuwa ukikabiliwa na changamoto nyingi, hivyo ni vigumu kufanya tathmini kwa sasa kama una faida ama la japo kuwa malengo yake ni mazuri sana," alisema Mwakifuna na kuongeza.

"Miaka ya 1991 mpaka 1995 watu waliingia hasara sana maana kulikuwa na ubadhirifu mkubwa sana wa mali za ushirika, sasa kutokana na historia hiyo baadhi ya wakulima mpaka sasa wamekuwa wakisuasua kupeleka mazao yao kwenye vyama hivyo wakihofia historia kujirudia," aliongeza.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kyela, Lucy Mganga, alisema katika makadirio ya bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 ni kutumia Shilingi bilioni nne.


Alisema bajeti hiyo inalenga katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo ya maji, zahanati, vituo vya afya na ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari na msingi ambazo zina changamoto hiyo.

Alisema wanakusudia hata fedha zinazotokana na makusanyo ya ndani ikiwamo ukusanyaji wa ushuru wa mazao hasa kakao, korosho na mpunga ambayo ndiyo mazao yanayoonekana zaidi kwa wilaya hiyo ambayo ipo upande wa kusini mwa Mkoa wa Mbeya.

"Bajeti yetu inalenga katika utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi hasa kwenye miradi itakayowanufaisha wananchi wa kawaida na hilo ndio lengo la serikali yetu," alisema Mganga.

Nao baadhi ya madiwani walisema makadirio ya bajeti ya halmashauri hiyo itawasaidia wananchi wa kata zao hasa katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mmoja wa madiwani hao, Godfrey Kingamkono, ambaye ni Diwani wa Kata ya Ikimba, alisema bajeti iliyopita mpaka sasa bado robo mbili kukamilika, lakini imeshatekelezwa kwa asilimia 46 na kwamba ana imani mpaka kufikia mwisho wa mwaka itakuwa imetekelezwa kwa asilimia 100.





# Halotel yarejesha faida kwa jamii

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha inatekeleza agizo la Serikali ya kurejesha faida kwa jamii, Kampuni ya Simu ya Halotel imemkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kiasi cha zaidi ya Sh. milioni 20 kwa ajili ya kuwawezesha vijana wa mkoa huo kujiajiri kupitia sekta ya ujenzi.

Mbali na fedha hizo, Halotel pia imekabidhi vifaa mbalimbali vya hospitali kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa vikiwemo vitanda, neti, mashuka na aproni vyenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni sita katika Hospitali ya Makole mkoani humo.

Akikabidhi misaada hiyo kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dk. Binilithi Mahenge, mbele ya Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, Mkurugenzi Mtendaji wa Halotel Tanzania, Nguyen Van Son, alisema pamoja na mambo mengine, misaada hiyo imelenga kuunga mkono juhudi mbalimbali za maendeleo zinazofanywa na Serikali ya awamu ya tano.

Son alisema katika kuhakikisha inaunga mkono jitihada hizo za Serikali, Kampuni hiyo ya simu ya Halotel imekuwa mstari wa mbele kurudisha faida kwa kile inachokipata kwa kuisaidia jamii mambo mbalimbali kwa lengo la kukabiliana na changamoto zinazowazunguka Alisema hatua hiyo imelenga kutoa shukrani kwa wananchi kwa hatua yao ya kuwaunga mkono kwa kutumia huduma za kampuni hiyo iliyosambaa nchi nzima ikitoa huduma mbalimbali na hasa katika maeneo na hasa vijijini. "Tunaamini misaada hii itakwenda kuwa chachu ya maendeleo katika sekta ya afya na ujenzi, hususani kwa kuwawezesha vijana kujiajri katika sekta za ujenzi unaoendana na kukua kwa mji wa Dodoma," alisema Son.

Aidha, aliishukuru Serikali kwa kuweka mazingira wezeshi na rafiki yaliyowavutia kuweza kwenye Sekta ya Mawasiliano nchini na kuongeza kuwa dhamira yao ni kuendeleza ushirikiano na kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano zinakuwa za viwango, ubora na gharama nafuu kwa mtumiaji.

Aliipongeza Halotel kwa hatua hiyo na kuzitaka kampuni zingine kuiga mfano huo ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Serikali linayozitaka kampuni za simu kurejesha sehamu ya faida kwa jamii.




Mkurugenzi wa kampuni ya Halotel, Nguyen Van Son (wa pili kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya Shilingi milioni 20.6 kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, kwa ajili ya kuanzisha kiwanda cha kufyatua matofali cha kikundi cha vijana wa mkoa huo, katika hafla iliyofanyika jijini humo juzi. Wa pili kulia ni Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaahidi nidhamu matumizi fedha za wananchi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imeahidi kumia vizuri fedha zitakazopatikana ili kuhakikisha zinaleta maendeleo kwa Watanzania wote pamoja na kuleta maendeleo ya umma.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Josephat Kandege, jijini Dodoma, wakati akifunga mafunzo elekezi kuhusu utekelezaji wa programu ya lipa kulingana na matokeo katika sekta ya elimu yaliyowashirikisha wakurugenzi wa halmashauri wa mikoa ya Dodoma na Morogoro, maofisa elimu wa shule za sekondari na msingi na wadhibiti ubora wa elimu.

Alisema hakutakuwa na utani kwenye fedha za serikali ili ziwe na tija kwa Watanzania wote, kwa sababu serikali hii ni ya viwanda na inahitaji kuona maendeleo kwa wananchi na si ufisadi.

Alisema pia haiingii akilini kuona kuwa halmashauri inapata hati za mashaka kutokana na kufanya malipo lakini, viambatanisho vya malipo hayo havionekani, kitu ambacho ni uzembe na makusudi.

"Ni wajibu wenu kuzingatia sheria, taratibu na miongozo ya serikali ili kuepuka hoja za ukaguzi," alisema.

Aidha, aliwacharukia baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo ambao ni wakurugenzi kusaini posho na kuondoka wakati mafunzo hayo yakiendelea.

Alisema wakati mwingine wakirudia kufanya hivyo atachukua hatua dhidi yao.

Aliwataka kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi hasa ujenzi wa miundombinu ya shule, ili ikamilike kwa wakati sambamba na ujenzi wa majengo mbalimbali uzingatie ramani zitakazotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Alisema programu ya lipa kulingana na matokeo katika sekta ya elimu ilizinduliwa Septemba 2014 chini ya mpango wa matokeo makubwa sasa kwa lengo la kuinua ubora wa elimu nchini.

Alisema, mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa programu hiyo 2014/2015, mamlaka za serikali za mitaa zilipokea Sh. bilioni 15.53 na mwaka wa pili jumla ya Sh. bilioni 22.36 na mwaka wa tatu 2016/2017 jumla ya Sh. bilioni 40.09.

Alisema katika awamu ya nne kiasi cha Sh. bilioni 40 kinatarajiwa kupatikana.

Mkurugenzi wa Idara ya Utaribu wa Elimu Tamisemi, Julius Nestory, alisema walengwa wa kikao hicho ni wakurugenzi, maofisa elimu wa sekondari na misingi na wadhibiti ubora wa shule.

Alisema kikao kililenga zaidi kutoa mafunzo na kufanya tathmini, ambapo serikali ilipeleka zaidi ya Sh. bilioni 40.8 katika halmashauri na mkaguzi na mdhibiti alipokagua wakapata hoja nyingi za ukaguzi wakaona ni vyema maofisa hao wakapata miongozo ili waelewe.

"Kuna fedha zililipwa kama masurufu lakini, viambatanisho havionekani zilileta tabu kujibu hoja za Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali (CAG).

Aidha, alisema upungufu mwingine ulioonekana ni ukosefu wa risiti kwa wale waliolipwa, orodha ya waliolipwa ilikuwa na shida na kuna fedha zilizokwenda kwenye miradi ya maendeleo lakini ilichelewa kukamilika na mingine ilikuwa chini ya kiwango.

# Ufisadi wapiga kambi kwenye ushirika

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

VYAMA vya ushirika nchini vinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa masoko ya uhakika na endelevu pamoja na ubadhirifu unaofanywa na baadhi ya viongozi wake.

Hayo yalielezwa jana na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Tito Haule, wakati wa mkutano wa makamishna wa tume hiyo, viongozi wa vyama vikuu vya ushirika pamoja na wadau wa ushirika uliofanyika jijini hapa.

Haule alisema ushirika unakabiliwa na changamoto ya ubadhirifu unaofanywa na baadhi ya viongozi wa vyama hivyo na ukosefu wa masoko ya uhakika na endelevu kwa mazao na bidhaa za wanaushirika.

"Kumekuwapo na changamoto mbalimbali zinazoikabili tume katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwamo ukosefu wa masoko ya uhakika na endelevu kwa mazao na bidhaa za ushirika," alisema Haule.

Alisema tume katika kukabiliana na changamoto hizo inashirikiana na taasisi zote zinazojihusisha na masuala ya uwekezaji ili kupata masoko.

Katika kukabiliana na changamoto ya baadhi ya viongozi wabadhirifu wa vyama vya ushirika alisema, hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na viongozi hao kuondolewa katika nafasi zao na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Alisema matokeo ya uchunguzi yalibaini upungufu mbalimbali ikiwamo upotevu wa fedha na mali za vyama, matumizi mabaya ya madaraka kwa viongozi na watendaji wa vyama hivyo vya ushirika.

Mambo mengine waliyoyabaini ni pamoja na ukiukwaji wa sheria ya vyama vya ushirika na miongozo pamoja na ukiukwaji wa taratibu za uendeshaji wa vyama vya ushirika.

Mrajisi huyo alisema baada ya kubaini mapungufu yaliyojitokeza katika uchunguzi huo hatua mbalimbali zilichukuliwa kwa wahusika ikiwemo kuondolewa madarakani kwa viongozi wa bodi za vyama vya ushirika.


Alitataja hatua zingine zilizochukuliwa ni wahusika kufikishwa kwenye vyombo vya dola kama polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kwa uchunguzi zaidi kwa ajili ya kufikishwa mahakamani.

Alisema hatua zingine zilizochukuliwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani watuhumiwa waliobainika kufanya ubadhirifu wa mali za vyama hivyo vya ushirika na kuwaandikia hati za madai wadaiwa wote waliobainika kusababisha hasara katika chama cha ushirika.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dk.Titus Kamani iliagiza mali zote zilizokuwa za ushirika popote nchini zilizochukuliwa kiujanjaujа zirudishwe haraka .

Dk. Kamani alisema kumbukumbu za mali za kila chama cha ushirika zipo na watakaothubutu kutaka kuzihujumu watakutana na mkono wa sheria .

Alisema serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Dk John Magufuli imedhamiria kuendeleza na kuimarisha ushirika hapa nchini kwa lengo la kumkomboa mwananchi kiuchumi.





# Wananchi walilia udogo kituo cha afya kukosa huduma

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANANCHI wa Kijiji cha Umbuji Wilaya ya Kati Unguja, wamesema kuwa udogo wa jengo la kituo chao cha afya unasababisha kukosa huduma za matibabu.

Wakizingumza na waandishi wa habari kijijini hapo, walisema kituo hicho cha afya hakikidhi mahitaji ya kuwahudumia wananchi wa Jimbo la Umbuji katika utoaji wa huduma.

Khatib Abdalla mkaazi wa kijiji hicho, alisema kituo hicho kilijengwa kwa ajili ya huduma za afya ya mama na mtoto, lakini kutokana na ukosefu wa kituo cha afya imelazimika kitoe huduma kwa watu wote.

"Hiki kituo ni kidogo sana hao kinamama wenyewe na watoto hakiwatoshi, hivyo tunaiomba serikali itujengee jengo jengine kwa ajili ya kituo cha afya kwa watu wote," alisema.

Khatib alisema mkusanyiko wa wajawazito na watu wengine ambao hupatiwa huduma za afya kituoni hapo ni changamoto pia kwa kinamama kwa kuwa wanahitaji eneo maalum ili kuweza kufichiwa siri zao.

"Tunaushukuru mradi wa uwajibikaji wa (PAZA) ambao unatekelezwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Maendeleo (WAHAMAZA) kushirikiana na Taasisi ya Msitu wa Ngezi (NGERENACO), tumekuwa tukipaza sauti zetu kwa kueleza changamoto mbalimbali ambazo baadhi zimefanyiwa kazi tunaomba na hili la kituo cha afya lifanyiwe kazi," alisema.

Alisema kuwa maradhi yanayowasumbua husikika na watu wengine, hivyo ni vyema kutengewa eneo la faragha ili kuweza kueleza matatizo yao bila ya kuona aibu.

"Wakati mwingine mama mjamzito anavua nguo ili kumuonyesha daktari ugonjwa unaomsumbua na wanaume wapo hapo hapo, hivyo haileti picha nzuri hasa huku vijijini,"alisema.

Naye Rashma Shaaban mkaazi wa Pagali ambaye alifika kituoni hapo kwa ajili ya kupata huduma alisema, kituo hicho kwa sasa ni kidogo na hakikidhi mahitaji ya kinamama na watoto wanaofika hapo kufuata huduma.

"Hiki kituo ni kidogo, lakini pia hakina madaktari wa kutosha, unakuja hapa unachukuwa muda mrefu kwa ajili ya kupata huduma za uchunguzi wa afya ya mtoto," alisema. Kwa upande wake mkuu wa kituo hicho ambaye hakutaka kutajwa jina lake alikiri udogo wa kituo hicho na upungufu mkubwa wa madaktari na wahudumu katika hospitali hiyo kulingana na mahitaji ya wananchi.

"Tupo wafanyakazi watano tu katika kituo hiki ambacho kinatoa huduma za afya kwa wananchi takribani 7,000 kwa mwezi," alisema.



Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi Zanzibar, Maryam Juma Sadalla, akichangia kuhusu maendeleo ya miradi ya wizara hiyo, wakati wa mkutano na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein (hayupo pichani), uliofanyika katika ukumbi wa Ikulu, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

## Waziri aagiza vyuo vya ufundi kusajiliwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka wamiliki wa vyuo na wadau wa elimu kuhakikisha wanafanya usajili wa taasisi zao kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Baraza la Elimu ya Sayansi na Ufundi (NACTE).

Akifungua mkutano wa baraza hilo na wakuu wa vyuo mbalimbali wa taasisi za sayansi na ufundi Mjini Unguja, alisema usajili utasaidia kuondoa tatizo la vyuo hewa na kupunguza wimbi la wahitimu wasio na sifa.

Alisema pia kufanya udahili pia kutawasaidia wadau hao kuondosha tatizo la wahitimu kutokua na namba za usajili ambazo zitawaruhusu wanafunzi kuendelea mbele katika masomo yao.

Alisema kuvisaili vyuo visivyo na sifa ya kutoa elimu ya juu husababisha usumbufu mkubwa hasa kwa wanafunzi kwa kuwapotezea muda na kushindwa kupata ajira baada ya kumaliza masomo.

# Wanawake waonywa kudai talaka bila utaratibu

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WANAWAKE wametakiwa kuacha tabia ya kudai talaka wakati inapotokea migogoro katika ndoa zao, kwa kuwa kufanya hivyo ni kuongeza matatizo na kusababisha kuwapo wimbi la watoto wa mitaani waliokosa matunzo.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Uwezeshaji, Wanawake, Watoto na Wazee, Mauldlic Castico, wakati wa uzinduzi wa jengo la Mahakama ya Kadhi kwa ajili ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa Mwanakwerekwe mjini Unguja. Alisema njia pekee ya kuleta ufumbuzi wa migogoro ya ndoa ni usuluhishi wa pande zote mbili kwa kuwatumia wazee na viongozi wa dini na siyo kudai talaka.

Alieleza kuwa migogoro ya ndoa kwa kiasi kikubwa imesababishwa na kusambaratika kwa familia na hivyo kuwapo kwa idadi kubwa ya watoto kukosa matunzo pamoja na haki ya msingi ya elimu.

"Njia pekee sahihi za kumaliza migogoro ya ndoa majumbani ni kufanya suluhu kwa kutumia wazee na viongozi wa dini," alisema.

Naye Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, alisema kazi kubwa inayofanywa na mahakama mbalimbali ikiwamo ya Kadhi ni kuzifanyia haraka ufumbuzi wa kesi za ndoa.

Alisema katika kipindi cha mwaka jana jumla ya kesi za migogoro ya ndoa 767 ziliwasilishwa katika Mahakama za Kadhi Unguja na Pemba na kusikilizwa na kutolewa maamuzi.

"Kesi za migogoro ya ndoa ikiwamo zinazohusu talaka tumezipa kipaumbele cha kwanza kwa ajili ya kusikilizwa na kupatiwa ufumbuzi katika Mahakama za Kadhi ziliopo Unguja na Pemba," alisema.

Kwa upande wake Kadhi wa dhamana ya mahakama ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa, Kassim Ali, alisema jamii inahitaji kupewa elimu zaidi kuhusu ndoa kabla ya kuingia katika makubaliano hayo.

"Kesi za migogoro ya ndoa na kudai talaka zimekuwa zikiongezeka katika Mahakama ya Kadhi, ambapo moja ya tatizo kubwa ni kukosekana kwa maadili na misingi ya ndoa katika jamii," alisema.

Mahakama za Kadhi zilizoko Zanzibar hutumiwa na jamii ya Waislamu kwa ajili ya kuzipatia ufumbuzi kesi za talaka, matunzo ya watoto pamoja na urithi.

HABARI KIMATAIFA

## May, Bunge waomba mkataba mpya

**LONDON,** Uingereza

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Theresa May, ametaka kufunguliwa upya mazungumzo na Umoja wa Ulaya (EU).

May aliwaambia wabunge wa Uingereza kuwa kuna haja ya kuwapo kwa mazungumzo mapya na EU.

Hatua hiyo imekuja wakati juzi wabunge wa Uingereza walipigia kura marekebisho kadhaa ya kuandaa mazungumzo hayo.

Licha ya onyo ambalo limekuwa likitolewa na nchi 27 mwanachama wa EU, kuwa makubaliano yaliyokataliwa Januari 15 hayawezi kujadiliwa tena, Bunge la Uingereza bado linaomba mkataba mpya.

Marekebisho hayo yalipigiwa kura na idadi kubwa ya wabunge, katika kura hizo wabunge waliopiga kura ya ndiyo walipata ushindi wa kura 317 dhidi ya 301 waliosema hapana.

May amekuwa akikabiliwa na shinikizo la kufanyika kwa kura mpya ya maoni kuhusu Uingereza kujitoa katika Umoja wa Ulaya.

Hata hivyo, May ameendelea kupinga hoja hiyo akisema kuwa itakuwa ni kwenda kinyume na matakwa ya wananchi ambao wengi waliomba nchi yao kujitoa katika umoja huo. **RFI**

## Tanzania, Rwanda vinara kupambana na ufisadi

**BERLIN,** Ujerumani

SHIRIKA la Kimataifa la Transparency International (TI), limetoa ripoti inayoonyesha hali ya ufisadi duniani mwaka 2018, ambapo imeonyesha Tanzania na Rwanda ndiyo mataifa pekee yaliyofanya vizuri katika vita dhidi ya rushwa.

Rwanda ilitajwa kufanya vizuri zaidi kwa kuwa na pointi 56 ikiwa katika nafasi ya 48, wakati Tanzania ikiwa katika nafasi ya 99 kwa kupata pointi 36.

Ripoti hiyo pia imebaini kuwa Kenya ilishuka kwa pointi moja kutoka mwaka 2017, ambapo ilikuwa na pointi 28, huku mwaka jana ikiwa na pointi 27 na kushika nafasi ya 144 kati ya nchi 180.

Uganda ilipata pointi 26 na kuchukua nafasi ya 149, Burundi iko katika nafasi ya 170, huku Sudan ikiwa katika nafasi ya 172 ikiwa na pointi 16.

Transparency International hutumia vigezo ambapo sifuri ni alama ya nchi inayofanya vizuri zaidi, huku 100 ikiwa ndiyo nchi iliyozorota zaidi katika nyanja hiyo.

Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Ferreira Rubia, alisema jinsi demokrasia ilivyokita mizizi kwa baadhi ya nchi, ndivyo uwezekano wa nchi hiyo kufanya vyema katika orodha hiyo ya nchi fisadi zaidi duniani. **VOA**

# Upinzani Zimbabwe: Kheri Mugabe kuliko Mnangagwa

**HARARE,** Zimbabwe

CHAMA kikuu cha upinzani nchini Zimbabwe MDC, kimelaani vikali ukandamizwaji uliotokea wakati wa kuzimwa kwa maandamano kupinga kupanda kwa bei ya mafuta nchini humo.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka mashirika ya mawakili kwa ajili ya haki za binadamu, zaidi ya watu 800 walikamatwa wakiwamo wafuasi wa upinzani na wale wa mashirika ya kiraia.

Katika mkutano na waandishi wa habari juzi chama kikuu cha upinzani cha Movement for Democratic Change (MDC), kimelaani ukandamizaji unaoendelea kutokea nchini Zimbabwe kwa siku za hivi karibuni.

Umesema ukandamizaji huo umesababisha vifo baada ya kuwapo kwa maandamano dhidi ya kupanda kwa bei ya mafuta wiki mbili zilizopita.

Watu zaidi ya 800 walikamatwa kwa mujibu wa Chama cha Wanasheria wa Haki za Binadamu kinachojumuisha wanaharakati, mashirika ya kiraia na wanasiasa wa upinzani.

**Ni uongo mtupu kusema kwamba MDC iliandaa maandamano hayo. Na bado tunaendelea kulengwa. Zaidi ya wabunge wetu arobaini wamefanyiwa vitendo vya udhalilishaji, wengine wamefanyiwa vitisho. Na sita wamekamatwa.**

Wameeleza kuwa ukandamizaji huo ni tofauti na hauhusiani na mgomo wa wiki mbili zilizopita.

Vikosi vya usalama nchini Zimbabwe vinashutumiwa kuendesha operesheni zao usiku katika maeneo yenye makazi, huku wakiwakamata na kuwapiga raia wasio kuwa na hatia na kuwafanyia vitendo vya dhuluma wanawake.

Chama kikuu cha upinzani cha MDC kimeshtumu mbinu zilizotumiwa katika operesheni hiyo ambazo wamedai ni za kikatili zaidi kuliko wakati wa Rais wa zamani wa nchi hiyo, Robert Mugabe.

Kwa mujibu wa kiongozi wa chama cha MDC, Nelson Chamisa, alisema serikali inatafuta kuangamiza upinzani wa kisiasa.

"Ni muungano wa wafanyakazi, ZCTU, ambao uliitisha maandamano hayo. Upinzani hauhusiki. Ni uongo mtupu kusema kwamba MDC iliandaa maandamano hayo. Na bado tunaendelea kulengwa. Zaidi ya wabunge wetu arobaini wamefanyiwa vitendo vya udhalilishaji, wengine wamefanyiwa vitisho. Na sita wamekamatwa.

"Wamekamatwa kwa sababu ya kuwa ni upande wa upinzani, kuwa katika upande wa upinzani leo ni uhalifu," alisema Chamisa.

Chamisa aliishutumu jumuiya ya kimataifa kukaa kimya, hasa jumuiya ya kikanda, SADC.

Kwa upande wa serikali ya Zimbabwe, unaushtumu upinzani kuandaa maandamano hayo na kuchochea vurugu. **RFI**



Rais wa Venezuela, Nicolas Maduro, ambaye kwa sasa amekataa kuitisha uchaguzi nchini humo. **PICHA: REUTERS**

# Maduro akataa kuitisha uchaguzi

**CARACAS,** Venezuela

KIONGOZI wa Venezuela, Nicolas Maduro, amesema yuko tayari kwa mazungumzo na upinzani na kuitisha uchaguzi wa mapema wa bunge.

Mapambano ya kuwania madaraka ya kuidhibiti Venezuela yamepamba moto baada ya serikali jana, kushinikiza uchunguzi ambao huenda ukasababisha kukamatwa kiongozi wa upinzani aliyejitangaza kuwa rais wa mpito nchini humo Juan Guaido.

Mahakama ya juu kabisa ya Venezuela imepitisha vikwazo dhidi ya Guaido kusafiri nje ya nchi hiyo na akaunti zake kuzuiliwa.

Hatua hii inaonekana kulenga kulipiza kisasi kutokana na vikwazo ilivyowekewa Venezuela na Marekani katika biashara yake ya mafuta.

Vikwazo hivyo vinatarajiwa kutikisa uchumi wa nchi hiyo, mwanachama wa shirika la nchi zenye kuzalishwa kiwango kikubwa cha mafuta duniani OPEC, uchumi ambao tayari umeshaporomoka.

Guaido anatambuliwa kama rais na Marekani pamoja na nchi nyingi za Magharibi, huku akionekana kuupa changamoto kubwa utawala wa miaka sita wa Rais Nicolas Maduro.

Rais Donald Trump wa Marekani alisema serikali yake pia inamtambua mjumbe wa kidiplomasia kutoka upande wa upinzani wa Guaido katika ubalozi wa Venezuela nchini Marekani, Carlos Alfredo Vecchio.

Vecchio baada ya kukutana na Makamu wa Rais wa Marekani, Mike Pence, juzi aliutaka ulimwengu kusaidia kuikomboa Venezuela.

"Tuliweka wazi kwamba hivi vita sio kuhusu itikadi. Hivi ni vita kati ya demokrasia na udikteta. Hivi ni vita kati ya udikteta ambao kwa hali zote unaendeshwa na utawala wa Cuba dhidi ya ulimwengu ulio huru. Hatuwezi kushinda vita hivi peke yetu."

"Tuna majukumu makubwa kama wana Venezuela, lakini tunawaomba nyinyi ulimwengu ulio huru kutukomboa kwa namna fulani, Venezuela ambayo iko kwenye ukoloni wa utawala wa Cuba. Kwa hivyo tutaendelea kupambana mpaka tutakapoipata tena demokrasia yetu na ndio sababu tutaendelea kuomba msaada wa kimataifa," alisema Pence.

Guaido ameitisha maandamano zaidi jana na anatarajia kufanya mengine mwishoni mwa wiki, ili kuendelea kumshinikiza Rais Maduro kupitia sauti za wananchi mitaani.

Maduro ambaye anamtuhumu Guaido kuendesha jitihada zinazosimamiwa na Marekani za kutaka kumpindua madarakani bado anaungwa mkono na uongozi wa juu jeshini na hakuna dalili kwamba atasalimu amri labda mambo yabadilike. **DW**

# Gesi asilia sasa yatua nyumbani, viwandani

**Na Salome Kitomari**

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, kwa mwaka wa fedha 2015/16, ilibainisha kuwa bomba la gesi asilia linatumika kwa asilimia sita, huku Shirika la Umeme (Tanesco) likiwa ndiyo mtumiaji pekee wa bomba hilo.

Katika ripoti yake hiyo, CAG Assad, alisema suala hilo ni kinyume cha matarajio ya wengi kwamba gesi hiyo ingenufaisha wananchi wengi.

Katika kutekeleza mapendekezo ya CAG Assad ambaye alishauri gesi hiyo itumike kwa mambo mengine mbali na ufuaji wa umeme, Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) limeanza kusambaza gesi asilia kwenye nyumba za wananchi katika maeneo ya Mikocheni na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Vilevile, gesi imewekwa kwenye viwanda mbalimbali, ikiwa ni pamoja na viwanda vya Coca-Cola na Bidco, vilivyopo Mikocheni. Awali gesi hiyo ilikuwa inatumika kwenye nyumba za TPDC pekee.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa TPDC, Maliki Munisi, alisema usambazaji umefanikiwa baada ya kazi hiyo kuanza mwaka jana kwa kutoa gesi kupitia bomba dogo kwenye Kituo cha Ubungo kwenda kwenye maeneo husika.

"Gesi asilia inasambazwa kutoka Ubungo kupitia Barabara ya Sam Nujoma hadi Mikocheni, na huko njiani nyumba zilizoko jirani na bomba zinashawishiwa kuunganishiwa huduma hiyo," alisema.

Aliyataja maeneo yatakayopata gesi hiyo kuwa ni UDSM, ambayo kwa sasa wataanza na mgahawani, wakifuatwa na Sinza, Mlalakua, Shekilango, Mwenge na Mikocheni.

"Tayari ujenzi umeanza kwenye nyumba 24 ambazo wanajengewe mfumo na kuungwa kwenye mita, pia mgahawa wa UDSM nao unaungwa, kazi hiyo inafanywa na TPDC yenyewe na mafundi wetu wapo kazini kwa sasa," alisema.

Aliongeza kuwa nyumba 55 za maeneo ya UDSM, nazo zitaunganishwa huduma hiyo baadaye kwa kuwa lengo ni kuhakikisha Watanzania wananufaika na huduma hiyo na kuachana na matumizi ya mkaa.

Kwa mujibu wa Munisi, wanashindwa kusambaza gesi asilia hadi maeneo ya ndani, kwa kuwa hakuna miundombinu mizuri na kwa sasa wanapitisha kwenye barabara zenye miundombinu mizuri na nyumba zilizoko maeneo hayo.

Alisema iwapo watajitokeza wananchi wakaungana kati ya 10 hadi 20 na kuwa tayari kuunganishwa na huduma hiyo, TPDC itafanya hivyo kwa kuwa ndiyo itakuwa rahisi kuliko kuunganisha mtu mmoja au wawili kwenye eneo moja.

"Kila mteja ataungiwa huduma hiyo baada ya kuletewa mita. Tunawahimiza watu waungane, walete maombi nasi tutawaungia huduma hiyo," alisema.

Munisi alisema lengo la serikali ni kusambaza gesi asilia kwenye maeneo yote nchini, ili kuachana na matumizi ya mkaa.

"Mkoa wa Mtwara na Lindi nako tumeanza kutengeneza mifumo, nyumba zinazostahili kulipwa fidia kupisha mradi zimeshafahamika. Changamoto ni upatikanaji wa vifaa ambavyo vingi vinaagizwa nje ya nchi kwa oda maalum ambayo huchukua muda mrefu kukamilika," alisema.



Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya Biashara ya DCB, Zacharia Kapama (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi wakati akitangaza faida iliyopatikana katika benki hiyo kwa mwaka 2018. Wengine kutoka kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano, Rahma Ngassa, Mkurugenzi wa Biashara, James Ngaluko na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani, Deogratius Thadei. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Serengeti yazindua kampeni kuzuia ulevi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL), imezindua kampeni inayolenga kutoa elimu kwa umma juu ya unywaji wa kistaarabu, ikiwa moja ya hatua muhimu zinazochukuliwa na kampuni hiyo kuzuia ajali nyingi zinazosababishwa na madereva wanaoendesha wakiwa wametumia vilevi.

Kampeni hiyo inayobeba ujumbe wa "usitumie kilevi na kuendesha chombo cha moto' ilizinduliwa jana jijini Mwanza na ilianza na kongamano lililojadili unywaji wa kistaarabu ambalo liliwaleta pamoja wadau kama vile Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Mamlaka ya Usafirishaji wa Majini na Nchi Kavu (Sumatra), madereva, abiria na wadau wa sekta ya usafirishaji.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mwanza, Mkaddam Hamis Mkaddam, alisema kwa kulishirikisha Jeshi la Polisi, SBL imeiunga mkono serikali katika kuelimisha umma juu ya unywaji wa kistaarabu na kusisitiza umuhimu wa kutatua tatizo hilo.

Mkaddam alisema baadhi ya watu na hasa madereva hunywa kiasi kikubwa cha pombe bila kujali madhara yanayoweza kusababishwa na kitendo hicho na kuonya kuwa vitendo vya aina hiyo vinaweza kusababisha ajali mbaya.

Alisema pamoja na kusababisha vifo visivyotarajiwa na majeraha, unywaji usiokuwa wa kistaarabu una maadhara makubwa kwenye sekta ya afya kwa kuwa kiasi kikubwa cha fedha kinatumika kwa ajili ya huduma, dawa na vifaa tiba kwa waathirika wa ajali za barabarani, hivyo kuwa mzigo kwa serikali.

"Ajali hizi pia ni mzigo kwa vyombo vyetu vya utekelezaji wa sheria kwa kuwa maofisa wanalazimika kuzishughulikia wakati zinaweza kuzuilika ambazo zinasababishwa na madereva wanaoendesha wakiwa wametumia vilevi," Mkaddam aliongeza.

# Kesi watuhumiwa mauaji mwanaharakati ujangili Feb.13

**Na Hellen Mwango**

KESI ya mauaji ya mwanaharakati dhidi ya ujangili, Wayner Lotter (52), inayomkabili raia wa Burundi, Habonimana Nyandwi na wenzake 16, imepigwa kalenda hadi Februari 13, mwaka huu kutokana na upande wa Jamhuri kudai upelelezi haujakamilika.

Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, iliketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salum Ally, na kuipiga kalenda kesi hiyo.

Awali Wakili wa Serikali, Saada Mohammed, alidai kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba upelelezi wake haujakamilika.

Hata hivyo, wakili wa utetezi, Herman Lupogo, aliiambia mahakama kuwa mara ya mwisho upande wa Jamhuri uldai upelelezi umekamilika, hivyo unasubiri kuwasilisha taarifa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka(DPP).

"Mheshimiwa hakimu, upande wa Jamhuri unatuchanganya, tarehe ya mwisho ulidai upelelezi umekamilika, lakini leo wanasema upelelezi haujakamilika, watueleweshe nini kinaendelea," alidai wakili Lupogo.

Mbali na Nyandwi, washtakiwa wengine ni raia wa Burundi, Nduimana Jonas maarufu Mchungaji (40) mkazi wa Kamenge Burundi; Godfrey Salamba (42), mkazi wa Kinondoni Msisiri A; Inocent Kimaro (23), mkazi wa Temeke Mikoroshini; Chambie Ally (32), mkazi wa Kia/Boma na Ofisa wa NBC, Robert Mwaipyana (31).

Wengine ni Meneja wa Benki ya Backlays, Khalid Mwinyi (33), mkazi wa Mikocheni B; Rahma Almas (37), mkazi wa Mbagala B na Mohammed Maganga (61). Wengine ni, Allan Mafue, Ismail Mohammed, Leornad Makoye, Amino Sham, Ayoub Selemani, Joseph Lukoa, Gaudence Matemu na Abuu Mkingie,

Katika shtaka la kwanza, washtakiwa kwa pamoja wanadaiwa kuwa kati ya Julai Mosi na Agosti 16, 2017 walikula njama ya kufanya mauaji ya Lotter.

Katika shtaka la pili, washtakiwa hao wanadaiwa Agosti 16, 2017 katika makutano ya barabara za Chole na Haile Selasie iliyopo Wilaya ya Kinondoni Dar es Salaam, wanadaiwa kumuua Lotter.

ITV

MALUMBANO YA HOJA: SAA 3:05 USIKU

Fuatilia mada ya leo" Mmomonyoko wa maadili nchini. Je, jamii inatimiza wajibu wake? Watazamaji wetu kipindi hiki kitawajia mubashara kutoka studio na mnakaribishwa kuja studio kushiriki kwa kutuma majina yako mawili kupitia simu namba 0759 322711. Pia Malumbano ya Hoja inapatikana mubashara ikiwa hewani kupitia akaunti zetu za facebook@ITVTanzania na Youtube ITV Tanzania.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## HUDUMA MBALIMBALI

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.

## ELIMU/MAFUNZO

**NAFASI ZA MASOMO:** Tanzania research and Career development institute. Reg pwf/041.Certificate na diploma za kilimo,mifugo, na maendeleo ya jamii. Mawasiliano:0767574701/0758753063. www.tracdi.ac.tz


## NAFASI ZA KAZI

**TUNAAJIRI WASICHANA WA MAUZO (SALES).** SIFA KIDATO CHA NNE. UMRI KUANZIA MIAKA 25 – 38 AWE MTANZANIA. MASLAHI MAZURI. PIGA SIMU NAMBA 0714 634046.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU


### KUPOTEA KWA CHETI



**Tresphory S. Gowele** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index S1711-0097** kilichotolewa na Baraza la Taifa mwaka 2011 katika shule ya Sekondari Mount Livingstone. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **MWJ/RB/1812/2016**

115037102

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**AGGEY KINASHA HERMAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari Yenye namba za usajili **T 963 DDD** aina ya **SUZUKI CARRY** Yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi: **OB/RB/48/2019**

115033702

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CRDB BANK LTD** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili namba T126 AUW aina ya **LANDCRUISER TOYOTA,** yenye chasis namba **JTERBIJ100042853,** engine namba IH20570278.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **MS/RB/451/2019**

115036902

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**THEONESTINA PROSPER BUYOBE** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba ya usajili **MC 948 CBG** aina ya **SANYA.**

Chassis namba **LK1PCKL18H1051403**
Engine namba **162FMJ470515682**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi.

**Taarifa ya Polisi: MW/RB/918/2019**

115037002

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**STANSLAUS HAROON NYONGO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 555 CAM TOYOTA IST.** Chassis namba NCP610035367. Engine namba INZA665919.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: KJN/RB/625/2019.**

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GRACE MUGYABUSO LESILWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya GARI i aina ya PRADO yenye namba za usajili **T 671 CVK.** Chassis namba **VZJ1Z1 - 0002412.** Engine namba **5VZ - 1612280.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: DOM/TR/ RB/185/2019.**

215038801

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**INES KAJIBU MBIMBI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari Yenye namba za usajili **T 725 BCL** aina ya TOYOTA NADIA,chasis no **SXN10022403,** Engine no.**SXN100022403** Yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi: **KJN/RB/625/2019**

115033602

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**JOSEPH WILBERT MHOHA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 204 ACR TVS KING.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: KJN/RB/621/2019.**

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**JOSEPH WILBERT MHOHA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 209 ACR TVS KING.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: KJN/RB/621/2019.**

### LOSS OF REGISTRATION CARD.

**PROFESSOR JAY FOUNDATION FOR TANZANIA COMMUNITY Registered under Non-Governmental Organisation Act, 2002** do here by announce the loss of Certificate of Registration with **Registration No. 00NG0/00003234.** Whoever finds it, kindly report to the nearest police station. **REF NO: DOM/RB/13822/2018.**

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**MARTHA JOSEPH KIMATI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari Yenye namba za usajili **T214 AHN,** aina ya **TOYOTA RAV 4** Chassis namba: **SXA117049241.** Engine namba **3S2230979** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi: **KJN/RB/630**

115032902

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Zuwena Twaha Hemedi** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili namba **T 622 CMN** aina ya TOYOTA PRADO ,yenye chasis namba **11ZJ950048204**, engine namba **BZJ95034089.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KJN/RB/344/2019**

115035502

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Fair Deal Auto (Pvt) Limited** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba y ausajili **MC 703 CAE** aina ya **BAJAJ BOXER,** yenye engine namba **PFZWJC19039**, chasis namba **MD2A21BYOJWC89433.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KJN/RB/344/2019**

115035702

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**George E. Mapunda** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye usajili namba **T345 BPL** aina ya TOYO. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **MAG/RB/10163/18**

115035802

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**RASHID AHMED AL-HADHRAMI** Anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **T.541 CTM** aina ya HONDA KAWASAKI rangi nyekundu,Chasis namba **JKAEXVA18HA008014,** Engine namba **1KAFE7326.**

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo kilichokaribu nae.

Taarifa ya polisi **MB/RB/9J/2019**


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# INTER: HATUJAPATA OFA NZURI KWA PERISIC




**LONDON,** England

MKURUGENZI wa Inter Milan, Piero Ausilio, amesema hakuna ofa yoyote nzuri iliyotolewa kwa ajili ya winga wao, Ivan Perisic.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia, Perisic amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua kwa miamba wa Ligi Kuu ya England, Arsenal baada ya kuwasilisha maombi ya kutaka kuondoka hapo Inter.

Hata hivyo, Ausilio amebainisha kwamba, miamba hao wa Serie A bado hawajapata ofa nzuri kwa ajili ya mchezaji wake huyo mwenye umri wa miaka 29, ambaye alifika fainali ya kombe la Dunia akiwa na timu yake ya taifa.

"Perisic anataka kuondoka, lakini hakuna ofa nzuri iliyotolewa," alisema Ausilio.

"Kama atabakia, natarajia atatulia. Tunatarajia kuendelea kupambana na naamini hakutakuwa na tatizo. Sidhani kama itachukua muda mrefu.

"Naweza kusema kwamba, soko la usajili kwa Inter limefungwa. Tulikuwa na tatizo la wachezaji kuwa fiti huku pengo la Sime Vrsaljko limezibwa haraka na ujio wa Cedric Soares kutoka Southampton.

"Inter ilikuwa na matatizo kidogo kwa miaka michache iliyopita, ikiwa imebadili wamiliki mara tatu, lakini sasa tumeimarika na mambo yanaonekana kwenda sawa."

## Guardiola ainyooshea mikono Liverpool



**MANCHESTER,** England

KIPIGO cha 2-1 kutoka kwa Newcastle 'kimemkata maini' kocha wa Manchester City, Pep Guardiola na kupunguza matumaini ya kuwa kinara wa Ligi Kuu ya England.

Kipigo hicho cha Jumanne usiku kiliwapa nafasi zaidi Liverpool kuendelea kujichimbia kileleni, ikifukuzia kuweka tofauti ya alama saba muhimu dhidi ya Manchester City inayowanyemelea.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mechi hiyo, Guardiola alisema kuwa ni muhimu kukubaliana na matokeo ya mpira wa miguu kwakuwa ni ushindani na kwamba unaweza kushindwa.


Alikiri kuwa kutokana na matokeo yao, kikosi chake kina mlima mrefu mbele yao kuifikia Liverpool.

"Ni ngumu. Ni kama hatuna faida ya wazi ya kupata ushindi lakini tunapaswa kuendelea. Tunapaswa kucheza michezo yetu na kufahamu tunachotakiwa kufanya," alisema Guardiola.

"Tulikuwa na nafasi leo (juzi) kupunguza tofauti ya alama za anayeongoza.. Unapokuwa nyuma unapaswa kushinda mechi zako, lakini hatukufanya hivyo," aliongeza.

Hata hivyo, kocha huyo hakutaka kuwatupia mzigo wa lawama wachezaji wake, badala yake aliamua kukumbushia jinsi ambavyo wamekuwa wakifanikiwa.

Jana Jumatano, Liverpool ilitarajiwa kucheza na Leicester City ambayo inashika nafasi ya 10 katika msimamo wa Ligi.




## *Juventus yamkatia tamaa Pogba*

**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus imevunja ukimya kuhusu tetesi za kutaka kumsajili tena kiungo wa Manchester United, Paul Pogba.

Tetesi za Pogba kurejea Juventus zilivuma zaidi wakati Jose Mourinho akiwa kocha wa Mashetani Wekundu hao wa Old Trafford, lakini zilianza kupungua baada ya Ole Gunnar Solskjaer kushika usukani akimpa nafasi ya kutosha nyota huyo wa Ufaransa.

Kiwango bora zaidi kilichooneshwa na Pogba katika wiki za hivi karibuni kimemuibua kocha wa Juve, Massimiliano Allegri ambaye amedai kuwa matumaini ya kumnasa tena mshambuliaji huyo yamefifia.

"Ni vigumu kumuona Pogba akiichezea Juventus tena," Allegri aliwaambia waandishi wa habari.

"Sitaki kujidanganya katika hili. Nadhani itakuwa vigumu sana kumuona Pogba akiwa ndani ya jezi ya Juventus," aliongeza.

Pogba alihamia Manchester United mwaka 2016 akitokea Juventus kwa dau la dola milioni 117 lililoweka rekodi ya dunia. Aliichezea Juventus tangu mwaka 2012 akiwa kijana mdogo.

Kaka yake, Florentin ameeleza kuwa kama ataondoka Manchester United, Pogba anaweza kuelekea kati ya timu tatu ambazo ni Manchester City, Real Madrid au Barcelona.

Januari 25, Manchester United ilipoichapa Arsenal 3-1, uwezo wa Pogba ulikuwa gumzo mitandaoni. Mwandishi wa habari nguli wa Uingereza, Piers Morgan, alichochea moto zaidi baada ya kumfananisha Pogba na Mesut Ozil wa Arsenal anayetajwa kuwa kati ya wachezaji bora zaidi duniani. Wengi hawakukubaliana naye.

## HABARI MICHEZO

# KOMPANY KUTOONGEZEWA MKATABA




**MANCHESTER,** England

NAHODHA wa klabu ya Manchester City, Vincent Kompany hatopewa mkataba mpya kwa mujibu wa kocha, Pep Guardiola.

Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 raia wa Ubelgiji unakamilika mwisho wa msimu huu .

Ameichezea klabu hiyo mara 14 msimu huu na sasa anauguza jeraha la misuli.

"Ni mchezaji mzuri, lakini ukweli ni kwamba katika kipindi cha miaka mitano iliopita amecheza mechi chache," amesema akinukuliwa na gazeti la Daily Mail.

"Kwa hiyo ndio hali tunayoweza kuweka mezani na klabu itajadiliana na wakala wake na kufanya uamuzi mzuri."

"Huwa tunapomkosa uwanjani. Yeye ni muhimu ni nahodha wetu na akiwa uwanjani anatupatia cha ziada ambacho mabeki wachache wa katikati duniani wanaweza kutoa."

Ripoti zaidi zinasema kwamba, kuwa City ilitaka kumpatia Kompany mkataba wa miezi 12, lakini hali yake ya majeruhi ndio ilizua wasiwasi.

Amecheza mechi tatu pekee tangu mwanzo wa Novemba huku mechi yake ya mwisho ikiwa ushindi dhidi ya Liverpool mnamo Januari 3. Kompany aliwasili katika klabu ya City mwaka 2008 kutoka klabu ya Hamburg ya Ujerumani.

# Lukaku: Mourinho anatakiwa kuheshimiwa

**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa klabu ya Manchester United na timu ya taifa ya Ubelgiji, Romelu Lukaku amefunguka na kutoa ya moyoni yanayomhusu aliyekuwa kocha wake, Jose Mourinho.

Mshambuliaji huyo amefunguka na kusema Mourinho anahitaji kupewa heshima yake hapo Manchester United kwa yale aliyoyafanya katika klabu hiyo.

Lukaku amesema; "Mourinho amefanya mambo makubwa na alihitaji heshima yake, kwani aliikuta Manchester United ikiwa katika nafasi ya 6 kwenye msimamo wa ligi na kuipandisha hadi nafasi ya pili.

"Lakini pia akiwa nafasi ya 6 alishinda mataji matatu likiwamo la Europa League."

Akizungumza na kituo cha Eleven Sport Lukaku ameongeza, "Mourinho alitegemea kujenga kitu kikubwa United, lakini mambo hayakuenda vizuri, naamini kwamba amefanya vitu vikubwa, hivyo kwa upande wangu namheshimu pia ni kocha aliyenisajili mimi."

Lukaku pia alimuongelea kocha wake wa sasa hivi, Ole Gunnar na kusema, "Solskjaer ndio anaanza sasa hivi, naamini kila kitu kitaenda vizuri nafikiri tutamaliza ligi katika nne bora na pia hata kushinda moja ya mataji tunayoshiriki."

Ikumbukwe kwenye ligi ya mabingwa Ulaya Manchester United watakutana na PSG Februari 12 na kwenye FA akipangwa na Chelsea baada ya kutupilia mbali Arsenal ambayo ndio mbabe wa michuano hiyo akitwaa mara 13.







# Rakitic: Nataka kubaki Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

IVAN Rakitic amesisitiza kwamba, anataka kubakia Barcelona na angependa kuongezewa mkataba wake, licha ya kuhusishwa na mpango wa kutakiwa na Chelsea.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 amekuwa na mafanikio makubwa na klabu hiyo tangu ajiunge akitokea Sevilla mwaka 2014, akishinda mataji 12, ukiwamo msimu alioshinda mataji matatu kwa pamoja ya LaLiga, Copa del Rey na Ligi ya mabingwa Ulaya ukiwa ni msimu wa 2014-15.

Hata hivyo, huku Frenkie de Jong akitarajiwa kuwasili hapo akitokea Ajax Julai mwaka huu kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 86, Rakitic amekuwa akihusishwa na uwezekano wa kuondoka hapo na kwenda Stamford Bridge mwishoni mwa msimu huu.

Barca kwa sasa wanapanga kupunguza kiwango cha mishahara pamoja na kuuza wachezaji na Rakitic, pamoja na Philippe Coutinho na Malcom, ni majina yanayotajwa kwamba watauzwa.

Lakini nyota huyo wa kimataifa wa Croatia hana mpango wa kuondoka Barca, akiliambia gazeti la Mundo Deportivo kwamba: "Ni swali zuri kwa bosi na rais. Watu wananijua mimi, wanajua kwamba nipo hapa kwa ajili ya kucheza.

"Nina umri wa miaka 30 na nafurahia mafanikio yangu ya uchezaji kwa sasa. Nataka kufurahia kucheza soka hapa Barca. "Nataka kuwa hapa, na kama nitaongeza mkataba hapa kwa miaka mingi nitafurahi zaidi na pia kushinda mataji zaidi na klabu hii."

# ONDOO SOKA
## M AGAZETI Y ILAYA




# SUAREZ ATUA ARSENAL, EMERY SASA AFUNGUKA

### ●●● Natumai baadhi ya wachezaji watakuwa pamoja nasi...

**LONDON,** England

KIUNGO wa Barcelona, Denis Suarez, atasaidia kutatua tatizo la mawinga Arsenal, kwa mujibu wa kocha Unai Emery, ambaye alisema pia anatumai Ainsley Maitland-Niles atakuwa fiti kuivaa Manchester City Jumapili.

**Suarez anajiandaa kujiunga na Arsenal kwa mkopo hadi mwishoni mwa msimu baada ya kukosa nafasi katika kikosi cha kwanza cha Barca chini ya Ernesto Va-l verde, lakini hakumudu kukamilisha uhamisho huo kwa muda ili kuiwahi mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Cardiff City ambayo 'Gunners' ilishinda 2-1 juzi usiku.**

Pia, Arsenal ilimkosa Maitland-Niles, ambaye alipata majeraha ya goti na kujiunga katika chumba cha matibabu na wachezaji wenzake Hector Bellerin, Sokratis na Laurent Koscielny.

Baada ya kushuhudia mabao kutoka kwa Pierre-Emerick Aubameyang na Alexandre Lacazette yakiisaidia Arsenal kupata ushindi dhidi ya 'Bluebirds' hao, Emery aliwaambia wanahabari: "Tunahitaji mawinga.

"Suarez, nani anajua, ana ubora huu." Alipoulizwa endapo Mhispania huyo mwenye umri wa miaka 25 atamudu mikikimikiki ya Ligi Kuu England, Emery alijibu: "Sijui kwa sasa.

"Ni changamoto kwake, na pia [ni changamoto kwake] kutusaidia sisi."

Wakati zikiwa zimebaki siku mbili [Jumanne] kabla ya dirisha dogo la usajili kufungwa, Emery hakuwa tayari kufunguka kuhusu kutua kwa sura mpya licha ya Arsenal kuhusishwa na winga wa Inter, Ivan Perisic.

Alisema: "Kama mchezaji anaweza kuja hapa kutusaidia, atakuja. Habari mpya nyingine, sijui. Akili yangu ni katika mechi. pengine usiku wa leo [juzi]ama kesho [jana] nitazungumza."

Akitazama kuhusu safari ya Jumapili kuelekea Etihad kuwavaa mabingwa watetezi wa EPL, Man City, kuhusu waliopo chumba cha majeruhi kurejea, Emery alisema: "Sijui kwa sasa. Tunahitaji kujua kesho [jana] katika mazoezi.

"Natumai baadhi ya wachezaji watakuwa pamoja nasi. Ainsley [Maitland-Niles], natumai."

Wakati huo huo, kocha wa Barcelona, Ernesto Valverde amemtakia Denis Suarez kupata mafanikio mema na Arsenal, wakati uhamisho wake ulitarajiwa kukamilika jana.

"Ninajua Denis alikuwa katika hali hili. Bado haijawa rasmi na tunahitaji kusubiri kidogo," Valverde aliuambia mkutano wa wanahabari Jumanne wakati alipoulizwa kuhusu taarifa ya Arsenal kumsajili.

"Ilikuwa ni uwezekano kwamba kila mtu ana thamani, na tunatumai mambo yatakwenda vizuri."

## ZISIKUPITE

### GUEYE AZIVUTA ARSENAL, CITY

ARSENAL na Manchester City wamejiunga katika mbio za kumsajili kiungo wa Everton, Msenegal Idrissa Gueye, 29. ***(Sky Sports)***

### CHRISTENSEN AZIVUTIA JUVE, BD

BORUSSIA Dortmund na Juventus zinavutiwa kumsajili beki wa Chelsea, Andreas Christensen, 22, lakini 'Blues' wanataka pauni milioni sita kama ada ya kumtoa kwa mkopo. ***(Sun)***

### TIELEMANS AGOMBEWA EPL

ARSENAL, Tottenham, West Ham na Newcastle United zote zimetoa ofa kwa kiungo wa Monaco, Youri Tielemans, 21, ya kumsajili kwa mkopo. ***(Star)***

### HUDSON-ODOI APIGWA PINI

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri amesema winga Callum Hudson-Odoi, 18, ambaye amewasilisha maombi ya kuondoka, anapaswa "kuiheshimu" shule yao ya vipaji na kuendelea kujiendeleza katika klabu hiyo. ***(Guardian)***

### ARSENAL YAITIWA PERISIC

ARSENAL imekuwa ikihusishwa na kumsajili winga wa Inter Milan, Ivan Perisic, lakini klabu hiyo ya Italia imesema haijapokea ofa "yoyote ya kuvutia". ***(Mail)***

### YAKWAMA KWA LOOKMAN

EVERTON imekataa ombi la AC Milan la kumsajili mshambuliaji wao, Ademola Lookman, 21, lakini klabu hiyo ya Italia inaweza kurejea na tena na ofa yao. ***(Mirror)***

### JOVIC KUMRITHI BENZEMA REAL

REAL Madrid inamuwinda straika wa Eintracht Frankfurt, Luka Jovic, 21, - kutoka kwa Benfica - kama mbadala wa muda mrefu wa Mfaransa Karim Benzema. ***(AS)***

### KAKA POGBA KUTUA ATLANTA

KAKA wa Paul Pogba, Florentin, 28, anajiandaa kujiunga na Atlanta United katika Ligi Kuu ya Marekani (MLS) na kuungana, hivyo kwa mara nyingine tena kuwa chini ya Frank de Boer. ***(L'Equipe)***

### LIVERPOOL KUMNASA OMUR

LIVERPOOL inahusishwa na kutoa ofa ya kumsajili kiungo wa Trabzonspor, Abdulkadir Omur, 19, ambaye anazivutia klabu nyingi za Ulaya. ***(iNews)***

### NEWCASTLE , SAMARIS WATETA

NEWCASTLE United ipo katika mazungumzo na kiungo Andreas Samaris, 29, ikitaka kumsajili kwa mkopo kutoka Benfica. ***(Chronicle)***

### YAMTAKA ELABDELLAOUI

SOUTHAMPTON ipo katika mazungumzo na Olympiakos kuhusu dili la kumsajili beki Mnorway, Omar Elabdellaoui, 27. ***(Sun)***

### DJU KUTUA WEST HAM

WINGA kinda wa Benfica, Mesaque Dju, 19, anajiandaa kujiunga na West Ham kwa uhamisho huru. ***(Sky Sports)***

## Kosuri aahidi makubwa TFF

**Na Mwandishi Wetu**

MGOMBEA wa nafasi ya Ujumbe wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF-Kanda ya Simiyu na Shinyanga), Kosuri Osuri, amesema kuwa endapo atachaguliwa katika cheo hicho atahakikisha programu za maendeleo zitatekelezwa ili malengo ya kukuza kiwango cha timu zote za hapa nchini yanatimia.

TFF inafanya uchaguzi mdogo wa kanda hiyo ili kujaza nafasi iliyoachwa na Mbasha Matutu ambaye alisimamishwa na shirikisho hilo kwa kosa la udanganyifu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kosuiri, alisema kuwa anaamini ana uwezo wa kusaidia maendeleo ya soka nchini endapo atapata ridhaa ya kuingia katika kamati hiyo ya TFF.

Kosuri alisema kuwa anawaomba wajumbe wa mkutano mkuu kumchagua kwa sababu anafahamu vyema changamoto zinazovikabili vyama vya wilaya na mikoa yote ya Tanzania Bara kutokana kupata nafasi ya kutembelea mara kwa mara.

"Napenda kuwaomba wajumbe wasisite kunipa kura zao, zitawalipa, ninajua kiu waliyonayo na hili linatokana na uzoefu nilionao," alisema Kosuri ambaye anatoka Simiyu na pia ni kamisaa wa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wagombea wengine wanaowania nafasi hiyo ni pamoja na Bannister Lugola, Joseph Bihemo na Kajanja Mugengere.

## ZFA yajipanga kuwanoa madaktari

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

CHAMA cha Soka Zanzibar (ZFA), kinatarajia kutoa mafunzo kwa madaktari wa klabu zinazosimamiwa na chama hicho ili kuwapa uelewa zaidi kwa ajili ya kutoa huduma bora katika timu zao, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Ufundi wa ZFA, Salum Ali alisema mafunzo hayo yatafanyika kesho kwenye Ukumbi wa Uwanja wa Amaan na madaktari watakaoshiriki ni wa timu za Ligi Kuu Zanzibar, Ligi Daraja la Kwanza Kanda pamoja na Ligi Daraja la Pili Taifa. Ali alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwaongezea uwezo katika kazi zao huku pia wapo baadhi yao wanafanya kazi hiyo bila kuwa na vyeti sahihi na badala yake wanatumia uzoefu.

Alisema kupitia mafunzo hayo, ZFA itapata fursa ya kujua idadi kamili ya madaktari wa michezo waliopo Unguja, huku utaratibu kama huo pia ukiandaliwa kuwafikia wataalamu hao waliopo Kisiwani Pemba.

Hata hivyo alikitaka Chama cha Madaktari wa michezo Zanzibar ( ZASMA) kuwasilisha orodha ya wanachama wao ili wajitokeze kwa wingi katika mafunzo hayo ambayo yana umuhimu mkubwa katika afya za wachezaji.

# KIEMBA AIONDOA SIMBA KIMATAIFA

**Na Somoe Ng'itu**

KIUNGO wa zamani wa Simba, Amri Kiemba, amekitaka kikosi cha Simba kuongeza nguvu zake katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ili waweze kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika hapo mwakani.

**Simba iliondoka nchini juzi kuelekea mjini Alexandria, Misri kuwavaa wenyeji Al Ahly katika mechi ya Kundi D itakayochezwa kesho kuanzia saa 4:00 kwa saa za Tanzania.**

Kiemba aliliambia gazeti hili kuwa ni wazi kuwa Simba ina nafasi ndogo ya kusonga mbele katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kutokana na aina ya wachezaji walionao na timu wanazopambana nazo kwenye hatua ya makundi.

Kiungo huyo alisema kuwa anaamini huu ni wakati sahihi kwa mabingwa hao watetezi kujipanga upya kwa ajili ya kushinda mechi zao zote za Ligi Kuu Tanzania Bara na kueleza kuwa mlengo yao kwa mwaka huu yalitimia.

"Malengo ya Simba yalikuwa ni kutinga hatua ya makundi, na hilo walifanikiwa, sasa kusema wanataka kuchukua ubingwa wa Afrika kwa sasa ni ngumu, inachotakiwa kufanyika ni kusaka nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa mwakani, nafasi yetu sasa ni kuhakikisha tunazoeleka kucheza hatua ya makundi," alisema kiungo huyo ambaye pia aliwahi kuichezea Yanga.

Aliongeza kuwa timu za Tanzania zinatakiwa kujiimarisha zaidi katika idara ya ufundi kama wanavyofanya klabu nyingine kwa kuwachunguza wapinzani kabla ya kukutana nao.

"Kwa mfano nilipokuwa Yanga, Micho (Sredojovic Milutin) alikuwa akimwachia programu kocha msaidizi na kusafiri kwenda kuwaangalia wapinzani na baadaye kuja kutueleza namna ya kuwakabili na kwa kiasi fulani tulifanikiwa, timu nyingine zinatanguliza mashabiki ambao hawawezi kutueleza kiufundi vitu vya kufanya," Kiemba alisema.

Mechi nyingine ya kundi hilo kati ya AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo dhidi ya JS Saoura ya Algeria pia itachezwa kuanzia saa 1:00 usiku mjini Kinshasa.



Kiungo wa Manchester United, Paul Pogba, akipambana kumiliki mpira dhidi ya wachezaji wa Burnley kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa katika Uwanja wa Old Trafford juzi na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2. **PICHA: MTANDAO**

# *Azam kupambana mwanzo mwisho*

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kufanikiwa kusonga mbele katika mashindano ya Kombe la FA, uongozi wa Azam FC umesema kuwa utapambana "mwanzo mwisho" katika mashindano hayo kwa sababu inataka kulinyakua taji la michuano hiyo mwaka huu.

Azam FC imesonga mbele katika mashindano ya Kombe la FA ambalo bingwa wake huiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa kuwafunga Pamba ya Mwanza mabao 2-0.

Mbali na taji hilo, pia Azam FC inajipanga kuhakikisha inatwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao unashikiliwa na Simba ya jijini Dar es Salaam.

Afisa Habari wa Azam FC, Jaffer Iddi, aliliambia gazeti hili kuwa mashindano hayo ni magumu lakini wachezaji wao wamejipanga kuongeza umakini na nidhamu ili waweze kupata ushindi katika kila mechi watakayoshuka uwanjani.

"Mashindano ya Kombe la FA ni magumu sasa, ila tunashukuru tumefanikiwa kutimiza ahadi yetu, tumesonga mbele, pia tunajua tuna kibarua kigumu katika Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini tunasema hakuna kulala," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kuwa tayari kikosi chao kimeshaanza mazoezi kwa ajili ya kuwakaribisha Allinace FC ya Mwanza katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Februari 6 mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini.

Micheo

Alhamisi Januari 31, 2019

Nipashe



Suarez atua Arsenal, Emery afunguka

HABARI UK. 30




Kipa wa Arsenal, Bernd Leno, akijitanua kumzuia Bobby Reid wa Cardiff kufunga bao katika kipindi cha kwanza kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi na wenyeji kushinda mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# Simba mikononi salama Misri

## ●●● Ubalozi wa Tanzania waipokea, waipa darasa la kuivaa Al Ahly Jumamosi huku...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kikosi cha Simba kimetua salama nchini Misri kwa ajili ya kuwavaa wenyeji Al Ahly katika mechi ya Kundi D ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa Jumamosi, uongozi wa timu hiyo umesema umejipanga vema kwa ajili ya mchezo huo utakaochezwa kwenye Uwanja wa Borg El Arab uliopo mjini Alexandria, licha ya kulia kukabiliana na baridi kali.

Akizungumza na Nipashe, Afisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, alisema wachezaji wote wako katika hali nzuri na jana jioni walitarajia kuanza programu ya mazoezi kuelekea mchezo huo wa raundi ya tatu.

Magori alisema hii si mara ya kwanza kwa Simba kwenda Alexandria, hivyo walijiandaa kuepuka changamoto na "hujuma" kutoka kwa wenyeji wao.

**"Tuko poa, tuko vizuri, kila kitu kitakwenda vema," alisema kwa kifupi Magori.**

Kuhusu hali ya hewa ya baridi, Magori alisema kuwa tayari walishajiandaa kukutana na hali hiyo baada ya kupata taarifa kutoka kwa ujumbe waliotangulizia nchini humo.

Kikosi hicho jana kilipokelewa na Balozi wa Tanzania nchini humo, Issa Suleiman Nassor, ambaye aliwaambia wachezaji wa Simba wajiandae kukabiliana na hali ya baridi iliyoko nchini humo.

Balozi Nassor alisema kuwa anawaamini Simba watafanya vizuri katika mchezo huo wa tatu kutokana na mazoezi waliyofanya na uzoefu walionao wachezaji wake.

"Siifahamu vema Al Ahly, lakini sio timu mbaya, ni mategemeo yangu mtafanya vizuri, mnajiamini sana, naamini mtaibuka na ushindi, niwaambie tu machache, kwa sasa ni baridi, ni vema mkajihifadhi, mwombeane mazuri, mjue mnaiwakilisha Tanzania," alisema balozi huyo ambaye aliahidi kwenda uwanjani kuwashangilia.

Simba imeenda Misri huku ikiwa na kumbukumbu ya kichapo cha mabao 5-0 ilichopata kutoka kwa AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia Kongo katika mchezo uliopita wa mashindano hayo.

# Yanga yampigia hesabu Amri Saidi

**Na Somoe Ng'itu**

REKODI ya Kocha Mkuu wa Biashara United, Amri Saidi, ni moja ya sababu zilizoifanya Yanga kuongeza umakini katika mechi ya raundi ya nne ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya timu hiyo kutoka Mara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Mechi hiyo ambayo awali ilitarajiwa kuchezwa jana, itaanza saa 1:00 usiku kwenye uwanja huo wenye uwezo wa kuingiza mashabiki 60,000.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa Yanga, Hafidh Saleh, alisema maandalizi kwa ajili ya mchezo huo yamekamilika na Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera, anafuraha kuona wachezaji wake wa kikosi cha kwanza waliokuwa majeruhi wamepona na wameongeza nguvu katika kikosi chake.

Saleh alisema kila mechi kwao ni sawa na fainali na wanafahamu ugumu wa mchezo huo ambao atakayefungwa, atakuwa ameiaga michuano hiyo.

"Tuko vizuri, tunaendelea kujipanga kuhakikisha hatufanyi makosa, tunamuomba Mungu atusaidie kutimiza malengo yote tuliyonayo msimu huu, wachezaji wengi waliokuwa majeruhi wamepona isipokuwa Jafary Mohamed na Baruan Akilimali ndio watakaukosa mchezo wa kesho (leo)," alisema mratibu huyo.

Aliongeza kuwa wachezaji wao wana morali ya kupambana katika kila mchezo na ushindani wa kuwania namba kati ya wachezaji wakongwe na vijana unasaidia kukifanya kikosi chao kuendelea kuimarika. Naye Saidi alisema kuwa, amekiandaa kikosi chake kutowaogopa Yanga na kucheza kwa umakini katika muda wote.

Baada ya mechi ya leo, kikosi cha Yanga kitaanza safari ya kuelekea Tanga kuwafuata Coastal Union kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini humo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >